# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

## Kikao cha Hamsini – Tarehe 19 Juni, 2017

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe.* Mussa Azzan Zungu*) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 408

### Kufutwa kwa Ushuru mdogo mdogo unaokusanywa na Halmashauri

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA (K.n.y. MHE. DEO K. SANGA)** aliuliza:-

Serikali iliahidi kufuta Ushuru mdogo mdogo unaokusanywa na Halmashauri ili wajasiriamali wadogo wakiwemo akina mama lishe waweze kuongeza kipato kupitia shughuli zao.

Je, ni lini Serikali itatoa tamko rasmi kwa Halmashauri zetu nchini ili wasikusanye tena ushuru huo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyanda Sanga, Mbunge wa Makambako kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefuta ushuru na tozo ambazo zilikuwa zinatozwa kwa wafanyabiashara wadogo wadogo wasio rasmi na wanaofanyia biashara katika maeneo yasiyo rasmi mfano Mama Lishe, wauza mitumba wadogo wadogo, wauza mazao ya kilimo wadogo wadogo kama mboga mboga na ndizi na matunda isipokuwa biashara za migahawa na maduka na wale ambao wako kwenye maeneo rasmi. Vilevile wafanyabiashara wadogo walio nje ya maeneo maalum ya kibiashara wenye mitaji chini ya shilingi 100,000 hawatatozwa ada, kodi na tozo zozote. Kodi nyingine zilizofutwa ni ushuru wa huduma *(service levy)* kwenye nyumba za kulala wageni, ada za vibali vinavyotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zilikuwa zinatozwa na *TFDA, OSHA, Fire* na Bodi ya Nyama na ada ya makanyagio.

Serikali pia imepunguza ushuru wa mazao kutoka asilimia tano haid asilimia mbili kwa mazao ya chakula na asilimia tatu kwa mazao ya biashara. Aidha, mazao yanayosafirishwa kutoka wilaya moja hadi nyingine yasiyozidi tani moja hayatatozwa ushuru wa mazao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mgimwa.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuipongeza sana Serikali kwa majibu mazuri lakini nina swali la nyongeza.

Pesa hizi zilizokuwa zinakusanywa na Halmashauri zilikuwa zinasaidia kazi ndogo ndogo kwenye zile Halmashauri. Namuomba Mheshimiwa Naibu Waziri atuambie Serikali imepanga vipi kuhakikisha inaziba hilo *gap?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Halmashauri mwanzo zilikuwa zinajielekeza kwa kukusanya tozo hizi ambazo zilikuwa zinasaidia katika kuendesha Halmashauri. Nadhani hiki kilikuwa ni kilio cha Watanzania wote, ambao Watanzania wadogo wadogo kule chini ilikuwa inapigwa kelele sana ndio maana Serikali sasa imeomua kulichukua hili na Wizara ya Fedha hapo alipoweka hotuba yake hapa nilizungumza hili wazi. Kwa hiyo, naomba tukifika katika *Finance Bill* mtaona jinsi gani Serikali imejipanga na ku-*address* jambo hilo vizuri kwa mustakabali wa Halmashauri zetu unavyoenda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mweyekiti, nakushukuru, pamoja na Serikali kuamua kuondoa tozo hizo tayari Halmashauri zilishaweka kwenye bajeti zao. Je, Serikali inatoa tamko gani ama wata-*review* hizo bajeti au itakuwaje? Hiyo ndiyo shida yangu ahsante na shida kwenye Halmashauri zetu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hii ni hofu ya Wabunge wengi humu ndani, na hata juzi Wabunge wengi walikuwa wananiuliza kule kwamba jinsi gani tunavyokuja. Na ndiyo maana naomba niwaambie kuwa Serikali itakachokifanya sasa hivi ndiyo maana nimesema tukifika katika *Finance Bill* tutaona jinsi gani mchanganuo utakavyokwenda. Lengo kubwa kwa sababu Halmashauri zimeshatenga bajeti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia bajeti ya Halmashauri ilivyotengwa kuna tofauti sasa na kama ambavyo vingine viliwekwa kama ni vyanzo vya mapato katika Halmashauri hiyo. Ndiyo maana Wizara ya Fedha itakapohitimisha mijadala hii tutaona ni jinsi gani mafungu hayo yatawekwa vizuri. Lengo kubwa bajeti ya Halmashauri

kama *property tax* ilivyowekwa katika suala la majumba, kwa hiyo, msihofu katika hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kaunje tunaendelea. Mheshimiwa Hassan Seleman Kaunje.

Na. 409

**Changamoto zinazoikabili Hospitali ya Rufaa ya Sokoine – Lindi**

**MHE. HASSAN S. KAUNJE** aliuliza:-

Hospitali ya Rufaa ya Sokoine Mkoani Lindi inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ukosefu wa maji na ubovu wa vyoo katika wodi zake, pia watumishi wa hospitali hiyo wamekuwa na lugha na huduma duni zinazokera wateja.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto zinazoikabili hospitali hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS,TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Seleman Kaunje Mbunge wa Lindi Mjini kama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutatua changamoto zinazokabili Haspitali ya Mkoa wa Lindi zikiwemo uchakavu wa miundombinu, katika mwaka wa fedha 2016/2017 iliidhinishiwa kiasi cha shilingi miioni 344 kwa ajili ya kazi ya ukarabati wa miundombinu ambapo fedha zote zimepelekwa.

Vilevile Mkoa umepanga kutumia shilingi milioni 185 kwa ajili ya kujenga kichomea taka *(incinerator)* ya kisasa na ukarabati wa hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kazi zinazoendelea hivi sasa ni ukarabati wa wodi ya wazazi, wodi ya upasuaji wa wanaume na aidha, katika kutatua tatizo la maji Serikali inakamilisha mradi mkubwa wa maji katika eneo la Ng'apa, Manispaa ya Lindi unaotarajiwa kumaliza kabisa tatizo la maji katika Manispaa ya Lindi. Wodi ya daraja la I. Aidha, mkandarasi atakayejenga kichomea taka ameshapatikana ili kuanza kazi hiyo. Vilevile Serikali ipo katika hatua za mwisho ya kupata mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa wodi ya watoto, jengo la upasuaji *(theatre)* jengo la huduma ya afya ya kinywa na meno na jengo la huduma ya macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imepanga kukarabati wodi ya wagonjwa ya akinamama, chumba cha mionzi na jengo la utawala. Ukarabati wa miundombinu utafanyika sambamba na uboreshaji wa mfumo wa maji safi na maji taka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kaunje.

**MHE. HASSAN S. KAUNJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri nina maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza Serikali ya Awamu ya Nne ilitoa ahadi ya kujenga kituo cha Afya katika kata ya Mnazi Mmoja. Ahadi hii ilikuwa ina inataka kutekelezwa na Serikali Kuu, mpaka tunapozungumza hakuna chochote kinachoendelea ikiwa ni mwaka wa saba sasa. Nini kauli ya Serikali kuhusu jambo hilo?

Swali la pili, wananchi wa Lindi tuliwahamasisha waanze kujenga vituo vya afya katika kata zao. Wamepata maelekezo kutoka TAMISEMI ya kwamba vituo hivyo visimame kujengwa kwa muda mrefu mpaka sasa. Nini kauli za Wizara dhidi ya watu wale ambao wameamua kujitolea kuweza kujenga vituo vile vya afya? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ya Serikali kama zilivyo ahadi zingine na nikifahamu sehemu ya Mnazi Mmoja ni *juction ya population* kubwa na imetolewa ahadi hii takriban miaka saba, nikijua kwamba kuna juhudi zimeshaanza pale. Naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali naomba ihamasishe Halmashauri yako muanze kuibua jambo hili vizuri halafu na sisi tutaliratibu vizuri. Naomba nikuambie Serikali itakupa ushirikiano wa kutosha lengo letu ni kwamba *commitment* ya Serikali ya ahadi zote zilizotolewa na viongozi wetu wa Kitaifa tunaenda kuzitekeleza.

Kwa hiyo, naomba nikusihi Mheshimiwa Mbunge katika mchakato huu bajeti utakao kuja sasa tuliweke hili vizuri ili na sisi tutalipa nguvu, lengo kubwa kituo cha afya tuweze kukitengeneza katika eneo lile. Jambo la hivi vituo vya afya vingine ambavyo wananchi wameanza ujenzi nikijua kwamba *commitment* ya Serikali ni kuwahamazisha wananchi katika suala zima la ujenzi wa afya. Kama vituo hivyo ni vipya vinaendelea basi naomba niseme kwamba tutaendeleza kuvihakikisha tunavipa nguvu. Lakini nikijua kwamba kuna utaratibu ambao wakati mwingine umejitokeza kuna utaratibu wa kubadilisha zahanati kuwa kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Ofisi yetu sasa ilitoa maelekezo kama hizi zahanati tuziache ziwe zahanati lakini tujenge vituo vipya viwe vya afya. Lakini kwa sababu Bwana Kaunje jambo hili umelileta hapa naomba nikuhakikishie kwamba ofisi yetu itakupa ushirikiano wakutosha kuangalia *scenario* ipi iliyoko kwenye Manispaa ya Lindi tuweze kusaidiana kwamba wananchi waweze kupata huduma kutokana na hali halisi ilivyo pale kwako Lindi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Nape.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa katika jitihada za kupunguza mzigo mkubwa unaobebwa na Hospitali ya Lindi, Serikali iliingia makubaliano na hospitali za *mission* kwa mfano Hospitali ya Nyangao pale Jimbo la Mtama kwa ajili ya kusaidiana nao katika kutoa huduma za afya ili tupunguze mzigo mkubwa katika Hospitali ya Lindi. Lakini utekelezaji wa makubaliano hasa upelekaji wa fedha na watumishi kwa ajili ya kufanya kazi katika hospitali hizi ambazo mmekubaliana nazo hautelekezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali sasa itaanza kupeleka pesa kama walivyokubaliana pamoja na watumishi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nape, naomba tulichukue hilo kwa sababu kuna hizi ahadi najua kwamba katika hospitali mbalimbali zinatekelezeka na nikijua kwamba kweli kuna shida kubwa na ndiyo maana kutokana na kesi ile ya kwako tumeona kwamba pale Kituo cha Nyangarapa ambao kituo cha afya kwenda kukiboresha zaidi kama tulivyokubali pale mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tutaenda kukiboresha kituo hiki lakini suala zima la *commitment* za hizi taasisi ambazo za dini au vituo mbalimbali vya dini au vituo mbalimbali binafsi ambao Serikali imeingilia nazo, kama kuna *scenario* ambayo kwa Wakilindi iko tofauti kidogo upelekaji wa fedha hauko vizuri tunakwenda kuufuatilia kuangalia jinsi gani tuuboreshe wananchi waweze kupata huduma vizuri.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea, Ofisi ya Makamu wa Rais Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis.

Na. 410

**Uharibifu wa Mazingira na Athari zake nchini**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Uharibifu wa mazingira nchini umeleta athari kubwa ya mabadiliko ya msimu wa kilimo, uhaba mkubwa wa maji na kukauka kwa vyanzo vya maji nchini.

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani za makusudi za kudhibiti uharibifu huo wa mazingira hasa katika ukataji wa miti?

(b) Je, Serikali inasema nini juu ya kupanda miti katika mashamba ya Serikali na ya watu binafsi ili kusaidia kuondoa hali hii?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira zinazolikabili taifa hili, Serikali imechukua hatua zifuatazo; kuwachukulia hatua kali za kisheria wale wote wanaokamatwa wakikata miti bila vibali kwa mujibu wa Sheria, kutoa elimu ya mazingira kwa umma ili kuongeza uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira hasa misitu na kuhamasisha wananchi kutumia nishati mbadala kama gesi na umeme pamoja na matumizi ya majiko banifu ili kupunguza matumizi ya mkaa na kuni.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeandaa mkakati wa Taifa wa kupanda na kutunza miti unaolenga

kuhamasisha upandaji miti katika maeneo ya mashamba na viwanja vilivyo wazi, ikiwemo mashamba ya Serikali na watu binafsi ili kudhibiti hali ya uharibifu wa ardhi nchini. Katika kufanikisha mkakati huu jamii wadau mbalimbali watahusishwa katika utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati umeweka muundo wa kitaasisi wa utekelezaji unahosisha wadau wote ikiwemo Wizara za Kisekta na Idara nyingine za Serikali, asasi zisizokuwa za kiserikali, asasi za kiraia, vijiji, shule, taasisi za dini na sekta binafsi. Kupitia mkakati huu, Serikali imepnga kupanda miti katika hekari laki 185,000 kila mwaka ambazo ni sawa na miti milioni 280. Mkakati huu utatekelezwa ipasavyo na utapunguza uharibifu wa misitu na urejeshaji wa uoto nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fakharia.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kuwa uaharibifu wa mazingira ni janga kuu nchini.

(a) Je, Wizara inasema nini katika kutoa motisha kwa wale wenye maeneo yaliyotunzwa na kuhifadhiwa vizuri miti?

(b) Je, idara ya hali ya hewa imejipangaje katika kuhabarisha umma sambamba na mabadiliko ya tabia nchi ambayo yanaenda kwa kasi hapa nchini? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza anasema ni motisha gani ambayo inatolewa kwa watu ambao wanajitolea katika kupanda miti na kufanya shughuli za biashara hii ya miti kama Wizara na kama taasisi za Serikali. Motisha tunazotoa tunatoa katika taasisi mbalimbali kwa mfano Wakala wa Misitu. Wakala wa Misitu amekuwa akitoa motisha wa kusaidia vikundi vinavyozalisha miti na vinavyopanda miti katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyowahi kuzungumza hapa kwamba kwa sasa hivi tumefanikiwa Wakala wa Misitu sasa yuko kila wilaya na katika kazi moja ambayo tumewaekeza ya kufanya ni kuhakikisha kwamba wanapokuwepo pale wanatengeneza miche kati ya laki moja mpaka laki tano na wanagawia wananchi. Pili, wanasaidia vikundi vinavyozalisha miti na tatu wanawasaidia wananchi wanaotaka miti ya aina mbalimbali pamoja na kuwapa mafunzo au aina ya miti inayofaa kulingana na eneo fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusu hali ya hewa sisi sote hapa ni mashahidi. Taasisi hii inayoshugulika na suala la utoaji wa hali ya hewa wamekuwa wakitujulisha kila wakati juu hali ya mvua kwa kila wakati na kila kipindi kwahiyo kati ya taasisi ambayo inafanya vuziri sana na mimi nachukua nafasi hii kuipongeza sana kwa sababu imekuwa ikitupa taarifa kila wakati, mwenendo wa wa mvua zilivyo, upungufu wa mvua ulivyo na jinsi ya wananchi wanavyotakiwa kuchukua hatua kulingana na hali inavyojitokeza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy atafuatiwa na Mheshimiwa Yussuf.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante leo ni karibu siku tatu *BBC* inatangaza kuhusu Ziwa Tanganyika kuathiriwa na kukata miti, na kutoweka samaki. Je, Serikali ina mpango gani kuzuia na kusaidia kuzungumza na nchi ya *DRC* Kongo, Burundi na Zambia ili kujenga kibanio katika mto Luguga ili maji yasiishe katika Ziwa Tanganyika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tutakachofanya tutafanya tadhimini ili tuone hasa ambacho kinasababisha upungufu wa samaki pamoja na uharibifu wa mazingira unaofanyaika katika Ziwa Tanganyika ili tuweze kujua hasa hatua stahiki tunazotakiwa kuchukua ili kuweza

kurejesha hali hii, na katika kufanya hivyo ushauri alioutoa Mheshimiwa Keissy tutauzingatia baada ya kuwa tumefanya uhakiki na kubaini yawezekana zipo *factors* nyingine ambazo hazifahamiki kwa sasa. Kwa hiyo, zitafahamika tu pale ambapo tutafanya tadhimini na kujiridhisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Yussuf.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru vyanzo vya maji vinaendelea kuathirika, na kupotea siku hadi siku nchini.

Je, Serikali imeanzisha vitalu vya miti inayotunza maji ili kuipanda na kuitunza kwenye vyanzo vya maji ili vyanzo vyetu vizidi kukua na kutoathirika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Halmashauri pamoja na taasisi zingine kukosekana kwa wataalam wanaotuelekeza aina ya miti ya kupanda na wapi. Ndiyo tukasema *TFS* lazima iwepo kila sehemu, kwa sasa hivi huyu wakala wa misitu ndiye anayetoa ushauri wa miti aina gani inafaa kupandwa eneo gani, eneo la vyanzo vya maji linafaa kupandwa miti ya aina gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge huduma hizi zote mtazipata sasa kila Wilaya kwa kila Ofisi ya Wakala ya Misitu ambaye anatoa maelekezo haya.

Lakini Wakala hawa watai-*guide* vizuri sana halmashauri kuhakikisha kwamba inavipitia vile vyanzo vyote vya maji na kuenda kupanda miti inayofaa katika kulinda vyanzo vya maji.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea muda wetu, Wizara ya Mambo ya Ndani Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi.

Na. 411

**Utaratibu wa *Visa on Entry***

**MHE: RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Tanzania imeridhia na kuingia mikataba mbalimbali ya kimataifa ikiwemo diplomasia na mahusiano.

Je, ni nchi ngapi na zipi ambazo Watanzania wanaweza kuzitembelea moja kwa moja kwa utaratibu wa *visa on entry* wakati wa kuingia ukiondoa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maelezo kwa kuwa *visa* ni ruhusa inayoambatana na masharti ambayo hutolewa na nchi husika ili kuwaruhusu raia wa kigeni kuingia, kuondoka au kuwepo nchini katika muda maalum. Ruhusa hiyo inapotolewa katika vituo vya kuingilia nchini inajulikana kama *visa on arrival.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa utoaji *visa on arrival* uko katika sura ya makubaliano ama mikataba baina ya nchi na nchi au taratibu zinazotokana na matengamano na ushirikiano wa kimataifa na kikanda. Utaratibu huu unaweza kubadilika kulingana na mahusianao na hali ya usalama kati ya nchi na nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo nchi 16 ambazo Watanzania wanaweza kuzitembelea katika utaratibu wa *visa on arrival*. Nchi hizo ni Benin, Burkina Faso, Cape Verde, Cote d’voire, Djibout, Gabon, Gambia, Ghana, Guinea, Guinea – Bessau, Liberia, Mali, Mauritania, Niger, Sierra Leone

na Togo. Pamoja na utaratibu huu wa *visa on arrival,* pia zipo nchi 67 duniani ambazo Watanzania wanaweza kuzitembelea bila hitajio la *visa.*

**MWNEYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante, majibu ya Wizara yanaonekana ni mepesi sana kwa sababu nchi nyingi anazozitaja ni nchi za kiafrika na lengo mahususi ya hili swali tulikuwa tunataka tujue nchi zote ulimwenguni lakini natambua kwamba nchi zilizopo chini ya Umoja wa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa jielekeze kwenye swali.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Nchi zilizopo chini ya Umoja wa Madola *(Commonwealth)* tuna utaratibu huu wa *visa on entry or visa on arrival.* Je, kwa nini wananchi wa India wanapokuja Tanzania wanakuja kwa *visa on arrival,* lakini sisi tunapokwenda nchi kama India lazima uombe *visa* hasa ikichukuliwa kwamba Watanzania wengi wanakwenda India kwa ajili ya kupata huduma za matibabu?

Swali la pili, zipo nchi za Afrika Magharibi ambazo wanaingia kwa *visa* ya *referred visa* ikiwemo Cote d'voire, Senegal na Mali. Je, kwa nini sasa isiwe ni wakati muafaka wa kuiunganisha Nigeria katika nchi hizi kwasababu inaonekana kwamba mara nyingi wanapoingia huku kwetu wanahatarisha usalama wa nchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nchi za Jumuiya ya Madola zina utaratibu wa wananchi wake kutembeleana bila *visa.* Lakini kama nilivyojibu katika swali langu la msingi kwamba ushirikiano na matengamano hayo ikiwemo la Jumuiya ya Madola, utaratibu wake unaweza kubadilika kulingana na mahusiano pamoja na hali za kiusalama. Kwa hiyo, sio jambo la kushangaza kuona India na Nigeria juu ya kwamba zote

mbili ni wanachama wa Jumuiya ya Madola lakini utaratibu wa *visa on arrival* ukawa hautumiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea kwa Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Halima Ali Mohammed.

Na. 412

**Kuwekeza Kwenye Tafiti za Kilimo**

**MHE. HALIMA ALI MOHAMMED** aliuliza:-

Tanzania ina dhamira ya kuwa nchi ya uchumi wa kati kwa kujikita katika uchumi wa viwanda; na viwanda vinategemea sana ukuaji wa sekta ya kilimo kwa ajili ya kupata malighafi.

Je, Serikali imewekeza kiasi gani cha fedha kwa ajili ya utafiti wa kilimo *(agricultural research)* ili kufanya tafiti za kilimo kubaini changamoto zinazodumaza kilimo nchini na kutoa ushauri kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji wa kilimo na hivyo kukuza sekta ya viwanda?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima Ali Mohammed, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa kilimo hapa nchini una lengo kuu la kugundua mahitaji halisi ya mkulima na walengwa wengine. Utafiti wa kilimo hufanywa kupitia vituo 16 vya utafiti vya umma vilivyopo katika kanda mbalimbali na taasisi za utafiti binafsi kama vile Taasisi ya Kahawa *(TaCRI)*, Chai *(TRIT)* na Tumbaku *(TORITA)*. Serikali imeanza kuboresha mfumo wa utafiti wa kilimo kufuatia kuanzishwa kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo *(Tanzania Agricultural Research Institute – TARI)* ili kuboresha zaidi uzalishaji wa mazao. Taasisi hii ndiyo itakayosimamia na kuratibu utafiti wa kilimo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuwekeza katika utafiti kwa kuendeleza rasilimali watu na miundombinu ya utafiti. Idadi watafiti walioajiriwa ni takribani 360 na kati yao asilimia 16 wana kiwango cha elimu cha Shahada ya Uzamivu *(Ph.D).* Vilevile Serikali imeboresha maabara kuu nne za udongo katika Vyuo vya Utafiti vya Mlingano, Seliani, Uyole na Ukiriguru kwa kuzinunulia vifaa vya kisasa vya kutathmini virutubisho vya udongo/mradi wa kupima rutuba ya udongo na kuchora ramani yenye thamani ya takribani kuthamini ya takribani shilingi bilioni 1.8. Mradi huu utasaidia wakulima na wawekezaji katika sekta ya kilimo kufahamu viwango stahiki vya mbolea na mazao yanayostahili kulimwa katika eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hutenga takribani shilingi bilioni tatu kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Pia vituo hufanya shughuli za itafiti kwa kushirikiana na taasisi za kitaifa na kimataifa. Ni matarajio yetu kuwa mahusiano haya yataboreka zaidi baada ya *TARI* kuanzishwa rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, utafiti ni mojawapo ya vipaumbele katika Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili *(ASDP II).* Chini ya programu hiyo uzalishaji na usambazaji wa teknolojia za kilimo utaboreshwa zaidi kwa kuendeleza miundombinu ya utafiti na rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka mitano ijayo utafiti utalenga zaidi katika utatuzi wa changamoto zilizokabili mazao yenye tija na yenye kipaumbele kitaifa ili kutekelezwa azma ya kufikia uchumi wa viwanda. Shughuli za utafiti zitakazowekewa mkazo ni pamoja na ugunduzi wa mbegu bora, uzalishaji na upatikanaji wake, magonjwa na wadudu waharibifu, matumizi sahihi ya mbolea, udongo na maji, lishe bora, uhifadhi wa mazao na uongezaji wa thamani ya mazao ili kufikia kilimo chenye tija na cha kibiashara. Jumla ya shilingi 164,532,000,000 zinatarajiwa kuwekezwa katika shughuli za kilimo wa mazao, mifugo na uvuvi kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA ALI MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana, pamoja na majibu marefu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetangaza Tanzania ya viwanda na bila ya malighafi kutokana na mazao ya kilimo na uvuvi basi hatuna viwanda Tanzania.

Je, ni kwa nini Serikali haijajielekeza katika kilimo cha umwagiliaji maji ambapo Tanzania tuna mito mingi na mabonde mengi ili kuhakikisha basi tunakuwa na malighafi za kutosha kwa kipindi cha mwaka mzima? *(Makofi)*

La pili, kwa nini sasa Serikali haiwekezi katika mazao ya maua ambayo pia yanategemewa kuingiza *income* katika nchi yetu? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, majibu haya marefu sana!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema kuna uhitaji wa kuwekeza zaidi katika kilimo cha umwagiliaji na nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge katika Programu ya Kuendeleza Sekta Kilimo Awamu ya Pili *(ASDP II)* kilimo cha umwagiliaji ni moja kati ya masuala ambayo yamewekewa mkakati mkubwa. Kwa hiyo, tunaamini huko mbele tunakokwenda kilimo chetu kitabadilika kwa sababu tutawekeza zaidi kwenye umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili; sekta ya maua ni moja kati ya sekta za kilimo ambazo Serikali inatilia mkazo. Ukienda Kaskazini mwa Tanzania, Kilimanjaro na Arusha kuna mashamba makubwa sana ya maua, lakini kwa ujumla wake *horticulture* ni moja kati ya maeneo ambayo vilevile tumeyawekea mkakati. Kwa asilimia kubwa kilimo cha maua kinaiingizia Serikali fedha za kigeni. Lakini ni kweli

inawezekana kwamba bado kuna *potential* kubwa namna ya kuhamasisha kilimo cha maua.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nassari.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, msingi wa swali langu unajikita kwenye suala la utafiti. Mataifa yote yaliyoendelea duniani ni yale ambayo yamefanya tafiti na kuzitumia tafiti hizi iwe ni kwenye masuala ya kielimu, teknolojia, kilimo au *move* ya viwanda kama ambavyo tumekuwa tunasema kwa sasa kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwa namna gani basi Serikali inatuhakikishia kwamba tafiti za kilimo zitafanyika na ziweze kutafsiriwa na kufika chini kwa wananchi kwa maana ya kwenda kwenye uhalisia ili hali kwenye bajeti ya Serikali tu ambayo tunamaliza sasa hivi peke yake, kwenye fedha za maendeleo Wizara ya Kilimo haijapata zaidi ya asilimia 30. Sasa ni kwa namna gani tunawahakikishia Watanzania tafiti na tafsiri yake na kufika chini ili ziende kwenye uhalisia kwenye kilimo?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti ambazo zinafanyika katika vituo vyetu 16 vya utafiti, kawaida huteremka moja kwa moja kwenda kwa wakulima kupitia huduma za ugani. Ndio maana kwa miaka ya karibuni kumekuwepo na maendeleo makubwa sana katika kilimo chetu, Serikali itaendelea kuongeza bajeti ya ugani ili tafiti zile ziweze kuwafikia wakulima na hatimaye kilimo chao kiweze kuwa kizuri zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa kuwa sekta ya kilimo, uvuvi na ufugaji ni sekta ambayo inapata shida sana kwa wananchi wetu. Ni lini Serikali itaona sasa wakati umefika kuwapa elimu ili

wakanufaika na kilimo, mifugo na uvuvi wakaacha kuwa wanakamatwa mara kwa mara hasa wavuvi wanachomewa nyavu zao ni kwasababu hawapati elimu. Lini Serikali itajikita sana kuwasaidia hao wananchi maskini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu swali la Mheshimiwa Nassari, niseme tu kwamba Serikali hufikisha elimu kwa wakulima, wafugaji pamoja na wavuvi kupitia huduma za ugani na nieleze tu kwamba katika uvuvi kawaida tunatumia *beach management unit* kama njia sahihi ya kuwafikia wavuvi walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu mara nyingi hata wavuvi wanaofanya uvuvi haramu sio kwamba hawajui kwamba ni tatizo lakini wanafanya kwa kukusudia. Hata hivyo, Serikali itaendelea kutoa elimu na kusisitiza wananchi wetu wafanye uvuvi ambao unakubalika kisheria.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Mheshimiwa Selemani Zedi.

Na. 413

### Vijiji Vilivyo Ndani ya Kilomita 12 Kuunganishwa na Maji

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza:-

Kwa mujibu wa Sera ya Usambazaji wa Maji kutoka bomba kuu litakalotoa maji ya Ziwa Victoria kutoka Kahama hadi Tabora Mjini, ni kwamba vijiji vyote vilivyo ndani ya kilometa 12 toka bomba kuu vitaunganishwa na maji.

Je, ni vijiji vingapi vya Jimbo la Bukene ambavyo vimo ndani ya kilometa 12 vitaunganishwa maji kutoka bomba kuu hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa naiba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Jimbo la Bukene kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kupitia Kahama una lenga kuwapatia huduma ya maji wakazi wa Miji ya Tabora, Uyui, Nzega na Tinde pamoja na vijiji 89 vilivyopo ndani ya eneo la kilomita 12 kila upande wa bomba kuu la Mradi wa *KASHWASA.* Mradi huu ni wa malengo ya muda mrefu ya kuwapatia huduma ya maji ya uhakika wananchi wapatao milioni 1.1 wa maeneo hayo. Ujenzi wa mradi umegawanyika katika Awamu Mbili. Awamu ya Kwanza itahusisha kupeleka maji katika Miji ya Tabora, Igunga, Uyui, Nzega na Tinde. Kazi zitakazotekelezwa katika awamu hiyo ni pamoja na ujenzi wa bomba kuu kutoka Kijiji cha Solwa, ulazaji wa mabomba na ukarabati wa mitandano ya usambazaji maji katika miji hiyo. Awamu ya Pili mradi itahusu kupeleka maji katika Mji wa Sikonge kutoka Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jimbo la Bukene lililopo katika Halmashauri ya Nzega Vijijini, jumla ya vijiji vitatu vya Iboja, Ilagaja na Chamipulu vitapata huduma ya maji kupitia bomba kuu la kutoa maji Ziwa Victoria kutoka Kijiji cha Solwa kwenda Nzega. Kwa vijiji vingine ambavyo vipo umbali zaidi ya kilometa 12, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya maji katika vijiji hivyo kwa kutumia vyanzo vingine vya maji. Kazi hii itaendelea kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 1.8 kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Nzega kwa ajili ya kazi hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zedi.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza linahusu tafsiri ya kijiji kwenye huu usambazaji wa maji. Ninataka kujua anaposema maji yatafika Kijiji ya Ilagaja, Kijiji cha Ilagaja kina Vitongoji kumi. Je, maji yatafika makao makuu tu ya kijiji au katika vitongoji vyote kumi vinavyounda Kijiji cha Ilagaja?

Swali la pili, sasa maji haya yatakapofika Nzega na kwa sababu maeneo yetu ya Bukene yana shida ya *water table* kupata maji kutoka chini. Je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa kuanza mipango ya muda wa kati ili maji haya sasa yatakapofika Nzega yatoke Nzega yafikishwe Bukene ambako ni umbali wa kilometa 40?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza ameomba tafsiri kwamba maji yatafika Kijiji cha Ilagaja, je, vitongoji itakuwaje?

Naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kuwa lengo letu ni kuhakikisha kwamba maji safi na salama yanawafikia wananchi wote. Yatatoka Nzega ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya, yataenda Ilagaja yakifika pale basi tutaendelea kuyaendeleza kwenda mpaka kwenye vitongoji mpaka kwenye *point* ya mwisho ili wananchi wote eneo la Ilagaja na vitongoji vyake wapate maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na labda tu nizungumze kwamba ndio maana katika bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji tunatenga fedha kwa kila Halmashauri. Bomba la *KASHWASA* maji ya kutoka Ziwa Victoria yakishafika kwenye kitongoji kwa upande wa Halmashauri kile ndio chanzo cha maji, zile fedha tunazotenga basi muendeleze mpeleke kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, jibu lake ni hivyo hivyo kuwa yakishafika pale basi Halmashauri kile ndio chanzo, watenge fedha waunganishe kutoka pale kwenda kwenye maeneo ambayo hayana maji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kiula halafu Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza Wizara swali lifuatalo; kwa kuwa mradi wa vijiji kumi vya maji umefika mpaka Nduguti ambako ndio Makao Makuu ya Wilaya ya Mkalama na chanzo cha maji kimepatikana. Sasa ni lini Wizara itajenga miundombinu ili watu waweze kunywa maji na hiyo ni Wilaya kamili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wazir majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kwanza ya sekta ya maji ni kutafuta chanzo. Chanzo kikishapatikana kinachofuata sasa ni kuyasambaza maji kuyapeleka kwa wananchi na ndio maana kama nilivyosema kwamba tunatenga fedha. Kwa hiyo, baada ya chanzo kupatikana tayari tumetenga fedha katika bajeti ya mwaka 2017/2018 Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Halmashauri na kwa sababu fedha iko kwenye Halmashauri na wewe ni Diwani katika hiyo Halmashauri basi tushirikiane kuyatoa maji pale yalipopatikana tuwapelekee wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante, pamoja na Mkoa wa Rukwa kupata mvua nyingi kuwa na Ziwa Rukwa na Ziwa Tanganyika wananchi wake bado wanapata adha kubwa ya maji. Serikali haioni umuhimu wa kutumia Ziwa Rukwa na Ziwa Tanganyika kuwafikishia maji wananchi hao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ajiandae Mheshimiwa Salum na Mheshimiwa Saumu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa, Mji wa Sumbawanga mwaka huu wa fedha tumekamilisha mradi

mkubwa ambao unatoa lita milioni 13 kwa siku, kwahiyo wananchi wa Sumbawanga wanapata huduma ya maji safi na salama. Lakini pili, katika mwaka ujao wa fedha tayari Mkoa wa Rukwa wameleta andiko ambalo sasa tutaweka *consultant* aweze kufanya *feasibility study* na usanifu wa kina kwa malengo ya kuyatoa maji kutoka Ziwa Tanganyika kupitia vijiji vinavyokuja Sumbawanga mpaka Sumbawanga ili tuwe na chanzo cha uhakika cha maji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salum.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, ya kuuliza swali la nyongeza; kwa kuwa sera hii ya kupeleka maji ndani ya vijiji vyote ambavyo vinapitiwa na bomba hili la Ziwa Victoria ziwe ndani ya kilometa 12 imepelekea baadhi ya vijiji katika maeneo yanayopita hasa kwenye Jimbo la Solwa ambalo bomba hili kuu kutoka Solwa linakwenda kwenye maeneo mengi katika Mikoa ya Shinyanga na Tabora. Je, kwa nini sasa Wizara isione namna bora ya kuweza kupeleka maji haya zaidi ya kilometa 12 kwa sababu vijiji vingi vimeachwa kwa kuongeza tenki dogo kuongeza *gravity* ili wananchi wengi zaidi waweze kunufaika na maji haya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, ajiandae Mheshimiwa Saumu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mtandao wa bomba la *KASHWASA* umeacha matoleo katika maeneo mbalimbali na ndiyo maana matoleo yaliyopo Shinyanga sasa tunapeleka maji Tinde. Kwahiyo, kwenye mradi hizi kilometa 12 ni yale maeneo ambayo yatachukua maji moja kwa moja kutoka kwenye hili bomba kuu, mradi unaoendelea kupeleka kwenye vijiji vya kilometa 12. Lakini kupitia kwenye matoleo yaliyopo tunaweza tukaenda hata kilometa 50 na tumeanza kufanya hivyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge hiki ni chanzo cha maji tutaendelea kupeleka maji mpaka zaidi ya kilometa hata 100 kutoka kwenye hili bomba.

**MWENYEKITI:** Ahsante ameshakuelewa Mheshimiwa Saumu.

**MHE. SAUMU H. SAKALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Wilaya ya Pangani miundombinu ya maji imechakaa mno na hii ni kutokana na maji ya chumvi ambayo yamekuwa yakitoka. Swali langu ni kwamba, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ambayo imekuwa ikiahidi kila mara ya kutumia maji ya Mto Pangani ili kuweza kuwapatia wakazi wa Pangani maji ambayo hayana chumvi? Lakini pia kukarabati ile miundombinu ambayo imeharibika kwa kiasi kikubwa kutokana na maji haya ya chumvi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu miaka ya sabini Serikali tayari ilishaanza kutumia maji ya Mto Pangani na pale Korogwe tayari tunayatumia maji ya Mto Pangani. Tunao mradi mkubwa ambao umefadhiliwa na *BADEA,* sasa hivi Kampuni ya *Karathi* inatoa maji kupeleka maeneo ya Mwanga, yatafika mpaka Korogwe pia. Lakini pia tumepata ufadhili wa aina mbili; tuna fedha kutoka Serikali ya India lakini pia tuna fedha kutoka Serikali ya Netherlands, usanifu unaendelea ili tuhakikishe kwamba tunapeleka maji maeneo mbalimbali, tutafika mpaka Pangani Mheshimiwa Mbunge, wala usiwe na wasiwasi.

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, swali la Mheshimiwa Pascal Haonga.

Na. 414

**Kuanzisha Kilimo cha Umwagiliaji Mbozi**

**MHE. PASCAL Y. HAONGA** aliuliza:-

Wakulima wa Wilaya ya Mbozi wamekuwa wakitegemea mvua za msimu zisizotabirika katika kilimo chao.

Je, Serikali haioni kwamba huu ni wakati muafaka wa kuanzisha kilimo cha umwagiliaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pascal Yohana Haonga, Mbunge wa Jimbo la Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya hivi karibuni, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi imeanza kuathirika na vipindi vya ukame hata wakati wa msimu wa mvua, tofauti na ilivyokuwa miaka ya huko nyuma. Kutokana na hali hiyo, halmashauri ya Wilaya kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilikwishaanza kutekeleza mipango ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika wilaya hiyo kupitia mipango ya kuendeleza kilimo cha wilaya. Kupitia mipango hiyo, Skimu za Umwagiliaji za Sasenga (hekta 540), Iyula (hekta 180), Songwe (hekta 250), Bara (hekta 300), Mbulu Mlowo (hekta 100), Mkombozi (hekta 150), Ikumbilo Chitete (hekta 60), Ruanda Mbulu (hekta 52) na Wasa (hekta 45) ziliainishwa na kuanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, Wizara yangu kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kushirikiana na Halmashauri ya wilaya ina mpango wa kufanya upembuzi yakinifu katika maeneo yanayofaa kujengwa mabwawa kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua ili kuongeza upatikanaji wa uhakika wa maji ya umwagiliaji kwa ajili ya Skimu za Nambizo, Msia na Hamwelo katika Halmashauri hiyo.

Aidha, kwa kutambua athari za mabadiliko ya tabianchi, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Halmashauri zote zinazotekeleza kilimo cha umwagiliaji ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kutafuta fedha kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, lakini kabla sijauliza maswali mawili ya nyongeza ninaomba kufanya marekebisho kidogo. Jimbo sio la Mbozi Mashariki ni jimbo la Mbozi, kwa hiyo, naomba liingie vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Skimu za Umwagiliaji za Wilaya ya Mbozi zimechukua muda mrefu sana, kwa mfano Skimu ya Mbulu Mlowo imechukua zaidi ya miaka mitano haijakamilika na skimu hii ina urefu wa mita 1,125, zimejengwa mita 700 tu bado mita 400 kukamilika, miaka mitano mita 700, hizi zilizobaki 400 sijui zitakamilika lini. Sasa ninaomba Mheshimiwa Waziri aniambie ni lini hizi mita 400 zilizobaki zitakamilika katika Skimu hii ya Umwagiliaji ya Mbulu Mlowo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Wilaya ya Mbozi ni maarufu sana kwa uzalishaji wa zao la kahawa aina ya *Arabica,* ni kahawa ambayo ni tamu sana na ina soko sana duniani. Lakini kutokana na mabadiliko ya tabianchi mikahawa mingi inakauka Mbozi, hali imekuwa ni mbaya na muda si mrefu mikahawa hii inaenda kupotea Mbozi hatutakuwa na kahawa tena. Mheshimiwa Waziri, ninaomba sasa Serikali iweze kutoa *commitment* hapa; je, mko tayari kuweza kujenga mabwawa ya umwagiliaji wa kahawa maeneo yote yanayolima kahawa Mbozi ikiwepo Isansa, Igamba, Iyula, Msia na maeneo mengine ya Wilaya ya Mbozi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, anasema kwamba hizo skimu zimechukua muda mrefu; ni kweli, utaratibu uliokuwepo hapo mwanzo ulikuwa kwamba washirika wa maendeleo, *JICA* wamekuwa wanatekeleza wenyewe moja kwa moja, sasa tumeanzisha Tume ya Umwagiliaji ambayo ndiyo itasimamia miradi yote ya umwagiliaji na tulichopanga ni kwamba kwa kuanzia tutafanya mapitio ya miradi yote ya umwagiliaji tuikamilishe ile ambayo inaendelea.

Kwa hiyo, na huo mradi ambao tayari unaendelea tutaukamilisha kwanza kwa fedha ambazo tumezitenga kwenye bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali lako la pili kuhusu tabianchi; tabianchi haina jibu la moja kwa moja ila ni lazima sisi tuchukue hatua kwanza ya kukabiliana nalo. Kwanza, tuweze kuona namna gani tutatunza mazingira, hii ni kazi ambayo lazima hata Halmashauri ya Mbozi ishughulike, ukataji wa miti, uchomaji wa mikaa ni lazima uachwe kwa sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia suala la kujenga mabwawa, tulichokipanga ni kwamba kwanza tutafanya kila Wilaya imeainisha maeneo ya kujenga mabwawa, tunafanya usanifu kwanza tuweze kujua gharama na tuweze kuona mahitaji jinsi bwawa lile linaweza kuwasaidia wananchi kwa kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, suala lake tunalishughulikia na Serikali kupitia Tume ya Umwagiliaji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea, Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande.

Na. 415

**Kuanzisha Miradi ya Maji Kutoka Kwenye Mito ya Ruvuma na Rufiji**

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE** aliuliza:-

Serikali ilianzisha mradi wa kupeleka maji kwenye Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Dodoma toka Ziwa Victoria Mkoani Mwanza; mradi huu ulisaidia upatikanaji wa maji safi na salama pamoja na shughuli za kilimo.

Je, kwa nini Serikali isianzishe mradi kama huu kutoa maji kwenye Mito ya Ruvuma na Rufiji kwa ajili ya wakazi wa Lindi na mikoa jirani ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa maji na kusaidia shughuli za kilimo na ufugaji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji inatekeleza miradi miwili mikubwa ya kutoa maji kutoka Mto Ruvuma kwenda Manispaa ya Mtwara/ Mikindani na Miji ya Mangaka. Kwa upande wa Manispaa ya Mtwara/Mikindani, Wizara imekamilisha taratibu zote za manunuzi hadi kumpata mkandarasi wa ujenzi wa mradi wa kutoa maji kutoka Mto Ruvuma kupeleka Manispaa ya Mtwara/Mikindani pamoja na vijiji 26. Kwa sasa kinachosubiriwa ni kusaini mkataba wa kifedha baina ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya China kupitia Benki ya Exim.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mji wa Mangaka upembuzi yakinifu wa mradi wa kutoa maji kutoka Mto Ruvuma kupeleka katika mji huo pamoja na vijiji 26 umekamilika mwezi Oktoba, mwaka 2016. Kwa sasa kazi ya usanifu wa kina na uandaaji wa makabrasha ya zabuni inaendelea na inatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uanzishwaji wa mradi wa kutoa maji kutoka Mto Rufiji, Wizara itaendelea kutafuta fedha za kufanya utafiti ili kuwa na michoro na thathmini ya kiutaalam ili kutayarisha andiko litakalosaidia kutafutwa fedha za utekelezaji wa mradi huo kutoka vyanzo vya ndani na nje ya Serikali. Malengo ya miradi hii yote ni kutoa huduma ya maji safi na salama. Pia Serikali itaangalia uwezekano wa kuanzisha miradi kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika Mkoa wa Lindi na mikoa jirani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lathifah.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa Mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani ina mito mingine mikubwa kama Mto Mbwemkuru, Mto Matandu

na Mto Lukuledi lakini cha kushangaza maeneo yanayozungukwa na hiyo mito bado yanakabiliwa na tatizo kubwa la uhaba wa maji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia mito hiyo katika kujaribu kutatua tatizo hili la uhaba wa maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kwa kuwa hii mito mikubwa kama Mto Rufiji na Mto Ruvuma na mingineyo iliyopo katika Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma ni mikubwa ambayo ingeweza hata kusaidia katika upatikanaji wa umeme.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwezesha mito hii kuwekwa kwenye mpango wa *hydro-electric* kwa ajili ya kuleta umeme katika vijiji ambavyo *REA* imeshindwa kuvifikia? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza amehoji, ni kweli tunayo Mito ya Mbwemkuru, Matandu, Lukuledi katika eneo hilo, lakini sasa mito hiyo Mheshimiwa Mbunge na mimi nimekaa kidogo kule, uzoefu unaonesha kwamba inakuwa na maji mengi sana kipindi cha masika lakini baadhi ya mito kipindi cha kiangazi inakauka. Kwenye taratibu tunazoendelea nazo kufanya utafiti ili tuweze kujenga mabwawa makubwa ya kuvuna maji basi tutahakikisha kwamba mabwawa hayo tutayawekea na skimu za umwagiliaji ili wananchi wanaoishi pembezoni na hiyo mito waweze kufaidika na kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, umeuliza kuhusu umeme. Mheshimiwa Mbunge, zipo taratibu zinaendelea kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaweka kituo cha kuzalisha umeme katika Mto Rufiji kwenye hilo neno linaitwa *Stiegler's Gorge* ambapo kutakuwa na kilimo kikubwa pamoja na kuzalisha umeme mkubwa ili tuweze kuongeza nguvu ya umeme katika Tanzania.

Kwa hiyo, Serikali yako Mheshimiwa Mbunge ya Chama cha Mapinduzi tayari imeshaliona hilo na inaendelea kufanya mawasiliano na wafadhili mbalimbali pamoja na kutumia vyanzo vya ndani ili tuweze kutekeleza huo mradi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Sware, Mheshimiwa Vulu, Mheshimiwa Deo Sanga na Mbunge wa Tanga Mjini Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, kwa kuwa Naibu Waziri naye amekiri kwamba mito mingi ni ya misimu na kwamba wakati wa mvua tunapata mafuriko na wakati wa kiangazi ni ukame. Sasa Wizara inaonaje ikajikita katika shughuli za kukinga maji ya mvua kuyahifadhi ili yaweze kutumika kwa ajili ya shughuli za kilimo, mifugo na shughuli nyingine za kimaendeleo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, wako wengi hao. Tena ukijibu subiri hapo hapo usipate taabu ya kwenda na kurudi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea na jitihada za kuhakikisha tunakinga maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya binadamu majumbani lakini pia na umwagiliaji kwa kujenga mabwawa na tumeshaelekeza kila halmashauri kila mwaka ihakikishe inatenga fedha na kufanya utafiti bwawa moja ili ikiwezekana kila halmashauri ijenge bwawa moja kila mwaka. Na pia tumeelekeza halmashauri wanapopitisha ramani za nyumba basi wahakikishe kwamba wanaweka na utaratibu wa kuvuna maji kutoka katika mapaa ya nyumba kama inavyofanyika maeneo mengine.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Vulu.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa swali la msingi limetaja Mto Rufiji ambao upo kwenye Mkoa wa Pwani ninaotoka, na kwa kuwa watu wa Mkoa wa Pwani

wamezungukwa na mito mingi, na kaulimbiu ya Serikali ni kumtua ndoo mwanamke. Je, Serikali ina mpango gani kwa kuanzia na Mto Rufiji kuweza kusambaza mabomba ya maji kwa wananchi na kuwaondoa na adha ya kuliwa na mamba mara kwa mara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, na ndiyo maana nimekuambia ukae hapo hapo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ni kwamba tayari tunatenga fedha kila Halmashauri na zimeshaanza kutekeleza miradi ya maji, upo ushahidi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wananchi wengi wanaliwa na mamba kwa Mto Rufiji, wale wanaokaa pembezoni na Mto Rufiji, lakini kama nilivyojibu katika swali langu la msingi kwamba tunatafuta fedha ili tuweze kufanya utafiti tutengeneze mradi mkubwa wa maji tuyatoe maji kutoka Mto Rufiji tuwapelekee wananchi pembezoni mwa huo Mto Rufiji ili wasiwe na haja tena ya kushuka kwenda kule mtoni kuchukua maji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo, ajiandae Mbunge wa Tanga Mjini Mheshimiwa Mbarouk, halafu Mheshimiwa Awesu na Mheshimiwa Sokombi.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makambako ni mji unaokua kwa kasi na Serikali ilishatenga fedha kutoka Serikali ya India ili kutatua tatizo la maji Makambako ambalo kuanzia mwezi huu wa nane, wa tisa, wa kumi na kuendelea mpaka Desemba hali huwa inakuwa ni ngumu sana.

Je, Serikali ina mpango gani sasa kuwathibitishia wananchi wa Makambako juu ya fedha za India kwamba sasa watapata maji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu Waziri kwa kifupi, ajiandae Mheshimiwa Awesu, Mheshimiwa Mbarouk, Mheshimiwa Sokombi na Mheshimiwa Ndassa.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepata dola milioni 500 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji katika miji 16 Bara na mmoja Zanzibar ikiwemo pia na Mji wa Makambako. Sasa kinachoendelea kwa sasa hivi, Mheshimiwa Mbunge, tunasubiri *financial agreement* isainiwe kati ya Hazina na Serikali ya India, lakini Wizara ya Maji na Umwagiliaji tunajiandaa na kuwapata wahandisi washauri kwa ajili ya kukamilisha usanifu haraka na kutangaza *tender.* Kwa hiyo, nikuhakikishie wananchi wa Makambako baada ya muda watapata maji ya uhakika kutoka kwenye huo mradi mkubwa utakaotekelezwa na fedha za Serikali ya India.

**MWENYEKITI:** Ameshakuelewa Mheshimiwa Aweso. Waheshimiwa Wabunge, mkipewa maswali haya kwa hisani ya kiti msilete ufundi mwingi, ulizeni swali moja kwa moja tu.

**MHE. JUMAA H. AWESO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tatizo la maji Pangani ni kubwa na kwa kuwa katika Wilaya yetu ya Pangani tumejaliwa kupitiwa na Mto Pangani katikati ya Mji wa Pangani. Je, Serikali haioni haja sasa ya kuutumia Mto Pangani ili kuondoa tatizo la maji katika Mji wa Pangani?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nikupongeze Mheshimiwa unawahudumia sana wananchi wako kwa sababu juzi umekuja ofisini, tumezungumza na tukaelekeza hatua za haraka uwasiliane na watu wa *DDCA* na Mhandisi aliniahidi kwamba katika muda wa wiki mbili atanipa majibu ili tufanye kwanza hatua za dharura. Lakini pia tunaendelea kutumia Mto Pangani ili tuhakikishe kwamba tunawapatia maji watu wa Pangani bila wasiwasi wowote Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mbarouk, ajiandae Mheshimiwa Sokombi na ajiandae Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. BAKARI M. MUSSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Halmashauri ya Jiji la Tanga ni moja ya Halmashauri zilizobahatika kupata mradi wa vijiji 10 kila Halmashauri. Upande wa Kusini mradi wa maji umekamilika lakini upande wa Kaskazini hadi leo mradi haujakamilika kwa kuwa mzabuni anadai.

Je, ni lini Serikali itamlipa mzabuni ili akamilishe mradi wa maji na Wananchi waweze kupata maji safi na salama kwa vijiji vya Kiruku, Kibafuta, Bwagamoyo na Chongoleani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweka utaratibu Serikali inatoa fedha baada ya kuleta *certificate* na wewe kama Mbunge naomba usaidiane kusimamia huo mradi ili mkandarasi azalishe. Akileta *certificate* Mheshimiwa Mbunge dakika yoyote fedha tunayo na fedha kutoka Mfuko wa Maji na kwa bahati nzuri *flow* yake ni nzuri, akileta *certificate* tunalipa ili akamilishe huo mradi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sokombi atafuatiwa na Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nashukuru pia kupata swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mara umezungukwa na Ziwa Victoria lakini cha ajabu Ziwa hilo hilo lime-*supply* maji kutoka Ziwa Victoria kuja Shinyanga, Tabora na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mara hasa Musoma Vijijini na Wilaya ya Bunda haina maji. Je, Mheshimiwa Waziri ni lini Wilaya hizo zitapata maji? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ni lini. Waziri wa Maji amesimama Mheshimiwa Naibu Waziri pumzika.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mara ukianzia na Mji wa Mara tumechukua maji kutoka Ziwa Victoria pamoja na vijiji vyote vinavyozunguka ule Mji wa Musoma kwahiyo siyo kwamba hakuna mahali tumechukua maji kutoka kwenye Ziwa Victoria. Pia katika maeneo mengine, unajua hatuwezi kusema tutapeleka maji ya Ziwa kupeleka kila Kijiji katika mradi huu wa WSDP tulikubaliana kwamba ili tuweze kufika maeneo mengi lazima tutafute teknolojia ambayo ni rahisi ili kila Kijiji kiweze kupata maji kwa haraka na ndiyo maana tulianza na *concept* ya visima. Sasa baada ya kuona kwamba visima maeneo mengine havijakuwa endelevu ndiyo tumeanza kurudi sasa kubuni miradi mikubwa zaidi ambayo teknolojia Wananchi hawawezi kuendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua maji kwenye bahari au kwenye ziwa utahitaji umeme mkubwa, mitambo mikubwa na wananchi hawawezi kuendesha na ndiyo maana sasa tunafikiria kwamba katika awamu inayokuja hii awamu ya tano ili tuwe na uhakika kwamba miradi yetu inakua endelevu tunataka tusimamie chini ya Wakala wa Maji Vijijini, hawa watakuwa na mfumo unaokuwa ni sahihi kwa nchi nzima kuliko sasa kila Halmashauri, unakuta Halmashauri nyingine umewapelekea fedha mpaka inafika mwezi Juni hawajafanya kitu chochote, fedha wanazo lakini hawafanyi chochote sasa nataka tuingize kwenye Wakala wa Maji ambao watasimamia ujengaji wa hii miradi, halafu hawa TAMISEMI, hizi Halmashauri zitakuwa zinaendesha pale ambapo wanaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua kwa mfano Nansio, tumejenga mradi mkubwa wa maji, Halmashauri haiwezi kuendesha kwahiyo imebidi Wizara tuendelee kuendesha kwahiyo maeneo mengine tutafanya hivyo. Ukichukua mradi mkubwa kutoka kwenye mto ni lazima pia uendeshaji wake uwe sasa chini ya Wizara maana yake

Halmashauri haziwezi kuendesha kwahiyo hili jambo tutalifanyia kazi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ameshakuelewa usitumie nguvu nyingi, Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Bwana Waziri naomba nikuulize swali. Serikali ina mpango gani mahususi kwa ajili ya kutumia mabonde yetu kama Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria pamja na Mito mikubwa, Serikali ina mpango gani mahususi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tuna mabonde tisa katika Nchi yetu na mpango mahususi tayari tunaanzisha *commission* kwa kila bonde kwasababu mabonde mengine ni kwamba matumizi ya maji yako *shared* na nchi zingine kwahiyo kupitia kwenye hizo *commission* ndiyo tunaratibu maji tuyatumiaje, tutatumia kwa maji safi na salama kama tunavyoyatoa *Lake Victoria* kupeleka Igunga lakini pia tutatumia kwa ajili ya vilimo vya umwagiliaji. Kwa hiyo, tunao mpango mahususi kuhakikisha kwamba mabonde yote tuliyonayo ambayo yako nchini kwetu tunayatumia vizuri kwa ajili ya umwagiliaji na pia kwa ajili ya maji safi na salama na maana ya mabonde ni nini? Ni pamoja na maziwa na mito.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha.

Waheshimiwa Wabunge, liko tatizo la Serikali mara nyingi inapeleka pesa za maji kwenye Wilaya zetu, lakini maji haya hayatoki kwa sababu Wakandarasi wengi hawana uwezo wa kufanya hizi kazi na pesa nyingi zinatumika, zinaliwa na maji hayatoki na hii inaathiri wananchi kupata maji lakini inaathiri na ninyi vilevile. Kwa hiyo naomba sasa Wabunge msimamie pesa zinazokwenda kwenye Majimbo yenu na kwenye Wilaya zenu ili maji yatoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, maeneo mengi kuna matatizo kuwa maji watu wanachimba, wanashindwa kupata maji sababu teknolojia waliyokuwa nayo na vifaa walivyonavyo ni duni sana. Hebu nendeni kwenye nchi mbili hizi, Morocco na Israel wanauwezo wa kuchimba maji mpaka mita 600 kwenda chini. Kero hii itakwisha *once and for all* na kila mtu atakuwa na furaha na maji yatapatikana kila mahali. *(Makofi)*

Waheshimiwa sasa nitangaze wageni, wageni 60 wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo wanaotoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao watashiriki shughuli za uzinduzi wa Kamusi kuu ya Kiswahili wakiongozwa na Profesa Elisante Ole-Gabriel, Katibu Mkuu, Ndugu Nuru Millao, Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Selemani Sewagi, Mtendaji Mkuu wa Baraza la Kiswahili-Tanzania (BAKITA), karibuni. *(Makofi)*

Pia wameambata na viongozi wa Kampuni ya LongHorn-Tanzania iliyochapisha Kamusi hiyo wakiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni hiyo Ndugu Khatib Senkoro, Mwenyekiti wa Bodi ya LongHorn, Ndugu Simon Ngigi, Mkurugenzi Mtendaji Kampuni ya LongHorn.

Ujumbe wa Bunge kutoka Bunge la Msumbiji ambao ni Wajumbe wa Kamati za Serikali za Mitaa wamekuja kwa ajili ya ziara ya mafunzoni, kubadilishana mawazo na Kamati za Kudumu za Bunge, Utawala na Serikali za Mitaa; *Comrade* Luca Chomera Jeremia, Mwenyekiti wa Kamati na Kiongozi wa msafara, Beatriz Mario Chaguala, Mjumbe, *Comrade* Martinha Januario Benfica, Mjumbe, *Comrade* Elisa Maria Silvestre Cipriano, Mjumbe, *Comrade* Jose Tsingano Camanula, Mjumbe. *Comesta chef comarade*. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 55 wa Mheshimiwa Juma Aweso, Mbunge ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kilichopo Mkoani Dodoma, karibuni. Pia kuna wageni 37 wa Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge ambao ni Wahadhiri na Wanachuo kutoka chuo cha Iringa kilichopo Mkoani Iringa, karibuni. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 100 na Walimu watano kutoka Shule ya msingi ya Maria Margreth kutoka Mkoa wa Moshi. Wageni 25 kutoka *Public Relation Society of Tanzania (PSRT)* wa kutoka Jijini Mwanza.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwatangazia Wabunge wote kuwa leo Jumatatu tarehe 19 Juni, 2017 kutakuwa na uzinduzi wa Kamusi kuu kuanzia saa 7.00 mchana katika ukumbi wa Bunge. Kufuatia shughuli hiyo muhimu, Wabunge wote mnaombwa kubaki ndani ya ukumbi wa Bunge mara baada ya kusitisha Bunge ili kuweza kushiriki katika tukio hilo ambalo litachukua muda mfupi sana. Kwa maana hiyo tukishasitisha shughuli za Bunge mchana tunaomba Waheshimiwa Wabunge msiondoke.

Mheshimiwa Spika anawaalika katika futari kesho Jumanne tarehe 20 Juni, 2017 mara baada ya upigaji kura wa Bunge kuahirishwa. Futari hiyo itakuwa katika viwanja vya Bunge eneo la wazi, mkabala na jengo la Idara ya Habari. Mwaliko huu utajumuisha Waheshimiwa Wabunge, Wazee wa Dodoma, Watumishi wa Bunge pamoja na wageni ambao watakuja kwa ajili ya shughuli za Bunge. Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kushiriki bila kukosa. Katibu!

## MWONGOZO

**MWENYEKITI:** Mwongozo. Nitachukua miongozo miwili, moja huku moja huku. Mheshimiwa Shangazi na Mheshimiwa Heche.

**MBUNGE FULANI:** Wote wanaume.

**MBUNGE FULANI:** *Gender.*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa mnazungumza bila utaratibu nitatoka huku vilevile. *(Kicheko)*

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naomba Mwongozo wako, wakati Serikali inajibu swali langu namba 411 majibu yake yalikuwa siyo ya kuridhisha. Sasa nilikuwa naomba Mwongozo wako kwamba Serikali ilete majibu siku nyingine, sikuridhika kabisa na majibu ya Mheshimiwa Waziri yalikuwa ni majibu mepesi sana na swali hili ni swali zito sana, majibu ni mepesi hayana uzito kabisa. Naomba Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 47 na vifungu vyake vyote. Kama mlivyosoma kwenye vyombo vya habari, jana wananchi wa Tarime hasa eneo la Nyamongo na leo asubuhi wamemuunga mkono Rais kwa vitendo kwa kuingia kwenye mgodi wa *North Mara* kuzuia wezi ambao Kamati zote za Rais zimethibitisha na Rais amewatangazia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jambo la ajabu ni kwamba polisi wanatumia nguvu kubwa sana kupiga Wananchi, kuwaumiza kinyume cha utaratibu wa Rais alivyoagiza, naomba mwongozo wako. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Naomba mkae, Bunge haliendeshwi na *issue* za *gender*, Mheshimiwa Kanyasu naomba ukae. Waheshimiwa huu muda huu tunauchukua kwenye kuchangia, wanapopungua watu kuchangia mnalalamika baadaye vilevile kwa hiyo miongozo miwili.

Mheshimiwa Shangazi ni kweli kwa mujibu wa Kanuni ya 45(3) ambayo ulibidi uitumie na ilibidi Spika aridhike lakini umeanza kuridhika wewe kabla sijaridhika mimi. Lakini nakubaliana na wewe naagiza swali hili lije lijibiwe tena kwenye Bunge lijalo.

Mheshimiwa Heche *issue* yako hiyo nakuomba uonane na Waziri wa Mambo ya Ndani i-*engage* Serikali na mtazame

njia muafaka ya kulitatua. Waheshimiwa tunaendelea. *(Makofi)*

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina hebu kaa.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa Kwa Mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea tunaanza na mchangiaji wetu wa kwanza Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, ajiandae Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani na ajiandae Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwa niaba ya Wananchi wangu wa Jimbo la Rufiji basi naomba nitoe mchangi wangu kuhusiana na bajeti hii iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako hili tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii nimpongeze sana Wazari wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa kuja na bajeti nzuri ambayo imezingatia maoni ya wananchi, maoni ya Wabunge na maoni ya wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwasababu ukiiangalia bajeti hii na ukipitia takwimu zilizowahi kutolewa na *Central Intelligence Agency (CIA)* katika dondoo zao za *World Fact Book* ambazo waliwahi kuzitoa ambazo

zimeelezea mipango mbalimbali ya bajeti ambazo zinatolewa na...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa mnavyotoka naomba mtoke kwa utaratibu, zogo limekuwa kubwa sana humu ndani.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** ...ambazo zinatolewa na *CIA* katika takwimu zao zinazotolewa mara kwa mara ambazo zinachunguza nchi mablimbali zaidi ya 267. Katika takwimu zilizotolewa na *World Fact Book* zinaifanya bajeti yetu ya Tanzania kuwa ni miongoni mwa bajeti bora kabisa hapa Afrika na dunia na ukiangalia takwimu hizi zimegawanya bajeti katika maeneo matatu; yaani nchi zinazojitegemea, nchi tegemezi na nchi zingine zikijumuisha nchi za Ulaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo, bajeti yetu ni dhahiri kabisa ni *stimula to economic sector* na imedhamiria ku-*alleviate poverty* katika nchi yetu hii ya Tanzania. Niipongeze Serikali sana kwa namna ya kipekee kabisa ambavyo imedhamiria sasa kutukwamua Wananchi wa Jimbo la Rufiji. Tukiangalia miradi mbalimbali ya Benki ya Dunia imefika Rufiji leo hii kutokana na maombi ya Mbunge wa Jimbo la Rufiji na tumeweza kupata miradi kadhaa ya kutoka Benki ya Dunia ambapo sasa wananachi wangu wa Kata ya Mbwala wataweza kupata maji ya kutosha katika maeneo ya Nambunju, Tawi, Kikobo lakini pia katika maeneo mbalimbali maeneo ya Miangalaya, Namakono, Tawi, Siasa kule Utete na pia Serikali imedhamiria kuchimba visima viwili katika Kata ya Chumbi na haya yote yalikuwa ni maoni yangu na maombi yangu kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali imekubali kutuchimbia kisima katika shule ya sekondari ya Mkongo pamoja na kusambaza mabomba katika kata hii ya Mkongo lakini pia katika kata ya Ngarambe, Njawanje, Kingulwe na Namakono, Kipugila pamoja na maeneo ya Nyaminywili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema niipongeze Serikali kwasababu maeneo yetu mengi wakati Serikali inafikiria kumkwamua Mwanamke au Mwanamama kumtua ndoo kichwani sisi kule wananchi tulidhamiria kuondoa vipara kichwani kwa akina mama kwa sababu wananchi wetu wamekuwa wakibeba maji katika umbali mrefu zaidi ya kilometa saba na yako maeneo na baadhi ya vijiji ambavyo wananchi wamediriki kuhama vijiji vyao kwasbabu tu ya kutokupatikana kwa maji. Kwa hiyo, kwa namna ya kipekee kabisa naipongeza sana Serikali kwa kudhamiria sasa kutatua kero ya maji kwa wananchi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija upande wa pili kuhusiana na suala zima la kilimo kama ambavyo Mwalimu Nyerere aliwahi kusisitiza katika kitabu chake cha Ujamaa kwamba *"The hidden story of the sociallist village"* kilichowahi kutolewa mwaka 2008 na kikarekebishwa tena mwaka 2014 na Bwana Ibott aliwahi kusisitiza kuhusiana na vijiji vya ujamaa katika kuboresha na kuhakikisha kwamba tunakuwa na uchumi wa kujitegemea sisi wenyewe Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi Wananchi wa Jimbo la Rufiji tunayo ardhi iliyo nzuri yenye rutuba na tunaamini kabisa ardhi ya Rufiji inaweza kulisha Nchi yetu hii ya Tanzania lakini pia inaweza kulisha mpaka Afrika Mashariki, lakini tatizo kubwa tulilonalo ni watu wachache ambao wamejimilikisha ardhi yetu ya Rufiji na imesababisha kwamba wawekezaji wengi wanakosa ardhi wanapokwenda *TIC* kuomba kufanya uwekezaji katika maeneo yetu ya Rufiji, tunaonekana Rufiji hatuna ardhi kwa sababu tu kuna watu wachache ambao wamejimilikisha ardhi, ardhi ambayo hawaitumii kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo kwa kupitia Sheria ya ardhi sura ya 113 na Sheria ya ardhi sura ya 144, nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Ardhi lakini pia Mheshimiwa Rais kunyang'anya Wawekezaj wote Matapeli walioingia Rufiji ambao wamejimilikisha ardhi na hawaitumii ardhi kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti iliyopita Waziri wa Kilimo alisimama katika Bunge hili na kuwaambia Warufiji kwamba watapata Kiwanda cha Sukari. Leo hii wananchi wa Rufiji wananihoji, wanauliza hiki kiwanda kimekwenda wapi? Lakini tunajua kwamba yupo Muwekezaji aliyechukua ardhi katika Kata ya Chumbi, Muhoro na maeneo mengine ya Tawi katika Kata yetu ya Mbwala akidhamiria kujenga Kiwanda cha Sukari lakini sisi tunajua kwamba mwekezaji huyu ni tapeli na hana uwezo wa kujenga kiwanda hiki na tunaiomba Serikali kupitia Waziri wetu wa Kilimo, Waziri wetu wa Viwanda asimame hapa atuambie na tunamuomba Mheshimiwa Rais afute hati hizi zote na ikiwezekana hati hizi wakabidhiwe mashirika ya umma kwa mfano *PSPF* pamoja na Mashirika mengine *NSSF* na *LAPF* ili waje Rufiji kutujengea cha sukari*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ya Rufiji ni ardhi yenye rutuba sana, tunaamini tukipata Kiwanda cha Sukari wananchi wangu wataweza kulima miwa. Nikuombe Waziri wa Kilimo au Waziri wa Viwanda au Mheshimiwa Waziri wa Fedha usimame hapa utuambie. Lakini pia Waziri wa Ardhi usimame utuambie wale wawekezaji matapeli waliokuja Rufiji na kuchukua ardhi ni lini watanyang'anywa ardhi hiyo na ardhi hiyo irejeshwe Serikalini ili sasa wawekezaji wanapokwenda *TIC* waweze kupata ardhi ya kuja kuwekeza katika maeneo yetu ya Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayasema haya kwa sababu wananchi wengi wa Rufiji hawana shughuli za kufanya yaani *economic activity* kwa wananchi wa Rufiji ni ndogo sana. Na ndio maana leo hii baadhi ya wananchi wanajiingiza kaitka mambo yasiyofaa. Kwa hiyo, ili kulikwamua tatizo hili niombe Serikali sasa kuhakikisha kwamba inawasaidia Warufiji ili sasa wananchi wangu waweze kupata shughuli mbalimbali za kufanya katika uwekezaji ambao utafanywa na wawekezaji watakaoletwa na Serikali kupitia *TIC* pamoja na Wizara nyingine mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona niseme hili kwa sababu ninaamini kabisa kilimo ndio kitaweza kumkomboa Mtanzania na kama tunavyofahamu kwamba asilimia 70 ya Watanzania ni wakulima, tunaiomba Serikali kuwa *serious* kabisa kwenye jambo hili la kilimo. Ninaamini kabisa kwamba iwapo tunahitaji kujitegemea ni lazima tuzingatie Kilimo hiki ambacho nimekizungumzia hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine tulilonalo kwa wananchi wa Rufiji ambao ninaomba niishauri Serikali kama ambavyo imezungumzwa katika ukurasa wa tisa wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni tatizo la barabara. Tuna kila sababu ya Rufiji kuomba Serikali sasa itujengee barabara ambazo zitasaidia kuongeza shughuli za uchumi, na barabara hizi ambazo nazizungumzia hapa zimezungumzwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukisoma ukurasa wa 46 wa Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ambayo inazungumzia uboreshaji wa Miundombinu. Niombe Serikali sasa, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kukubali kutujengea barabara yetu ya Nyamwage kwenda Utete, niiombe Serikali sasa ujenzi wa barabara hii uharakishwe na uanze sasa. Kwani wananchi wana kiu kubwa ya kusubiri ujenzi wa barabara hii yenye kilometa 33.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia barabara ningine ya kutoka Ikwiriri kwenda Mwaseni kule Mloka, itasaidia kufungua shughuli za uchumi. Na ninaamini kabisa wa Rufiji watashiriki kwa hali na mali katika kushiriki katika shughuli za uchumi. Na barabara nyingine ni yakutoka Kibiti kuelekea Mkongo, barabara hii pia ni muhimu sana kwa shughuli za uchumi wa Rufiji. Na barabara ya kutoka Bungu kuelekea Nyamisati ni barabara muhimu sana iwapo barabara hii itajengwa itaweza kuwakomboa Warufiji na Warufiji wengi watashiriki katika shughuli za uchumi na itawaondoa katika fikira za kushiriki katika mambo yasiyofaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie dakika mbili tatu kushauri katika suala zima la madini. Nchi yetu

imefika hapa kwa sababu ya kuwepo kwa mikataba mibovu kama ambavyo Wabunge wengi wamelizungumza jambo hili. Na mimi nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kupambana na ukoloni mamboleo, mimi nauita ukoloni mamboleo kwa sababu hili limezungumzwa na watu wengi Duniani akiwepo Profesa Lumumba. Pia tumeona mfano wa yeye aliyofanya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli, wameanza kuiga Marais wengi na viongozi wengi wa Dunia wameanza kuiga. Kwa mfano Rais wa Latin America hivi juzi amezuia kilo 1300 ya dhahabu, ni kwa sababu tu mikataba mingi ya dhahabu, mikataba mingi ya madini imekuwa ni mikataba mibovu ambayo inawakandamiza wananchi ambao wanamiliki madini yale. Na tunasema mikataba hii ni *detrimental to public interest,* mikataba hii ni mibovu na mikataba ambayo haifai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwanza naomba niishauri sana Serikali yangu, kabla hatujafikia hatua ya kurekebisha mikataba hii, basi tuanze kwa kurekebisha Sera ya Madini, sera hii ya mwaka 1997. Sera hii ya madini inayoiondoa Serikali katika umiliki wa madini yetu hapa nchini na kuyafanya madini kuwa chini ya wawekezaji. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, ajiande Nkamia.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi...

**MWENYEKITI:** Subiri kidogo dakika moja, subiri kidogo. Waheshimiwa Wabunge kuna tangazo, Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi, leo saa 8.00 mchana wanatakiwa wakutane kwenye Ukumbi wa *White House* na wote wahudhurie bila kukosa. Leo saa nane mchana.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, mwingi wa Utukufu ambaye ameniwezesha kusimama hapa siku hii ya leo nikiwa na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nianze na barabara ya kilometa 130 ambayo inatoka Kitai kwenda Mbambabay. Barabara hii ni ndefu, lakini kulingana na changamoto ambayo iko katika barabara hiyo ya kipande cha kilometa 40 inayotaka Kitai kwenda mpaka pale Rwanda kwenye uchimbaji wa makaa ya mawe, mimi naomba Serikali ichukue kipande hiki cha kilometa 40 kwa maana ya changamoto yake, ili iweze kurahisisha uchimbaji wa makaa ya mawe na usafirishaji wake. Kilometa 40 hizi zitasaidia sana kurahisisha utekelezaji huu wa uchimbaji wa makaa ya mawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niende kwenye suala la maji, wanawake wenzangu wa Mkoa wa Ruvuma wanapata shida sana kwenye eneo hili la maji. Maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Ruvuma bado yana shida kubwa ya maji. Inawezekana kabisa asilimia chache sana za upatikanaji wa maji, naomba suala hili Serikali ilichukue na kuhakikisha kwamba maeneo yote ya Mkoa wa Ruvuma wanawake wenzangu wanapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika niseme kuna Benki ya Kilimo. Benki ya Kilimo hata mwaka jana nilisimama hapa. Benki ya Kilimo imekwenda kuwekwa kwenye maeneo ambayo mengine hayana walengwa sahihi wa masuala ya kilimo.

Ninaomba benki hii ya kilimo, nilisimama mwaka jana Mheshimiwa Mpango, nikakamata na shilingi yako ukaniahidi kwamba mimi hii ni bajeti yangu ya kwanza, naomba uniachie ili mimi nitahakikisha kwamba mwaka huu wa fedha Benki ya Kilimo inakwenda Ruvuma. Mpaka leo ng'oo hakuna Benki ya Kilimo, sasa sijui nikueleweje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utakapokuwa unakuja ku *wind up* hapa unieleze benki hii inaanza lini? Kama shida ni majengo basi mimi nitawapa jengo langu ili wakae pale wafanye kazi hiyo. Tafadhali naomba ili wanawake waweze kukopa mikopo na wananchi wengine wote waweze kukopa mikopo waweze kufanya kilimo chenye tija ambacho kitawasababisha wapate mitaji mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye kodi ya nyumba. Kodi ya nyumba ni nzuri, hata mimi mwaka jana nilisimama hapa nikapongeza Serikali kuchukua uamuzi wa kuipa *TRA* iweze kukusanya pesa hiyo kwa maana ya kodi ya majengo. Lakini sasa naona kwamba yaani napata picha namna gani ambavyo utakwenda kwa mwananchi ukasimama pale akamwambia akupe shilingi 10,000 ya pamoja ni maumivu, na inawezekana kabisa utekelezaji wake utakuwka na rabsha mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mawazo yangu ni kwamba, kwenye ile tozo ya shilingi 40 tuliyoiweka tungeongeza tozo ya shilingi 50 ili iingie huko na watu waweze kulipa kodi hii bila maumivu ya moja kwa moja wanayoyaona. Na ninaamini kabisa hili litatekelezeka bila kelele zozote. Lakini pia tutenganishe nyumba, nyumba ziko za biashara na nyumba za makazi. Kwa hiyo, wale wa biashara basi wachukuliwe kibishara na hizi za makazi iongezeke tozo ya shilingi 50 ili waweze kulipa kwa mtindo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwenye afya. Niombe sana, kuna maeneo ambayo wakati wa Wizara ya TAMISEMI nilichangia hapa. Nikaainisha maeneo ya Namtumbo kule, kwenye Kituo cha Afya cha Rusewa, tunahitaji gari la afya, *ambulance* kwa ajili ya kurahisiha wanawake ambao wanakwenda kujifungua kutoka pale Rusewa kwenda kule katika Wilaya ya Tunduru. Kuna eneo ambalo lazima watembee kwa kilometa 150 ambalo wanakwenda kubebwa kwenye matenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais uliko huko naomba unisikie na mimi naomba *ambulance* moja ili iende kule Namtumbo ikasaidie wanawake wa Namtumbo katika Mkoa wa Ruvuma. Nakuomba sana baba yangu, pamoja na jitihada zote na kazi zote unazoendelea kuzifanya basi na hilo naomba wanawake wa Ruvuma kule, walikutwangia kura nyingi sana za kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nizungumzie wazabuni wa ndani. Wazabuni wa ndani kama wa mawakala wa pembejeo wamekuwa wakinyanyasika mpaka sasa hivi hawajalipwa pesa zao, naomba Serikali ione umuhimu. Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli wewe ni Rais wa wanyonge, unagusa kabisa matatizo ya wanyonge. Waone hawa wazabuni ambao wamekuwa wakihangaika mpaka sasa hivi hawajui hatma yao, wasaidie ili waweze kupata haki yao. Wale ambao hawajafanya vizuri wawekwe pembeni, waliofanya vizuri kwa uaminifu walipwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika wazabuni wa ndani, kwa mfano wako waliohudumia mashule, vyuo, lakini pia wapo waliohudumia kwenye vikosi vya jeshi, nao pia waweze kulipwa hizo pesa ili waweze kuendeleza mitaji yao. Tunahitaji uchumi wa viwanda wakati watu wetu wa ndani tunawaumiza na kuwaangamiza na kuua mitaji yao, tuwalipe waendeleze shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo anatekeleza majukumu yake na kubainisha matatizo moja baada ya lingine na kuyaondoa kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza hapa masuala ya makinikia. Makinikia yamezungumzwa na Wabunge wengi, lakini juzi mmemsikia Mbunge alizungumza hapa, Mbunge huyu anaitwa Mheshimiwa Heche, alizungumza akawa anahamasisha wananchi wake waende kuvamia migodi, kwa hiyo kazi aliyoifanya na leo anajikosha kwa kuomba mwongozo hapa. Mimi niseme tu hicho ndicho

alichokitaka na amesha-*organize* wameenda kuvamia migodi, Rais hajasema kwamba watu wakavamie migodi, kwa hiyo, huo ni uvunjaji wa sheria, hao watu washughulikiwe kama wahalifu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo mwongozo wako umeelekeza kwamba aende kwa Waziri wa Mambo ya Ndani, mimi naomba aunganishwe na yeye kama mhalifu namba moja, kwa sababu yeye ndio aliyekuwa anahamasisha hapa ndani tumemsikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie pia suala la Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Tundu Lissu anapinga ripoti hii iliyotolewa ya vyombo vya utafiti uliofanyika. Mimi nataka niseme hivi, hawa wajumbe walioingizwa kwenye ile Kamati sio kwamba wanajipangia wao wenyewe, vipo vyombo mahsusi vinavyochuja na kubainisha sifa za watu ili waweze kuingizwa kwenye vyombo hivyo.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti Taarifa!

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji anaendelea kuchangia, anatumia jina langu vibaya, wananchi wa Tarime walikuwa *live* kwenye *tv* wanamuangalia Rais anavyozungumza kuhusu Kampuni *ACACIA* na mimi kama Mbunge wao nilisema humu kwamba sisi tumeumizwa na kwa sababu Kampuni imethibitika ni *fake,* kwa sababu sio sisi tuliochunguza, wananchi wachukue hatua ya kuzuia mwizi ndicho nilichosema. Kwa hiyo, kama unafikiri mimi naogopa kuunganishwa njoo uniunganishe wewe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline, taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Heche nakuonya usirudie tena kunipotezea muda, naendelea kama ifuatavyo, nina mambo mengi ya msingi ya kuchangia hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchunguzi uliofanyika ni sahihi na ripoti ambayo imeletwa kwa Mheshimiwa Rais ni sahihi na ninaomba ikumbukwe kwamba uchunguzi unapofanyika na ripoti inapopelekwa maana yake mwenye haki wa hiyo ripoti ni yule ambaye aliagiza ripoti ifanyike ambaye ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, kifo cha nyani kila mti huwa unateleza, imefika mahali hawa wenzetu sasa hata wanayoyasema kwamba Rais anatekeleza waliyoyasema wao, leo hii wanayakataa tuwaeleweje? Lakini pia amesimama Mbunge hapa, ametumia dakika 10 Mbunge wa Arumemeru Magharibi ametumia dakika 10 kulalamikia shamba la maua la Mheshimiwa Mbowe, hivi ni akili ni matope. Wananchi wake hawana shughuli zingine, hawana changamoto ni mambo ya aibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia alisimama Mbunge hapa akasema sisi Wapinzani ni kioo cha Chama cha Mapinduzi, mimi sikatai, inawezekana kuwa ni kioo, lakini kioo cha sasa hivi cha huo upinzani tayari kina *crack* hivi mtu utajionaje? Kioo kina ukungu utajionaje, ninyi wenyewe mnaenda mbele, mnarudi nyuma hamjitambui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba lakini pia niseme, kwa maana hiyo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja na

*waache na kula hela za msiba wa Mheshimiwa Ndesamburo. (Kicheko/Makofi)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Subiri kidogo Nkamia.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa kanuni ya 64 pamoja na kanuni ya 63, mchangiaji aliyemaliza hapa kuchangia sasa hivi, pamoja na mchango wake alioutoa, lakini amemalizia kauli kwamba waache kula hela za rambirambi za Mzee Ndesamburo. Tunaomba afute kauli yake na atuombe radhi ndani ya Bunge kwa sababu anachoongea ni uongo na au athibitishe haya maneno anayoyasema.

Mwongozo wa pili Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Mwongozo mmoja tu umeniomba.Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Ngonyani, nakuomba ufute haya maneno ambayo umeyatamka mwisho.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijawaambia wao labda kama wanajihisi.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, sasa mnaleta matatizo, nimempa fursa afute haya maneno, nyinyi mnapiga makelele sisikii, msinijibishe wewe Mheshimiwa Paresso tulia, Mheshimiwa Hawa, Mheshimiwa futa tu haya maneno.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni mambo ya msiba nafuta.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. JUMA S.NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii, ili na niweze kuchangia kwenye Bajeti Kuu ya Serikali ya mwaka 2017/2018.

Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu *Subhana Wataala* kwa kunijaalia kuwa na afya njema wa Bunge wote katika Bunge hili la Jamhuri ya Mauungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze sana Dkt. Mpango na dada yangu Dkt. Ashatu kwa bajeti nzuri sana, bajeti ambayo inaonekana dhahiri kwamba ikitekelezeka nchi yetu itafikia hatua nzuri sana ya maendeleo. Bajeti ambayo inamgusa kila Mtanzania kwa nafasi yake, mkulima, mfanyakazi, mwanafunzi na Watanzania wote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, bajeti hii sasa iende kwenye maeneo yaliyodhamiriwa. Watanzania wengi tatizo kubwa maji, nashangaa leo Mbunge wa Pangani, Mto wa Pangani umepita katikati ya Mji wa Pangani lakini wananchi wanalia maji. Chemba kule tuna matatizo makubwa ya maji, fedha ziende kwa ajili ya kukamilisha miradi ya maji. Tukimaliza hili, twende kwenye tatizo la nishati ya umeme; wananchi wakiona mambo haya yanafanyika naamini kabisa kwamba nchi yetu itaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara, ninasikitika kwamba kuna Mbunge mmoja hapa, nisingependa kumtaja jina, alisema barabara ya lami ya kutoka Dodoma kupita Chemba, Kondoa kwenda Arusha haina manufaa kwa wananchi wa Chemba.

Wananchi wameniambia nimsihi tu kwamba, kama yeye hapendi kupita kwenye barabara apite porini. Eeh! Lakini Wabunge wa Arusha, Manyara na kwingine kote, wanaunga mkono juhudi za Serikali kuhakikisha kwamba barabara hii inakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukitoka Arusha, Dodoma masaa manne, lakini mtu anabeza juhusi za Serikali katika kuhakikisha kwamba barabara hii imejengwa kwa kiwango cha lami. Mwenyekiti wewe ni shahidi ulipotoka Moshi kupita hapa, ulipokuja hapa ukasema hivi ile ni barabara ama kiwanja cha ndege. Vijiji vilivyoko karibu na barabara hii maisha yao yameanza kubadilika kwa wale wanaojishughulisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama mtu hajishughulishi anasubiri barabara ile iende mpaka chumbani kwake, haiwezekani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa nadhani kwamba ni vizuri tuunge mkono juhudi za Serikali zinazofanywa bila kujali tofauti yetu. Maslahi ya Taifa hayana mgawanyiko, maslahi ya Taifa lolote hayana mgawanyiko, ningeomba pia bajeti hii ijielekeze zaidi kwenye elimu. Pia ni vizuri mkafanya *analysis* kidogo kuhusu fedha zinazo kwenda kwenye shule hizi za msingi huko vijijini, zinafanya kazi iliyokusudiwa? Nina wasiwasi kwamba inawezekana fedha nyingine zina kwenda huko kwenye hili suala la elimu bure bado fedha zile hazifanyi kazi iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Mheshimiwa Waziri niliwahi kusema nilipoingia Bungeni kwa mara ya kwanza hapa hebu lete kwenye *financial bill* ile tozo ya ving'amuzi ili *TBC* iweze kuendelea. Muache kutoa fedha kutoka Hazina kupeleka *TBC* ichukuliwe fedha ya ving'amuzi ambayo itakwenda kuendesha shirika la umma lile. Na mimi nitakuwa mwizi wa fadhila nisipompongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwenye hili suala la makinikia. Nitoe rai kwa Wabunge wenzangu kwa wana CCM wenzangu wote tunakadi za kijani hakuna mwenye kadi ya kijani zaidi ya mwingine, tumuunge mkono Mheshimiwa Rais kwenye hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wapinzani maslahi ya Taifa hayagawanyiki, tuungane sote, Mheshimiwa Rais ameonyesha jambo jema baada ya kuunda tume zile mbili.

Kwa mliosoma mambo ya *negotiations*, kuna aina mbili za *negotiation* baada ya jambo hili. Kwa kuwa sasa sisi kama Taifa tumekuwa na *power* kwenye *negotiation* itakayofuata kwenye *compromise negotiation,* nina amini kabisa tutafaidika na jambo hili. Jambo hili linahitaji umakini mkubwa sana, ni jambo linalohitaji akili ya kutosha Mheshimiwa Rais ameshaonyesha njia, nina wasiwasi kwamba inawezekana kabisa tusipate ile trilioni 1.08; kwa sababu ni suala la *negotiations.* Lakini tunapokuja kwenye mjadala huu *automatically* kwenye *win win situation* nchi yetu itafaidika. Ndio maana nikasema wapinzani, wana CCM tuungane pamoja tum-*support* Mheshimiwa Rais kwenye jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hawa wachimba madini wanakwenda kuweka mgodi mkubwa sana kule Chemba, endapo jambo hili litafanikiwa na tukawa na *win win situation, automatically* hata wananchi wa Chemba watapata mafanikio kwenye huo uwekezaji unaokuja kule Chemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni suala la kisheria, mimi sio mwanasheria, lakini kwa kuwa sio kuku na sitagi mayai lakini najua yai viza ni lipi? Tufike mahali, si rahisi na siamini hivyo kwamba mikataba ikusanywe na maroli iletwe hapa Bungeni siamini. Kinacholetwa Bungeni ni muswada wa sheria sisi Wabunge tusimame kuhakikisha kwamba tunabadilisha Muswada wa Sheria ili nchi yetu iweze kufaikika kutokana na madin haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine nashangaa kusikia Mbunge anasema leteni mikataba hapa Bungeni, maana yake unazungumza maroli mawili/matatu na hilo sio jukumu la Bunge, jukumu la Bunge ni kutunga sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwamba endapo sheria hii ikija wote tuungane pamoja wapo wanasheria humu watusaidie tuone ni namna gani nchi yetu inaweza kupata mafanikio kwenye suala hili la uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana nikasema Mheshimiwa Rais ameonyesha ujasili wa hali ya juu sana, lazima tumuunge mkono, lazima tushikamane wote wapinzani, wana CCM na ndio maana nikatoa mwanzoni nikasema sisi wote Wana-CCM hakuna mwenye kadi ya kijani zaidi kuliko mwingine lazima tuungane wote tu kwa sababu kadi zetu wote zinafanana. Niombe na wapinzani tuungane kwenye jambo hili na nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mbunge wa Iringa Mjini, Mheshimiwa Peter Msingwa aliposema suala la maslahi ya Taifa halina mgawanyiko mimi chama fulani, mimi chama fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bomba la mafuta kutoka Uganda linapita Singida, linapita Chemba linakwenda Tanga. Naomba ajira zitolewe kwa watu wa maeneo hayo, lakini pia wananchi waelezwe mapema litapita kwenye vijiji vipi? Sambamba na hilo ile barabara ya Handeni, Kiberashi, Kibaya, Chemba, Donsee, Lalta, Farkwa, Kinyamshindo hadi Misung'aa kule kwa Mheshimiwa Tundu Lissu ambayo inajengwa kwa kiwango cha lami kazi ianze sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu umekwisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Nape, ajiandae Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri waliyofanya. Kwa kiasi kikubwa Mheshimiwa Waziri mmejitahidi kusikiliza kelele za Wabunge hapa na ambao ndio wawakilishi wa wananchi na kwa kweli bajeti hii kwa kiasi fulani na kwa kiasi kikubwa ime-*reflect* ambacho tulikuwa tukikipigia kelele. Kwa hiyo, nadhani ni mfano mzuri wa Serikali kuwa sikivu kwa wale ambao inawasimamia hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayofanya na hasa kwenye usimamizi wa rasilimali za nchi yetu. Nadhani

ameonyesha mfano mzuri na kwa mjadala unavyoenda nadhani watu wengi wanamuunga mkono, wanaweza kupatikana wachache ambao pengine wana mawazo tofauti, lakini hiyo haitufanyi tusisonge mbele na msimamo wa kulinda rasilimali za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ambalo ningelipenda kulisema katika hili nadhani ni vizuri ukweli huu ukasemwa kwamba hizi juhudi za kulinda rasimali za nchi yetu hazijaanzwa na Awamu ya Tano, zimeaanzwa kutoka Awamu ya Kwanza ya Mwalimu Nyerere kuna mambo aliyafanya katika kuhakikisha rasilimali za nchi yetu zinalindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo aliyafanya hata kama kunaweza kuwa na mapungufu. Awamu ya Pili ya Mzee Mwinyi yako mambo aliyafanya, Awamu ya Tatu ya Mzee Mkapa yako mambo aliyafanya, Awamu ya Nne ya Mheshimiwa Kikwete yako mambo aliyafanya mazuri. Kwa hiyo, hakuna namna ambayo tutapuuza juhudi zilizofanywa na watangulizi wa Mheshimiwa Magufuli, kwa sababu nao wana mchango hata kama leo yataonekana yalikuwepo mapungufu lakini kwa nafasi yao walitimiza wajibu wao. Na ni vizuri tukatambua mchango wao na kuuheshimu mchango wao badala ya kubaki tunawanyooshea vidole kama vile hawakufanya lolote kabisa katika juhudi za kulinda rasilimali za nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukisoma Ilani zote za Uchaguzi za Chama cha Mapinduzi, tumezungumza habari ya ulindaji wa rasilimali zetu. Kwa hiyo, hiki anachokifanya Rais anatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ambayo ndio mkataba wa CCM na wananchi tukiunda Serikali. Hapa nitanukuu Ilani ya Uchaguzi inasema hivi; "kubuni na kutekeleza mikakati mahsusi itakayowezesha kupunguza au kukomesha kabisa vitendo vya utoroshaji wa madini kwenda nje ya nchi na biashara haramu ya madini nchi." Kwa hiyo, iko kwenye Ilani ukisoma mwongozo, ukisoma muelekeo wa sera kote tumezungumza. Alilolifanya Rais Magufuli ambalo ndilo tunalomuunga nalo mkono

ametupeleka kwenye hatua kubwa zaidi ukilinganisha na hatua tulizozichua mwanzoni. Lakini anajenga kwenye msingi ambao ulishaanzwa na wenzake, kwa hiyo, kwa kweli tusitenganishe na kufanya kama vile waliopita ni waharifu hivi, hapana. Naamini walitimiza wajibu wao Magufuli anatimiza wajibu wake tumuunge mkono. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Safi.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na katika hili tunaweza tukagawanyika katika mitazamo, wapo wale wanaunga mkono asilimia 100, wapo wale wanaopinga kwa namna wanavyowaza wao. Sasa kelele zisiturudishe nyuma lazima tusonge mbele kwa sababu vita hii ni takatifu, lakini tusipuuze katika kelele nyingi kunaweza kuwa na ushauri mzuri ndani yake. Tusifike mahali tukapuuza kabisa nadhani sio jambo jema, hii vita ni yakwetu wote nchi hii ikifaidika na jambo hii ni faida kwetu wote bila kujali itikadi zetu za vyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tusitoboane macho, tusitupiane vijembe visivyokuwa na sababu ni wakati wa kuileta nchi yetu pamoja twende tukapigane hii vita tuishinde. Kwa hiyo, wapinzani na CCM na watu wengine wote kwa ujumla wetu bila kujali tofauti zetu nadhani ni vizuri tukaungana katika hili, tuondoe tofauti zetu tusitafute mchawi kati yetu wenyewe sisi tuungane. Kama vita yoyote safari yoyote inaweza kuwa na mashimo na mabonde kunaweza kuwa na ghrama za vita hii, tukubali kuzilipa faida yake ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Rais kwa kazi hii na nadhani sasa ni wakati mzuri tumuunge mkono kama yako maeneo ya kurekebisha, kushauri tushauriane ili vita iishe salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ambalo nilitaka nilizungumzie Mhehimiwa Waziri uchumi wa gesi na mafuta. Sisi Kusini, Mikoa ya Lindi na Mtwara gesi na mafuta ndio ilikuwa inazungumzwa kuwa ni ukombozi. Bahati mbaya

ugunduzi ulipopatikana habari zilizotolewa ni kama vile ndio tunageuza siku moja kule kuwa nchi ya asali na maziwa. Na ninyi mnajua habari ilipotoka kukatokea vurugu kubwa sana Lindi na Mtwara, kwa sababu habari iliyopelekwa kwa wananchi ilijaa chumvi nyingi badala ya kupeleka ukweli kwamba faida ya gesi yenyewe iliyogunduliwa na mafuta inaweza ikatuchukua zaidi ya miaka 20, 30 kabla hatujaanza kuifaidi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wako wananchi waliokata mikorosho yao wakiaamini biashara imeisha, wako watu waliokaa na kubweteka wakadhani mambo yameisha. Sasa nadhani hili lilikuwa kosa moja kubwa sana ndio maana ikatokea vurugu ya Lindi na Mtwara juu ya gesi na bomba lake na mambo yote yaliyoendana na hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi tulidhani kwamba mchakato kuelekea huko kwenye kufaidika ungeenda vizuri na kwa wakati. Na hapa nataka nizungumzie ujenzi wa mtambo wa kuchakata gesi *(LNG plant)* pale Lindi. Kwetu sisi huu ndio ungekuwa ukombozi wa mwanzo wa kuanza kuyaona matunda ya ule ugunduzi, bahati mbaya hali ilivyo ni kama vile hili jambo linasuasua sana na linawezekana kabisa sijui lisiwezekane linatupa tabu. Kwa sababu leo makampuni yote matano ambayo ndio yangeshirikiana katika ujenzi kinu hiki, ukichukua *British gas, orfil energy, start oil*, *Exon Mobil* na hata *Petrobrass* tulidhani ofisi zao zingekuwepo Lindi na Mtwara na ziwe *active,* tulidhani vifaa vyao mahelkopta yao yale, meli zao zile leo hazionekani? *(Makofi)*

Sasa tunataka Serikali ituambie kinachoendelea ni nini huu mradi bado upo? Ukisoma kwenye hotuba ya Nishati na Madini unaona imezungumzwa ka-*para* kamoja lakini kweli mradi mkubwa wa zaidi ya dola bilioni 33 kitu unazungumzwa kwa *para* ndogo kama vile hakuna kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Serikali hapa kuweni *serious* tuambieni ukweli huu mradi upo au haupo?

Na kama haupo tujue namna ya kufanya na kama upo unaanza lini tulijua mwanzoni tatizo lilikuwa ni ardhi. Rais amefuta hati hili jambo lilitakiwa liwe limekwisha kwanini bado inaendelea hivi na ziko habari kwamba hawa jamaa sasa wanahamia Msumbiji, tuambieni ukweli hali ikoje, mradi upo au haupo? Na tungedhani kwa sababu mradi huu ungeanza uchumi wa Lindi ungebadilika, pesa zingeingia nyingi hata katika ile *process* yenyewe tu ya kuujenga huu mradi ambao ungechukua zaidi ya miaka nane, lakini zaidi ya dola bilioni nne zingiingia Lindi zingebadilisha maisha ya watu wetu pale. Lakini kwa hali tunavyoenda nayo tunapata mashaka. Sasa ni vizuri Serikali tukawa wa kweli, kauli ya Serikali itolewe katika jambo hili, tukowapi, tunaenda wapi, nini matumaini ya mradi huu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka nilizungumzie la mwisho nadhani kwenye hotuba yako Mheshimiwa Waziri pamoja na uzuri wa hotuba hii, lakini kuna mahali umezungumzia sera za mapato. Hapa ukisoma umeweka mipango karibu saba, lakini Mheshimiwa Waziri mipango yote inalenga kubana na kukamua wakwepa kodi na kukamua ukusanyaji wa kodi. Sijaona mpango *straight* unaozungumza namna ya ku-*stimulate growth* ya *economy* ya nchi yetu. Sasa kama hata...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kakunda jiandae Mheshimiwa Ahmed Ally.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kusikiliza maoni ya Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili nampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli Mwenyekiti wa CCM kwa kazi iliyotukuka aliyoifanya katika kipindi cha miezi 18 iliyopia na nina muomba Mungu ampe nguvu zaidi ili aendelee kutusaidia kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amefanya kazi nyingi lakini nitanukuu chache hapa; "kusimamia uadilifu katika ukusanyaji wa mapato na nidhamu ya matumizi, kuondoa watumishi hewa, wanafunzi hewa, madeni hewa na vyeti *fake,* kuhamishia Serikali Dodoma baada ya miaka 44 baada ya uamuzi, kutekeleza mpango wa elimu bure, kuvunja *CDA* baada ya miaka 42, kufufua shirika la ndege, anajenga reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa, anajenga bomba la mafuta kutoka Uganda hadi Tanga, anaendelea kujenga barabara za lami hadi Sikonge hadi Mpanda itafika, analeta maji ya Ziwa Victoria hadi yatafika mpaka Sikonge, amapeleka umeme vijijini kwa kasi kubwa na mambo mengine mengi sana kuhakikisha kwamba ajenda ya uchumi wa viwanda inatekelezwa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, tuna Rais ambaye halali usingizi kila siku anafikilia namna ambavyo atahakikisha anasimamia rasilimali za nchi ili zinafaidishe zaidi Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwenye maeneo mawili hasa; kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Madini kinachompa mamlaka Waziri kuingia makubaliano ya uwekezaji au *mineral development agreement* na wawekezaji, na hao wawekezaji wanapewa *mineral ownership rights.* Mheshimiwa Waziri mhusika wa sekta husika pamoja na Profesa Kabudi wanakumbuka jinsi tulivyorekebisha kwenye sekta ya maji tuliondoa kitu kinaitwa *water right* badala yake tukaweka *water permit*. Kwa hiyo, hiki kipengele kinatakiwa kifanyiwe marekebisho haraka sana ili kusudi kuweza kuhakikisha kwamba madini yetu hayamilikiwi na wageni, madini yetu yanamilikiwa na Watanzania wenyewe kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kwenye sekta ya gesi kuna *production sharing agreement* na tuna tatizo kubwa sana la wataalamu kwenye sekta ya gesi yasije yakajitokeza matatizo kama yaliyoonekana kwenye sekta ya madini. Inatakiwa tuwe makini sana kwenye sekta ya gesi ili tujiandae vizuri tusije tukapata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *point* yangu ya tatu ni kwenye hali ya uchumi. Hali ya uchumi ambayo imenukuliwa kwenye vitabu vya taarifa ya uchumi Pato la Taifa kukua kwa kiwango cha asilimia 7.0 sio mafanikio madogo kwa nchi yetu, ni mafanikio makubwa sana. Kwa viwango vya kimataifa vya ukuaji wa uchumi, tuko juu ingawa baadhi ya wananchi wetu walio wengi bado ni maskini, kwa hiyo naipongeza Serikali. Tuendelee kuhakikisha kwamba shughuli zetu za ujenzi, mawasiliano, usafirishaji, uchimbaji wa madini na mawe ambazo zimechangia zaidi ukuaji huu wa Pato la Taifa tuziimarishe zaidi na sekta nyingine tuweke nguvu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ambazo tunahitaji kuongeza nguvu zaidi ni sekta ya kilimo, sekta ya ardhi, sekta ya maliasili na utalii ambako napo kwenye sekta ya maliasili na utalii kuna majangili wenye vibali, ni hivi lazima tuangalie kwa makini sana. Maana yake kama huku kwenye madini wenye leseni wanatuletea matatizo ya kutuibia madini na kwenye sekta ya maliasili na utalii kuna majangili ambao wana vibali, ambao wanasumbua sana nadhani tutaendelea kukosa mapato mengi kama hatutawaangalia kwa jicho la karibu watu kama hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuboresha mazingira ya biashara ni pamoja na kuwasajili wote ambao wako kwenye sekta isiyo rasmi, hayo ni mambo ya msingi sana. Tumefanya vizuri sana kwenye bajeti yetu ya mwaka 2017/2018 kufuta matozo mengi kwa wakulima, kufuta kodi ya leseni ya magari, kuondoa ushuru wa huduma kwenye *Guest Houses* ni miongoni mwa mambo machache ambayo ni mazuri kuifanya bajeti yetu hii iwe ya kihistoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo ambao wanabeza mafanikio, wengi wanaobeza mafanikio wanabeza kwa sababu tu ya hasira ya mafanikio kwamba hii Serikali ya CCM imepata mafanikio. Kwa hiyo, wanakuwa na hasira hawapendi, wangependa tusipate mafanikio ili kusudi wao wapate sasa sehemu ya mambo ya kusema wananchi. Kadri ambavyo Serikali ya CCM inapata mafanikio wanakosa cha

kusema kwahiyo lazima wakasirike ndiyo maana wanakuja juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hotuba ya upinzani, ziko takwimu chache zimewasilishwa humu, kwa kweli jinsi hotuba hii ya upinzani ilivyo kubwa na takwimu zilivyo chache, inaonekana kabisa kwamba ndugu zetu kadri siku zinavyoenda wanakosa cha kusema na mimi nilikuwa nafikiri wangepata ushauri kutoka kwa Mawaziri Wakuu Wastaafu wangeleta hotuba ambayo ni nzuri zaidi kuliko hii waliyoleta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu kwenye Katiba, Katiba yetu ina Sura Kumi. Sura ya Pili, Sehemu ya Tatu inazungumzia Waziri Mkuu, Ibara 52(1) Waziri Mkuu atakuwa na mamlaka juu ya udhibiti, usimamiaji, utekelezaji wa siku hata siku wa kazi na shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano (2) Waziri Mkuu atakuwa kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni sasa Mawaziri Wakuu Wastaafu wawili Mheshimiwa Lowassa na Mheshimiwa Sumaye, kama wangepewa hotuba ya upinzani wasome ili watoe ushauri, hii hotuba hii waliyoleta ingekuwa ni nzuri zaidi kwa sababu wao wana-*experience* kubwa sana katika masuala ya kuendesha Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa ambalo ningependa nizungumze ni kuhusu Wilaya yangu ya Sikonge. Wilaya ya Sikonge kubwa sana, kilometa za mraba 27,873 kubwa kuliko maeneo ya Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro inaingia mara mbili kwenye Wilaya yangu, Mara, Kagera, Rukwa, Dar es Salaam, Mtwara, Zanzibar na Pemba inaingia mara 12; Njombe, Simiyu, Shinyanga, Geita, Mwanza, Songwe, mikoa yote hii ni midogo kuliko Wilaya yangu ya Sikonge. Sasa kwa nini Serikali isitoe tamko la kuanzisha Wilaya mpya kwenye Tarafa ya Kitunda au Kiwele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka Pangale kijiji cha kwanza unapotoka Tabora Mjini kwenda Sikonge, kutoka Pangale hadi kijiji cha mwisho cha Matagata ni kilometa 416.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa mzungumzaji anayezungumza juu ya hotuba ya upinzani kwamba Mheshimiwa Sumaye na Mheshimiwa Edward Lowassa walipewa hiyo hotuba, wakaisoma, wakaweka *input* zao na ndio waliyosema kwamba Mheshimiwa Sumaye aliunda Kamati ya Madini na kwamba makinikia wao hawakusaini mikataba.

Kwa hiyo, nampa hiyo taarifa mzungumzaji aelewe kwamba anachokizungumza sio sahihi, usahihi ni kwamba Mheshimiwa Sumaye na Lowassa walisoma hiyo hotuba na ndiyo maana imekuwa hotuba bora kabisa ya upinzani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kakunda taarifa.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina wasiwasi na taarifa yake kama ni sahihi kwa sababu mimi nimefanya kazi na Mheshimiwa Lowassa kwa karibu sana yeye labda hamjui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea, kutoka Pangale hadi Matagata kuna kilometa 416 sawasawa na kutoka Dodoma hadi Chalinze hivi ni Wilaya gani katika nchi hii unaipata ya namna hiyo, Wilaya gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaye Mkuu wa Wilaya mchapa kazi, tuna Mkurugenzi mchapa kazi safi kabisa, lakini kuna maeneo tangu waje hawajawahi kufika na huwezi kuwalaumu kwa sababu kwenda kama Matagata lazima ajaze *full tank* gari na bado kuna mafuta mengine yanatakiwa yawe kwenye dumu. Sasa gharama za uendeshaji wa namna hiyo nani ataziweza. Tumekubaliana kwamba tuanzishe

ajenda ya kisheria iende kama sheria inavyotaka, kwamba tupitishe kwenye Kamati za Vijiji, kwenye Kata, iende Wilaya, iende Mkoani halafu ije kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alipokuwa Nzega alisema kwamba yeye hatarajii kuanzisha Wilaya mpya wala Mkoa mpya, kwa hiyo, hapo viongozi wanakuwa na kigugumizi kidogo namna ya kutekeleza hii.

Naomba kwa makusudi kabisa namuomba Mheshimiwa Rais huko aliko kwa makusudi kabisa, Sikonge tupate Wilaya mpya na ninajua hili Mkuu wangu wa Wilaya na Mkuu wangu wa Mkoa wananisikia hapa na nimeishazungumza na Mheshimiwa Waziri Mkuu suala hili ni muhimu sana, kama mwananchi wa Matagata anahitaji kumuona Mkuu wa Wilaya anatakiwa atumie siku tano, siku tatu za kusafiri, siku tatu za kurudi nyumbani, siku sita, kwa uchache kabisa siku nne, sasa kwa nini wananchi katika nchi hii moja wawe wanapata adhabu na wananchi wengine hawapata adhabu kama hizo. Kwa hiyo, tunaomba sisi Sikonge tupate Wilaya mpya, Mheshimiwa Rais akubali tupate Wilaya mpya. *(Makofi)*

La mwisho tuna sababu nyingi lakini sababu kubwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Ahmed Salum, ajiandae Mheshimiwa Susan Kiwanga, na ajiandae Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, kwanza kabisa naunga hoja bajeti hii kwa asilimia 100. Katika hoja ya mpango aliyoleta Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tulimshauri mambo mengi, tulimshauri suala zima la bandari kachukua, kaweka

mezani kafanyia kazi, tukamshauri masuala haya ya leseni za magari, kachukua, kaweka mezani na kafanyia kazi, tumemshauri mambo mengi sana kwa wakati ule na tuliongea kwa hisia na ndio maana nasema leo Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba nikupongeze sana umekuwa msikivu, umesikiliza ushauri wa Bunge na umelinyia kazi kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Hongera sana nakuunga mkono kwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna mawili machache madogo sana naomba nikudokeze, kuna wenzetu hawa wa bodaboda ambapo *SUMATRA* wamewaambia mpaka tarehe 30 wasipolipa 22,000 kutakuwa na *operation* moja kali sana na vijana hawa ndio wanaanza maisha katika Taifa letu hili, hebu lione hili katika kufata kodi hii, ili vijana hawa wa bodaboda waweze kufanya kazi kwa raha zao zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile sekta utalii, nilikuwa na rafiki yangu mmoja yuko Ulaya pale London na Marekani wakasema inakuwaje watalii wengi wanakwenda Kenya, tatizo ni nini, ukitazama kwenye *records* za watu wanaosafiri kutoka nchi za Ulaya ni asilimia kubwa sana wanaokwenda Kenya, zaidi ya kuja kwetu Tanzania. Kwa *research* ndogo tuliyofanya inaonekana, bado tatizo la *VAT on tourism sector* linaathiri mapato makubwa. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha litizame hili, lichukue nina imani kabisa kwa hekima zako unaweza ukalifanyia kazi, ama kama sio mwaka huu, kwa mwaka wa fedha ujao, lichukue ondoa kabisa wenzetu wa Kenya wanatuingiza mkenge kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tulikaa pamoja na Kenya, Wakenya wakaondoa wakasema sisi hatukujipanga, matokeo yake ni kwamba wametuacha sisi tumeweka *VAT* wao wameondoa *VAT* wameongeza watalii wengi sana katika nchi yao ya Kenya. Na hii Mheshimiwa Thailand inachukua asilimia 30 ya mapato yao katika utalii, naomba sana suala hili ni kubwa mno katika kuingizia mapato ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, huwezi kuongea bajeti hii kama huongei suala zima la makinikia. Makinikia ndiyo fedha na tunatarajia sana baada ya *negotiation* hii kwenye bajeti ya 2018/2019 tutakuwa na fedha nyingi sana itaweza kutekeleza mradi wa reli bila mkopo, anaweza akaongeza ndege, tunaweza tukaongeza miundombinu mikubwa ya nchi yetu tukaweza kufanana na nchi zote katika nchi za Afrika zilizopiga maendeleo. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru tena kwa mara nyingine Mheshimiwa Rais katika Kijiji cha Nyaligongo, Kata ya Mwakitolyo aliweza kufuta leseni ya mwekezaji na kusema kwamba wachimbaji wadogo wa Kata ya Mwakitolyo wasiondolewe, wachimbe, wanufaike na raslimali zao, kwa bahati mbaya sana mwekezaji aliyefutiwa leseni yake akafutwa akabakizwa mmoja mwekezaji Mchina, Mchina huyu amepewa leseni zaidi ya miaka nane, hakuna alichokifanya, ni utapeli, anachukua leseni anakwenda nchi za nje anapata pesa, anachukua mkopo na kuuza hisa katika mabenki ya nje. Tarehe 08 mwezi uliopita, Ofisi ya Mkoa kwa bahati mbaya sana ni masikitiko makubwa sana, imekwenda Mwakitolyo kwenye Kitongoji cha Mahiga wamewafukuza wachimbaji wadogo wadogo kwa mtutu, kwa polisi kwa kuwatisha na risasi zililia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamekimbia, wachimbaji wadogo wadogo wamekimbia, watoto watano wamepotea mpaka leo baada ya siku tatu, tathimini inafanywa kwa mtutu. Polisi anakwenda kwa familia anamuambia wewe kama haukubali hii, shauri yako itakula kwako, kwa mtu ambaye hajaja hajakuwepo ananyang'anywa hiyo haki.

Kwanza kabisa nimuombe Waziri wa Mambo ya Ndani kwa hekima na busara zote, polisi siwalaumu kwa sababu wale wanaamuliwa tu, siwalaumu sana Jeshi la Polisi ila namuomba Mheshimiwa Waziri aondoe Jeshi la Polisi kule kwa hekima zote, wananchi hawana raha Kata ya

Mwakitolyo, wanakaa kama wakimbizi na nimuombe Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, kama alivyowasaidia wanyonge hawa katika Kijiji cha Nyaligongo aendelee kuwasaidia kwenye Kitongoji cha Mahiga, ninaomba sana Mheshimiwa Rais afanye hivyo, namuomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, namuomba sana Mheshimiwa Makamu wa Rais na wote wenye maamuzi ya maeneo haya wawasaidie wachimbaji wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la njaa linapotokea katika nchi hii au upungufu wa chakula Mkoa unaoathirika ni Mkoa wa Shinyanga, namba moja, kwa hiyo kwa bajeti ijayo ninaomba sana, Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa sababu wewe ni Waziri wa Fedha na vilevile una mpango wa nchi nzima, suala zima la kukabiliana na tatizo la upungufu wa njaa ni kwenye *irrigation scheme* (kilimo cha umwagiliaji). Kwa mfano mimi nina kilimo cha umwagiliaji pale Nyida, nina kilimo cha umwagiliaji katika Kata ya Bukande ni kubwa zinaweza zikalisha Mkoa wa Shinyanga na mikoa mingine mitatu/minne mitano, kwahiyo ninaomba sana fedha ziweze kutengwa ili kukabiliana na hali ya njaa hii kwa miaka ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda, Mheshimiwa Magufuli anataka aitoe nchi hii yaani ingewezekana katika miaka mitano hii, tungeweza kufika mbali sana, lakini kwa bahati mbaya sana yako maeneo ni vikwazo katika *speed* ya Magufuli, Mheshimiwa Rais ana *speed,* kuna maeneo yanazuia. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, chukua *report* ya *REPOA,* chukua *report* ya *CTI* wanafanya kazi nzuri, kutaneni na wawekezaji ili mpate matatizo yanayofanya uwekezaji katika suala zima la viwanda kwenda kwa mtindo wa kinyonga. Ukipata hii Mheshimiwa Waziri wa Fedha, utakuja na bajeti ijayo ambayo utaisaidia na tutarekebisha sheria, ili *speed* ya Magufuli kwenye suala zima la Tanzania viwanda iende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tazama mfano wa Ghana, Ghana leo wame *demolish VAT on everything on the industry*

*on the manufacture industry* wamefuta kila kitu, ukitizama hapa hapa juzi tu Rwanda hawa, wanasajiri kampuni leo masaa manne *on line*, masaa manne wanasajiri kampuni hawataki kukuona wanakujibu wanakupa *registration card* wanakupa *TIN number,* wanakupa *VAT,* wanakupa kila kitu kwa masaa manne, juzi tu hawa, leo wanatushinda kwa namna gani. Ndiyo maana nasema tufanye *research,* tupate ukweli mzima kabisa wa namna gani kuweze kwenda *speed* ya Magufuli kwenye suala zima la viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TIB* tuwaongezee fedha benki hii ili iendelee kutoa mikopo na mnaweza mkawa *specifically* kabisa Mheshimiwa Waziri wa Fedha unajua ukawa *specifically* kabisa kwamba tunatoa fedha hizi ziende kusaidia mikopo ya viwanda na utoa riba kutoka asilimia 18 mpaka asilimia nane kama mlivyofanya kwenye kilimo, tunakwenda, tunatoka tu. Kwa hiyo, ni suala la ku-*negotiate* ni suala la kubadilisha sheria na kuiweka vizuri ili watanzania waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majengo, katika Jimbo la Solwa nina majengo mengi sana, mimi na wananchi tumejenga na tumefikisha kwenye usawa wa renta, na suala hili nazani ni la Taifa, la nchi nzima, hakuna Mbunge anaweza akasimama hapa akasema mimi nimekamilisha majengo kwa asilimia 100 hayupo. Mimi nina zahanati zilizofika renta 45, nina Hospitali ya Wilaya moja ambayo imefika renta, nina maeneo mengi ambayo ninahitaji msaada wa Serikali Kuu, sasa kwenye bajeti ijayo, najua bajeti hii itakuwa ni ngumu lakini weka tu kwamba kuwepo na mwongozo kwa majengo yote yaliyo tayari kwenye majengo yote yaliyofika renta vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, hospitali za wilaya, vituo vya afya vyote viwe *observed* kwenye bajeti ya mwaka ni ili tuweze kumaliza tatizo kwa sababu hayo ndiyo maendeleo ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukijenga vyumba vya madarasa, tukajenga nyumba za walimu zilizokuwa zimefika renta, tutakamilisha angalau kupunguza kwa asilimia 50 tutakuwa tumefika. *(Makofi)*

*(Hapa kengele Ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako, Mheshimiwa Susan Kiwanga atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Abdallah, ajiandae Mheshimiwa Agness Marwa na Mheshimiwa Aeshi.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema siku hii ya leo na kutoa mchango wangu kuhusu bajeti ya mwaka 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kabisa kwa moyo mkuu na akili zangu zote kuunga mkono maoni yaliyotolea na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Fedha na Mipango ya Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge ambayo imewasilishwa Bungeni kama maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Mheshimiwa Silinde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno yote yaliyozungumzwa humu yana mantiki na miaka yote bahati nzuri tangu niingie Bungeni hii ni awamu yangu ya pili kuna mambo ambayo tuliyazungumza kama Kambi na nimeona kwamba Chama cha Mapinduzi ndio kinatembea humo humo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo, pamoja na kwamba yakiletwa yanabezwa lakini utakuta labda wanajifungia chumbani na kuyachukua kuona kweli haya ndiyo maoni ya wananchi. Kwahiyo, ni muhimu sana Waziri mwenye dhamana akachukua, akatendea kazi na Rais wa Nchi, akachukua akayafanyia kazi kama anavyofanya sasa, kwa hiyo, ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingekuwa ni uungwana wa hali ya juu kama Chama Tawala kingekiri na Wabunge wenzetu wa Chama Tawala kingekiri walitukosea, walituzarau, walitubeza, lakini ndio ukweli wenyewe, sasa

hivi Awamu ya Tano ndio wanachukua na kuyafanyia kazi. Lakini sisi tunatimiza wajibu wetu kama Kambi tunawapa maoni, pale mnapoyatekeleza tunaona wananchi wetu ndio wanapata nafuu. Kwa hiyo, tutakwenda tu mpaka Watanzania wapate uelewa kwamba watuingize madarakani ili tuyatekeleze yale tunayowashauri. Kwa sababu mtu ukimshauri anaweza akayatekeleza, lakini wazo kwa sababu sio lake, hawezi akalitekeleza sawa sawa kwa mfano kama elimu bure, sisi tungeingia madarakani tungeifanya sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo hayo, nimeona kwenye kitabu hiki cha Waziri nataka niseme kwamba katika ukurasa 85 amezungumzia kuhusu *TAZARA* na nilivyokuwa naangalia nilizani anazungumzia reli ya *TAZARA,* lakini kibaya zaidi amezungumzia *TAZARA flyover* pale Dar es Salaam. Nataka nipate majibu ya Serikali ni namna gani sasa watumishi wa *TAZARA* walioenea katika Mikoa ya Morogoro mpaka Mbeya ni namna gani hatima yao kwa sababu hali ni tete wengine wamestaafishwa, hawajapewa mafao yao, Serikali imekaa kimya, *TAZARA* yenyewe ina kizungumkuti, haijulikani namna gani. Jamani hii hali inatisha watu wanateseka wameshindwa kusomesha watoto, wengine wamekufa, hawajui hatma yao, naomba nipate majibu ya Serikali, nini hatma ya *TAZARA* na wastaafu wa *TAZARA* na uboreshaji wa reli ya *TAZARA.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwenye barabara, kwenye kipindi cha miezi miwili iyopita hakuna mama aliyetoka Mlimba kwenda kwenye Hospitali ya Wilaya ya Rufaa Ifakara, barabara haipitiki, barabara zimekatika, barabara kilometa 230 Waziri asikie, nasimama hapa kila siku kilio ni barabara, wanaoteseka ni akina mama, watoto, wazee, hivi hata nikisoma hii bajeti inazungumzia *flyover*, ndege na mambo mengine treni. Mimi wananchi wa Mlimba wanaionaje hiyo bajeti, wanaona kama sio yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sasa watuhakikishie wananchi wa Mlimba Waziri wa barabara amefika kule lakini hali ni tete, na Meneja wa *TANROADS*

nimeongea naye anasema wakati Serikali inajipanga kujenga barabara ya lami, basi tupate hela za kutosha za kujenga angalau kilometa 50 ambazo tunyanyue tuta ili ile barabara ipitike mwaka mzima, lakini hela wanazopangiwa hazitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba hebu muwahurumie wananchi wakule na wale tuwe tumepata uhuru pamoja mwaka 1961, lakini mpaka leo wale watu kama hawajapata uhuru. Lakini eneo lile ndio linalotoka mazao ya kilimo, *Kilombero Planting Limited* iko pale Mngeta lakini hamna barabara. *TAZARA* haiboreshwi, barabara hakuna, hivi mnataka yale mazao watu wabebe kichwani na kule kuna kilimo kikubwa?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuhusu maji, Waziri amesema atakwenda lakini maji Jimbo la Mlimba ni mtihani, hivi mji mzima mdogo wa Mlimba hivi mtu anapata maji kwa siku saba mara moja, hivi kinamama kuna Mawaziri hapa akina mama, hivi mama anaweza akakaa akapata maji siku saba mara moja,huyu mama, msichana anaishi vipi katika mazingira gani. Anaenda kujifungua inakuwaje, kwa hiyo, shughuli za maendeleo kule tunalima, shughuli za maendeleo zinarudi nyuma kwa sababu tumekosa maji. Naomba haya maendeleo twende kwa pamoja, sio wengine wanasonga mbele, wengine tunarudi nyuma, haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mahakama, swali linakuja lakini kule hakuna mahakama, kilometa 230 mtu anatoka anakwenda kufuata mahakama ya Wilaya Ifakara, barabara hazipitiki kwahiyo kule haki hakuna. Yaani kule kama dunia ndio imeumbwa leo, yaani ni hatari, sasa vilio vyote ninavyosema ni vya uhakika. Vilevile kuhusu vituo vya polisi Mheshimwia Mwigulu ameenda kule amejionea mwenyewe, hakuna vituo vya polisi kule, hali ni mbaya sasa watu wanakosa mahakama, wanakosa vituo vya polisi, wamekosa barabara, wamekosa maji, hawa watu hebu muwafikirie, hivi wanaishi ishi vipi wale watu kule! Kwa hiyo hivyo ni vilio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji kule ni ndogo kuna mradi mmoja tu wa Njagi mito mikubwa inapita lakini hakuna umwagiliaji na kule Njagi wanamwagilia wakati wa mvua, wakati wa kiangazi hola, hicho ndio kinaitwa kilio cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu naenda kwenye makinikia, kwenye hii bajeti inazungumzia *flyover,* lakini wamegundua wanavyosema kwamba kuna makinikia yana *grams* chungu mzima za dhahabu na tutapata karibuni trilioni mia moja sijui na ngapi, sasa naomba hebu geuzeni tusubiri hizi za makinikia ambazo tunaenda kuzipata, zije zijenge reli hizo hela ambazo zipo sasa hivi kwenye bajeti hii tukaimarishe miundombinu vijijini kwa wanakijiji huko, ili hizo zinazokuja za makinikia tuweke sasa hiyo miundombinu tununue ndege nini, nini au vipi! Si hela zipo zinakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mikataba na sheria, iletwe Bungeni lakini tulipiga kelele nyuma hamna kitu. Kule Mahenge, Ulanga kuna mgodi mkubwa madini ya *graphite*, madini ya hali ya juu duniani, lakini mpaka leo wananchi wa kule hawajui hatma yao, mikataba yenyewe ndio hivyo imefungwa fungwa, mtuletee hiyo mikataba na sheria hapa Bungeni tuone tunaendaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, gesi na mafuta, yamegundulika Wilaya ya Malinyi kule Morogoro, Kijiji cha Ipela Asilia, lakini mikataba hata wananchi wa kule hawajui itawafaidisha vipi, kwahiyo ndio haya haya tunayoyasema sasa baadaye ndio mnasema sasa tumeibiwa tumeibiwa sasa si muanze sasa? Kwa nini mnangoja mpaka tuibiwe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba haya mambo twende kwa pamoja wote ni watanzania tunahitaji maendeleo, hatuhitaji matatizo kama hivi vyanzo vya Halmashauri wameshavipora huko juu, lakini kuna hiyo hoja kwamba ikifika mwaka 2025 Halmashauri zote ziwe zimejitegemea kwa 25% ile hoja mmeifuta au bado ipo? Zisije Halmashauri zikapata hoja za mkaguzi wakati

zimenyang'anywa mapato zitashindwa kufikia malengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sera vijiji lazima vifanye uchanguzi, nasema hivi Mrimba mpaka leo kuna vijiji vitatu havijafanya uchaguzi tangu mwaka ule wa uchaguzi wanasema kuna mwekezaji, sasa kwenye uwekezaji hakuna uchaguzi. Sasa ninachokiomba ile kesi iliyoko mahakamani.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah ajiandae Mheshimiwa Agness Marwa na ajiandae Mheshimiwa Aeshi.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wako mwingi wa Bunge hili umetumika zaidi kwa kujadili makinikia, na zaidi ya hilo umekwenda mbali zaidi kwa kuwataja Mawaziri ambao walifuatia, kuwataja wanasheria ambao walipita. Kufanya kitendo hiki cha kuwataja Mawaziri au wanasheria waliopita kisheria hasa sio sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameteua Kamati yake, na ameelekeza nini cha kufanya muache Rais afanye shughuli zake, sisi tujadili hotuba ya Bunge ambayo ni bajeti. Cha msingi ni kuhakikisha kwamba sheria zote za madini, maliasili na sehemu nyingine zote zinafumuliwa upya na kufanywa vizuri na kupitiwa mikataba mbalimbali ili tujue tunaanza wapi katika kuleta uchumi huu wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo niseme kwamba bajeti ni mpango maalum wa kupanga mfumo ule wa mapato na hatimaye kuweka matumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha msingi baada ya kukusanya ni matumizi, Mheshimiwa Waziri nitamnukuu katika ukurasa wake wa 14 anasema ifuatavyo; "Nidhamu ya hali ya juu katika matumizi lazima isimamiwe kwa nguvu zote ili kuhakikisha tathmini ya fedha inapatikana" lakini pia aliendelea; "kutokufanya matumizi pasipokuwa na kasma iliyoidhinishwa kwenye bajeti husika katika fungu husika." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri hapa amesisitiza nidhamu ya matumizi, mwaka jana tulikusanya 70.1% lakini Wizara zote zinalalamika hazina fedha za maendeleo, sasa fedha hii imetumika wapi, je, Waziri amekuja kutuambia kuna tatizo wapi, kwa nini Wizara zisipate hela za kutosha, kwa mfano, Wizara ya Kilimo 3.8%; Chuo Kikuu Dar es Salaam 0%; Wizara ya Maji 8%. Katika mwendo huu ni dhahiri kwamba kulikuwa hakuna nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali. Na nasema kwamba nidhamu lazima ianze juu ije chini, nidhamu ikianza chini isiende juu haina maana yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sidhani kwamba matumizi yaliyofanywa kwa mji kuhamia Dodoma ilikuwa *budgeted*, sifikirii kama hii ilipita katika bajeti. Na hii ndio iliyotikisa bajeti hii kufikia Wizara zote hazina fedha, kwa hiyo, nidhamu ni lazima ijengwe kutoka juu kwanza, halafu chini ifuate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala la utekelezaji wa bajeti. Kuna kasoro kubwa, bajeti mara hii ya maendeleo ilitekelezwa kwa 35% mpaka 40% na nchi haihesabiwi kama ina maendeleo mpaka itekeleze miradi ya maendeleo. Lakini *OC* 80% na maendeleo 35% mpaka 40%, Wizara haijatuambia ni kwa nini bajeti hii hata masuala ya maendeleo hayakupita vizuri, hawajatueleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika vipaumbele. Mheshimiwa Rais ailipohutubia hapa alisema atahakikisha anafuata maelekezo yote ambayo viongozi wengine walipita, ni vizuri ninukuu anasema katika hotuba ya uzinduzi

wa Bunge la Kumi na Moja mwaka 2015 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alieleza Watanzania kwamba; "vipaumbele vya Serikali kuhusu uchumi ni kuendeleza na kuimairsha misingi imara ya uchumi wa nchi iliyojengwa katika awamu ya uongozi uliotangulia."

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi bado nina wasiwasi Serikali hii ya Awamu ya Tano imetoa kipaumbele zaidi na msukumu mkubwa zaidi kwenye viwanda lakini msukumo mdogo kuja kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kinaongeza pato hasa mifugo 4.4%   na nasema kwa mfano *FAO* ilifanya utafiti na ikesama kwamba kama Mtanzania atakula nyama kilo 11 kwa mwaka ambapo kwa mwezi ni kilo moja au atakunywa maziwa lita 45 kwa mwaka ambapo kwa mwezi ni lita nne, au atakula mayai 72 kwa mwaka ambapo kwa mwezi ni mayai sita basi tutakusanya shilingi trilioni 20.  Hii ni sehemu ndogo tu, lakini pia Misri na Zambia ilitaka kununua nyama Tanzania tani 50,000.  Lakini Tanzania ilikuwa inazalisha tani 23,000, nchi ziko tayari kununua tani 50,000 sisi tuna tani 23,000, ng'ombe wanakufa, mifugo wanapigana na watu huko, nini soko la wakulima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inapoteza fedha hizi. Sasa ninasema wakulima elimu yao ni kilimo, maskini matibabu yao ni kilimo, maskini afya zao ni kilimo, leo Wizara haijapewa kipaumbele na Wizara hii ya kilimo. Tumepewa kipaumbele viwanda, viwanda hatujajua changamoto zipi, kilimo tumezoea changamoto zake, mwaka 2015/2016 awamu iliyopita Rais Kikwete alitoa pembejeo zenye thamani ya shilingi bilioni 78, lakini Mheshimiwa Magufuli kipindi cha mwaka 2016/2017 alitoa pembejeo shilingi bilioni 10, kutoka shilingi bilioni 78 mpaka shilingi bilioni 10 hii maana yake nini? Maana yake nyingine kwamba hana habari na kilimo, 65% ni kilimo, hii sekta kubwa ambayo inaajiri Watanzania, ni sekta ambayo sasa tunaipa mgongo tunakwenda kwenye viwanda hatujui changamoto zake zikoje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri ni lazima ukitaka tusitake kilimo ndio asili yetu, wewe hukuwa na profesa umekwenda kwenye kilimo, watu wote waliosoma hapa wamesomeshwa na kilimo, leo kilimo unatoa shilingi bilioni 10. Kwa hiyo hii kilimo sio mvua tu, kilimo mvua na pembejeo, pamoja na dawa za kilimo ili kuimaisha kilimo kiwe viruzi zaidi na kilimo cha biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii haiwezekani kabisa kuvumilika ni lazima tubadilishe mwelekeo turudi kwenye kilimo kwanza.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Agness Marwa ajiandae Mheshimiwa Aeshi, ajiandae Mheshimiwa Kanyasu na Mheshimiwa Magige hayupo nafasi yake atakuwa Mheshimiwa Chikota.

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwa bajeti hii iliyosheheni weledi na kuonesha kuwajali wananchi na hasa wananchi wa hali ya chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali katika bajeti hii iangalie jinsi ya kupata fedha mahali, shilingi hamsini au arobaini ili kumtua mwanamke ndoo kichwani na hasa mwanamke wa kijijini. Kule kwetu Mkoani Mara inafikia hatua wanawake wa kijijini inapofika jioni wanakosa hata hamu ya kuwapa mapenzi waume zao, kwa hiyo, niiombe sana Serikali ijitahidi kwa hili na iliangalie sana suala la maji na ikiwezekana hii pesa ya makinikia basi itakapokuja suala la kwanza liwe ni maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikumbushie suala la ahadi ya Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli lile la shilingi milioni 50 kwa wajasiriamali. Kwa kweli wananchi wetu wanaiulizia sana

hiyo pesa na ninaamini Mheshimiwa Magufuli hadi sasa kafikisha asilimia kama 98 hivi ya utekelezaji wake imebakia hiyo asilimia mbili ambayo ni hiyo shilingi milioni hamsini hamsini, Mheshimiwa Magufuli tunaiomba ili kusudi hawa ndugu zetu walale kabisa vitandani wajue hawana chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee zaidi naiomba Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya kushughulikia hili suala la kilimo, basi benki ya kilimo ipewe pesa na Serikali ili wapeleke mitaji vijijini, wananchi wangu wa Mkoa wa Mara mara kwa mara wanalalamika vyakula ni kutokana na hali halisi ya uchumi. Lakini pia ni kutokana hali halisi ya kwamba wanakuwa hawana mtaji na hawana vifaa, kwa mfano, wanatakiwa wakopeshwe na Benki ya Kilimo ili wafanye kilimo cha *irrigation,* kinaweza kusababisha kupunguza shida na matatizo kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimsikia kaka yangu Mheshimiwa Heche akiongea kuhusu suala la kuwaandamanisha wananchi kule mgodini, ni kweli hakuna asiyejua kwamba wananchi wa Tarime kule mgodini wameumia, wamepata makovu, lakini hili suala Serikali imeshalishughulikia kwa kiasi kikubwa sana, lakini pia Mheshimwia Heche anapaswa kujua yale malipo au zile fidia za wale wananchi Mheshimwa Rais muda si mrefu sana wananchi wote watalipwa na Mheshimiwa Magufuli hakubali wananchi wa hali ya chini wanyanyasike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya labda hana ripoti hiyo na mimi ntakapoenda kule kuwakabidhi wale wananchi malipo yao nitamwita Mheshimwa, kwa sababu Jimbo lake sasa hivi amemwachia Mheshimwa *DC* wa Tarime ndio mwenye Jimbo anaitwa Mheshimiwa Luoga, ikiwezekana Mheshimiwa Rais muangalie sana huyu umpe hata Ukuu wa Mkoa maana kwa kweli ana kazi kubwa sana ya kufanya kule Ubunge badala ya u-*DC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Magufuli kwa kazi nzuri

anayoifanya. Hawa wanaombeza Mheshimiwa Rais kwamba ooh! Sijui ananunua ndege! Mlitaka awanunulie magari ma-*vogue* ili kusudi muendee Majimboni kwenu. Wananchi wa hali ya chini wanapanda hizi ndege na bei au gharama za ndege zimeshuka na sisi Wabunge tuna uwezo wa kwenda Dar es Salaam kufanya shughuli zetu na asubuhi tukarudi Bungeni. Isitoshe hizo ndege ninyi wenyewe mnazipanda, kila siku tunakutana ndani ya hizo ndege, kwa nini msiache kupanda? *(Makofi)*

Kwa hiyo, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais na kwa taarifa yenu kinakuja kitu kipya tena mwezi ujao. Hiyo ni kuonyesha jinsi gani Mheshimiwa Rais anavyotekeleza utekelezaji wake au kutekeleza Ilani aliyoiahidi. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuhusiana na masuala ya miundombinu hasa barabara. Hivi ni kweli kwamba hamuoni wakati tunawaona huwa mnaondoka hapa siku ya Jumamosi na Jumapili mnarudi hapa na Jumatatu mnakuwa Bungeni tena kwa magari. Zamani mlikuwa mnaenda hivyo kukiwa kuna mabonde?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kutoka hapa Dodoma mpaka Musoma kupitia Singida ilikuwa inatumika siku tatu lakini leo unaondoa asubuhi, jioni unafika na kesho yake unarudi unafika Bungeni na kipindi hicho Mheshimiwa Magufuli alikuwa ni Waziri wa Barabara. Kwa hiyo, mnapaswa kujua kwamba ametekeleza kwa kiasi gani au ametekeleza amefikia hatua gani. Hata wewe ukiamka nyumbani kwako sio kila kitu unachokitekeleza kwa siku moja! Mambo yanaenda taratibu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Mheshimiwa Aeshi, ajiandae Mheshimiwa Kanyasu, ajiandae Mheshimiwa Chikota na ajiandae Mheshimiwa Kikwembe.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye hotuba hii ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri. Kwanza kabisa naomba nimpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa, kazi ya uzalendo, kazi ya kujitoa na kuhakikisha anatetea maslahi ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu kuwakumbusha Wabunge tukumbuke nyuma tulikotoka, Tanzania haikuwa kama hivi ilivyo leo. Wako watu walioumia, wako watu waliopoteza nafasi na wako watu waliopoteza muda wao kulitumikia Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabisa naomba niwapongeze viongozi wote waliotangulia kwa kazi kubwa sana waliyoifanya. Ndiyo maana mpaka leo Chama cha Mapinduzi kiko madarakani kwa sababu naamini kila baada ya miaka kumi tunabadilisha uongozi na bahati nzuri Chama cha Mapinduzi kinashika nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yake yote kwa ujumla inafanya kazi kubwa na ninaamini kabisa tunakwenda mpaka mwaka 2025 amalize muda wake yaani miaka kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuwa msikivu. Mwaka jana ni miongoni mwa watu niliochangia bajeti hii ya Wizara ya Fedha. Lakini kwa bahati mbaya wako baadhi ya Mawaziri waliniomba mwongozo kuhusiana na jambo la *VAT on transit goods.* Lakini leo nimeona wakishangilia. Hili nilitaka niliweke sawa tu kwamba ni vizuri na sisi ambao hatuna *Ph.D* tunapokuwa tunachangia, mnatusikiliza. Sisi wengine tunafanya biashara, sisi wengine tumezaliwa humo humo kwenye biashara, kwa hiyo, tuna baadhi ya mambo tunayajua muwe mnatusikiliza na tuna *Ph.D* za mitaani. Sasa Mheshimiwa Waziri nataka niombe sana pale ambapo sisi tunataka kuchangia basi yale mambo ya msingi muweze kuyachukua na kuweza kuyafanyia kazi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la *VAT on transit goods* tulilipigia kelele sana lakini mmelichukua mwaka huu mmeliondoa. Ninavyoona kwa bahati mbaya sana, mmeliondoa mmewekea kipengele cha wiki moja. Baada ya wiki moja mnawachaji tena *VAT* kwa mzigo unaokwenda nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka turekebishe, turekebishe jumla! Nataka kushauri tu, Mheshimiwa Waziri, basi *at least* wekeni hata siku 30 kwa sababu kwa wiki moja kwa Bandari yetu ya Dar es Salaam na *TRA* yetu ya Dar es Salaam kila siku *system* iko *down.* Wiki moja itapita na matokeo yake tutawa-*charge* tena upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kukuomba sana Mheshimiwa Waziri hili uliangalie, kesho unapokuja hapa basi uje utueleze nikuombe sana kama unataka kurekebisha jambo tulirekebishe moja kwa moja kwa sababu leo hii tumepoteza wateja wengi sana. Wateja wengi wamekimbilia Msumbiji kule Beira, wengine wamekimbilia nchi nyingine. Sasa tunapoanza utaratibu wa kutaka kuwarudisha wateja hawa basi tuhakikishe tunawawekea masuala yote ya msingi vizuri. Mfano, *VAT* tuiondoe, iwekeni mwezi mmoja, nafikiri kabisa hawa watu watarudi na biashara itaweza kuongoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kutoa *road license,* kusamehe hii tozo ya *road license,* lakini tumechukua shilingi 40 tumeipeleka kwenye mafuta, naunga mkono hoja ya kuweka shilingi 40 katika kila lita, lengo letu ni maendeleo. Lakini toka uhuru tunalia suala la maji, ni wimbo wa Taifa kila siku maji, maji, maji. Kwa nini sasa shilingi 40 hizi tusizichukue tukaziwekea mfuko maalum wa maji vijijini. Tuitengee kabisa, tuiwekee kabisa *ring fence* pale kwamba hili hizi pesa tunazozipata ziende kwenye maji vijijini.

Mheshimiwa Waziri, kero ya maji bado ni kubwa na magonjwa yanayosababishwa na maji bado ni makubwa. Niombe sana suala hili tuliweke kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine siungi mkono kwa baadhi ya Wabunge wanaosema tuongeze shilingi 50 kwenye mafuta. Unajua ni rahisi kusema tuongeze na ninavyoona sasa itakuwa kila kitu unaongeza kwenye mafuta, tutafute vyanzo vingine ili tuweze kupata fedha za kuweza kutimiza bajeti yetu. Naunga mkono shilingi 40 lakini siungi mkono shilingi 50 kuongezwa kwenye mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yalikuwa mengi sana ambayo nilitaka kuongelea ni jambo hilo. Lakini la tatu nataka kuongelea uwanja wa ndege wa Sumbawanga. Kwenye bajeti ya mwaka jana tulipitisha bajeti ya uwanja wa ndege ujengwe wa kiwango cha lami, tumekuwa tukipigania sana. Lakini kubwa ambalo ninaliona sasa hivi ambalo nalipigania ni kwamba wale watu ambao wanatakiwa walipe fidia ambao wanazunguka uwanja wa ndege gharama za ujenzi zimezidi, ninaomba wafikiriwe upya ili waweze kufanyiwa uhakiki kwa gharama ya sasa. Na niipongeze kabisa bajeti yako, lakini nimpongeze kabisa kwa kujenga uwanja wa ndege sio uwanja wa ndege peke yake Sumbawanga lakini viwanja vingine vyote ambavyo vinajengwa kwa sababu ninaamini kila kwenye uwanja wa ndege maendeleo yatakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kuliongelea, nataka niulize tu hivi shisha Mheshimiwa Waziri wa Fedha uko hapa na Waziri wa Mambo ya Ndani yuko hapa. Shisha hii ni haramu? Shisha hii ni madawa ya kulevya? Na kama ni madawa ya kulevya kwanini *TRA* mnakusanya kodi? Kwa nini ile tumbaku inapofika bandarini mnai-*charge* kodi? Na kama ni madawa ya kulevya, Waziri Ummy yuko hapa naye atujibu na kama ni madawa ya kulevya au shisha inatumika vibaya, hata sigara inatumika vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sigara watu wanaweka bangi mule, sigara unaweza ukaweka kitu chochote kile. Ni kazi ya polisi kuhakikisha ile shisha haitumiki vibaya lakini sasa leo tunaipiga marufuku, anatoka mtu tu huko sijui kagombana na mke wake au na mpenzi wake anakuja kusema shisha marufuku na hiyo marufuku ya shisha iko Dar

es Salaam peke yake! Ukienda Arusha wanavuta shisha ukienda Dodoma hapa wanavuta shisha, ukienda sehemu nyingine wanavuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niombe Mheshimiwa Waziri kama shisha hii ni madawa ya kulevya tuipige marufuku leo na kwenye kodi tuiondoke maana kwenye kodi imo, ukiwauliza wale jamaa wa *TFDA* wanasema haina madhara. Ukimuuliza yule Mkemia Mkuu anakwambia haina madhara, lakini ukija huku wanakuambia hii inatumika na madawa ya kulevya. Ni wajibu wa polisi, ni wajibu wa kila raia akiona kama kuna mtu anatumia madawa yale au anatumia shisha vibaya akamatwe. Lakini ukienda nchi za kiarabu wanavuta, ukienda Uingereza wanavuta, ukienda dunia nzima kasoro Dar es Salaam. Nataka niseme, liangalieni tusiwaumize wananchi, wako watu wanalipia kodi Dar es Salaam lakini ikitoka inapigwa marufuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuongelea jambo la mwisho, ni suala la Bodi ya *SELF*. Bodi hii mwaka jana iliahidi kutoa mikopo ya shilingi bilioni 12 lakini hatimaye mwaka jana walitoa shilingi bilioni tisa. Mwaka huu walipanga shilingi bilioni saba kuweza kuwakopesha wafanyabiashara/taasisi kubwa. Lakini kwenye bajeti hii tumepanga shilingi bilioni 20 mwakani lakini bodi hii imevunjwa, haipo. Sasa hizi fedha zote tunazozipanga jamani tunangoja nini? Bodi hii imevunjwa leo ina mwaka mzima. Hebu jaribu kuangalia kama kuna jambo ambalo lingetakiwa kufanyika kwa haraka, lifanyike kwa haraka. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako. Mheshimiwa Kanyasu, ajiandae Mheshimiwa Chikota.

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. CONSTATINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba pia nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na kuweza kupata nafasi ya kuchangia kwenye bajeti hii ya mwaka 2017/ 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo wazungumzaji wengine waliotangulia wamesema, mimi ni miongoni mwa Wabunge ambao tunatoka kwenye maeneo ambayo uchimbaji wa dhahabu ni kazi kubwa kabisa ya maisha ya kwetu ya kila siku. Kwa hiyo, juhudi za Mheshimiwa Rais za kupambana na namna ambavyo madini haya yatakuwa na manufaa kwa wananchi sisi wananchi wa Jimbo la Geita Mjini na Mkoa mzima wa Geita tunazipa kipaumbele kikubwa na tunaziunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuishauri Wizara ya Fedha namna ambavyo inapoteza fedha nyingi kutokana na mikataba mibovu ambayo ilikuwepo. Nilipata nafasi ya kuchangia mwaka jana na sikuona mabadiliko yoyote yale wala hatua zilizochukuliwa. Kampuni nyingi zinazofanya kazi na migodi mikubwa ni kampuni za nje na migodi hii mikubwa imepewa uwezo inapotaka vipuli au bidhaa zozote inaweza kumpa yeyote aliyeko ndani au nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kampuni hizi zinazopewa kazi nyingi hazina ofisi Tanzania. Wanapokuletea orodha ya kampuni ili uweze kwenda kudai *service levy* wanakupa orodha ya kampuni ambayo ipo Canada, Australia, South Africa ambao hawana ofisi hapa, hawana *license* hapa wala hawana wafanyakazi. Lakini gharama ya manunuzi yao yameingizwa kwenye *corporate tax,* kwa hiyo, yanapunguza sehemu ya faida ambayo Serikali ingeweza kulipwa na ndiyo maana migodi mingi haiwezi kulipa kodi kwa sababu wanaweza ku-*deal* na kampuni iliyoko Canada ambayo ninyi Serikali hamna kumbukumbu nayo, haina ofisi, haina *address,* matokeo yake ni kwamba sisi tunapoteza pesa nyingi kwa sababu hatuwezi kwenda kudai *service levy.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka kumkumbusha Mheshimiwa Waziri, niliseme hili mwaka jana na miongoni mwa makampuni haya ni makampuni ya bima. Kampuni hizi za bima zime-*insure* wanafanyakazi lakini wana-*insure strong room, processing,* mgodi mzima. Kampuni hizi kubwa za bima unapoomba ile orodha ya makampuni ya *service levy* hawakuletei kwa sababu hazipo Tanzania. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri, hii ni sehemu kubwa ambayo tunapoteza pesa nyingi sana. Kama kampuni hii itakuwa ipo Dar es Salaam au ipo Mwanza watakuwa na ofisi, watalipa *working permit,* watalipia wafanyakazi wao na matokeo yake Serikali itapata fedha na itapata kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Halmashauri tunataka tupate hii *service levy* kama Serikali wanaona hii pesa ni ndogo hawana sababu ya kuyafanya makampuni yaje Tanzania, wayaache yakae nje. Sisi tunaomba watusaidie wawalazimishe sheria watu hawa wafungue ofisi Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, mwaka jana nilishauri hapa nikasema tatizo kubwa tunakwenda kwenye viwanda lakini ili viwanda viweze kufanya kazi lazima kilimo kwanza kipewe kipaumbele. Watu wengi wamezungumza kuhusu kilimo. Tatizo ninaloliona kwenye kilimo tangu tumeanza kuzungumza unaona *transformation* inayotupeleka kwenye kilimo ambacho kitalipa inakwenda kwa kasi ndogo sana. Mtu anayehamasisha viwanda ana kasi kubwa. Viwanda vinahamasishwa kwa kasi kubwa, *raw material* ni *products* za kilimo, lakini *transformation* ya kufanya kilimo kiweze kusaidia viwanda inakwenda kwa kasi ndogo ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu mfano, sisi Geita tunalima mananasi, mbegu ya nanasi ambayo ingeweza ku-*supply* au kuuzwa nje kwa sababu tunaambiwa mananasi tuliyonayo yanafanana sana na madawa ya kienyeji wala huwezi kuuza nje. Ili tuweze kupata *product* ya nanasi ambayo inaweza kuuzwa nje nilidhani kwa sababu nchi inajua tunalima nanasi, tayari wangekuwa wamepeleka wataalam wakatupa mbegu za kisasa zile mbegu ambazo

tunaweza tukauza yale mananasi nje, tukawa na soko ambalo lingeweza kuwabadilisha wakulima wa mananasi katika Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu tumeanza kuzungumza kuhusu kilimo, wakulima wa mpunga wanalima kienyeji vilevile walivyolima miaka kumi iliyopita. Tunafikiria kuongeza ukubwa wa mashamba, sio ukubwa wa uzalishaji. Kwahiyo, matokeo yake, mbegu za mpunga zile zile ambazo tulilima miaka kumi iliyopita ndizo tunazozungumzia kuendelea kulima kwenye mfumo wa viwanda. Kwa hiyo, haiwezekani viwanda tunavyovizungumza vikaja viwaka *productive* kama hatuwezi kufikiria kubadilisha kabisa namna ambavyo tunalima. Ukienda kwa wakulima wetu wengine wanalima ukubwa wa shamba. Anaweza kulima ekari kumi akapata gunia tano za mahindi, lakini kumbe angeweza kulima heka mbili akapata gunia 60 za mahindi na eneo lingine akalima kitu kingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mabadiliko tunayotaka kwenye kilimo lazima yaendane na *speed* ya ujenzi wa viwanda tunavyovifikiria vinginevyo tunakwenda mahali tutajenga viwanda, halafu tutaagiza *raw material* kutoka nje. Alisimama hapa Waziri wa Kilimo akasema hata Bakhresa maziwa anayopaki kwenye pakiti mengine ni ya unga kwa sababu maziwa hakuna. Lakini leo utaona vita ya Serikali na mifugo, vita ya Serikali ya wafugaji ni kuhakikisha wale wafugaji wanafilisika badala ya kuwasaidia wale wafugaji waweze kutengeneza uzalishaji mkubwa wa maziwa ili Bakhresa apate maziwa. Bila kufanya hivyo, hata viwanda tunavyovihamasisha vije vitakuja vifungwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la pili nilitaka kuona mchango wa Idara ya Uvuvi kwenye uchumi wa Tanzania. Ziwa Victoria miaka kama 15 ya nyuma tulikuwa tunapata pesa nyingi sana za kigeni kutokana na uvuvi, taratibu taratibu *productivity* imeendelea kushuka sasa tunabuni mikakati mbalimbali kwa ajili ya kuwalinda wale samaki. Lakini tatizo kubwa lililoko Ziwa Victoria, lile ni ziwa, uvuvi ni mkubwa hakuna juhudi za ziada za Serikali za kuhakikisha

kwamba tunapandikiza vifaranga vya kutosha kwenye Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu mfano, kuna maeneo mengi sana yemetengwa kwa ajili ya samaki kuzaliana na yale maeneo yaliyotengwa, Serikali ingeweza kuwa na mkakati kabambe wa kuingiza vifaranga hata milioni 100 kila mwaka vifaranga wa sangara unawaweka katika Ziwa Victoria, wakisaidiana na wale ambao wanazaliana kwa mfumo wa kawaida, samaki hawawezi kuisha katika Ziwa Victoria. Tatizo letu tunavuna tu, tunavuna tu matokeo yake badala ya kugundua kwa nini samaki wanapungua tunaweka masharti ya kuwaambia wavuvi wapunguze *size* ya nyavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema hapa wakati nachangia kwenye Wizara ile na bahati nzuri Waziri hakutaka kulijibu. Amefanya operesheni ya kukamata wavuvi wanaovua samaki kwa nyavu ambazo zina macho zaidi ya 26 lakini hiyo nyavu ambayo inatumika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Chikota, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Kikwembe, ajiandae Mheshimiwa Omary Badwel.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niungane na Waheshimiwa Wabunge ambao wametangulia kusema kuunga mkono na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua anazochukua katika ulinzi wa rasilimali zetu. Kazi anayoifanya ni kubwa, kazi hii inahitaji uthubutu mkubwa na kazi hii ni ya kizalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachotakiwa kukifanya wote kwa umoja wetu tunaomba tumuunge mkono Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili kama anvyoomba yeye mwenyewe, tuendelee kumuombea katika sala zetu ili aweze kuendelea kutekeleza majukumu yake na hatimaye ahamie kwenye sekta ndogo zingine hata sekta za gesi, utalii na maeneo mengine ambapo kunahitaji usimamizi madhubuti ili kuweza kuleta tija katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili niungane na wenzangu kumpongeza Waziri kwa kazi nzuri aliyoifanya, Mheshimiwa Dkt. Mpango na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji na wataalam wa Wizara hii wakiongozwa na Ndugu Dotto na Gavana wa Benki Kuu Profesa Ndullu. Tunaona kabisa waziwazi kwamba utaalam wao na weledi wao unasaidia sasa kuja na sera za kifedha ambazo zinasaidia katika uchumi wa nchi yetu. Kama takwimu zinavyoonesha kwamba uchumi wa nchi yetu unaendelea kupanda na kuimarika kwa asilimia saba kila mwaka, kwa hiyo tunakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa mfumuko wa bei tumeona kwamba muda mrefu mfumuko wa bei bado uko kwenye *digit* moja. Siyo hivyo tu, pamoja na takwimu zinazotolewa kwamba kuna biashara zinaendelea kufungwa lakini kwenye kitabu cha Waziri hapa imeonesha wazi kwamba kuna biashara mpya zaidi ya laki 224,000 zimefunguliwa. Vilevile kitabu kimeonesha takwimu kwamba sasa pato la kila Mtanzania yaani *per capita income* imeongezeka kutoka milioni 1.9 mpaka milioni 2.1. Kwa kweli wanastahili hongera, bila usimamizi wa Waziri na watendaji wakuu haya yote yasingetokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nikupongeze vilevile kwa kuja na kitabu chako ambacho kimejibu hoja nyingi za wananchi na za Wabunge. Utakumbuka mwaka jana hapa uliambiwa kwamba wewe huna jimbo na una mpiga kura mmoja, lakini maneno hayo mwaka huu yote tumeyafuta, kwa hiyo, tunakupongeza sana kwa usikivu wako na kwa kweli Wabunge tunakupongeza kwa sababu mimi kila nikiangalia ukurasa, naona unajibu hoja ya Mbunge au unajibu kero za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo naomba nitoe mchango wangu kuhusu mambo matatu, suala la kwanza ni hii ukurasa wa 48 umezungumzia hatua za mapato na hapa umezungumzia kuwatambua rasmi wafanyabiashi wadogo wadogo wasio rasmi na wanaofanya biashara katika maeneo yasiyo rasmi, mama lishe, wauza mitumba, wauza mazao ya kilimo wadogo wadogo, mboga mboga na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni kitendo kibubwa sana kwa sababu mara nyingi kundi hili lilionekana kwamba halina msaada na halina nafasi katika uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, tendo la kuwatambua na kuwasajili hii inaonekana wazi kwamba hawa sasa ni wadau wa maendeleo ya nchi yetu. Nishauri sasa kwamba kinachotakiwa kufanya sasa hivi ni kwamba Mamlaka ya Serikali za Mitaa basi zishirikiane na watu hawa yaani mipango ya kuwatambua na kuwatafutia maeneo iwe shirikishi tusiwe na ule utaribu kila siku tunawafukuza watambuliwe, wawekwe kwenye maeneo rasmi na tusahau ile miradi ya zamani, nafikiri wote tuna historia ya mradi ule wa *Machinga Complex* na lile soko la Mchikichini nini kinaendelea ni kwa sababu hatukuwashirikisha. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa tendo hili ambalo sasa hivi tunaenda kuwatambua tuwasajili hii itasaidia sasa kuwapa maeneo ambayo yatakuwa karibu na wateja wao na maeneo yao ya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa pili sehemu ya pili ni ile suala kupunguza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vyakula vya mifugo, lakini vilevile ni kupunguza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mayai ya kutotoa vifaranga hii itaongeza ajira kwa vijana wetu, kwasababu kuna vikundi vingi vya kinamama na vijana wanashughulika na ufugaji kwahiyo tukifanya hivi tutaongeza ajira kwa vijana wetu. Tunachotakiwa kutoa ushauri kwa mambo mawili kwamba tupunguze kodi ya madawa ya mifugo, lakini pili vikundi hivi vya vijana na kinamama sasa iweze kupewa mkopo ili waweze kufuga vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu naenda kwenye sekta ya kilimo. Sekta ya kilimo nako kuna unafuu umepatikana kwa kupunza tozo mbalimbali kwa wakulima. Lakini kwa kipekee niishukuru Serikali kwa uamauzi wao kwa kuamua kugawa pembejeo za kilimo bure kwa wakulima wa korosho nawapongeza sana, lakini kwenye korosho bado tunatakiwa twende mbele zaidi tujikite katika ubanguaji wa korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakosa fedha nyingi sana tuna viwanda vya kubangua korosho 12; lakini kwenye mpango wetu tunazungumzia viwanda viwili tu. Kuna viwanda vingine kumi hebu tuviwekee mkakati ili tupate fedha nyingi lakini vilevile tutaongeza ajira kwa wananchi wetu, na wenzetu wa Msumbiji wana-*practice policy*, korosho nyingi za Msumbiji zinabanguliwa kwa nini sisi Tanzania tusibangue, kwa hiyo naomba sasa tujikite katika ubanguaji wa korosho ili tuache kuuza korosho ghafi nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine ni utekelezaji wa miradi. Inaonekana miradi yetu inachukua muda mrefu sana kwenye utekelezaji kuna mradi huu wa miradi 17 ambayo inagusa Muheza, mradi wa Makonde, kuna mradi wa Njombe, miradi hii inatakiwa kuanza kutekeleza...*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, ahsante Mheshimiwa Dkt. Kikwembe.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ajiandae Mheshimiwa Badwel.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi niweze kutoa

maoni yangu kuhusiana na hotuba ya Mheshimiwa ambayo imeletwa kwa ajili ya mapendekezo ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nitoe pole kwa ndugu zetu walemavu waliopata *rapture* pale Dar es Salaam, ni sawa inawezekana ni katika kutekeleza sheria, lakini ni vema sasa hata utekelezaji wa hizi sheria tukaangalia ni namna gani, nimuombe Mheshimiwa, ndugu yangu, dada yangu Mheshimiwa Jenista, dada ambaye unasikiliza na unasimamia masuala haya hasa mambo ya Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu nina kuamini utalishughulikia suala hili kwa kushirikiana na mamlaka husika ili tuweze kuona ni namna gani wale walemavu wameweza kutendewa ndivyo sivyo, kwa kweli si jambo jema kwa kupiga walemavu hata kama tunatekeleza sheria. *(Makofi)*

Kwa hiyo nikuombe ndugu yangu kwa umahiri wako dada yangu Jenista ulionao ninaamini suala hili utalishughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia vilevile masuala yaliyotokea Tabora kwenye michezo tunasema michezo inadumisha amani, upendo, utulivu. Wamecheza kule pamoja na Jeshi la Wananchi sasa sielewi matokeo yalikuwaje, matokeo yake *MP's* wakaingia uwanjani na kuanza kupiga wachezaji na wananchi, hilo nalo naomba Waziri anayehusika alishughulikie hili tujue sasa nini maana ya michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo naomba nipongeze sasa bajeti hii iliyoko hapa mbele yetu inayopendekezwa. Bajeti hii kwa kweli imeweza kulenga maeneo mbalimbali na lengo lake kubwa tunaona ilikuwa ni kupunguza kodi ili kuweza kuwasaidia wananchi kufikia uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii imeweza kutoa misamaha mingi ya kodi ambazo nyingi zilikuwa ni kama kero kwa wananchi, kwa mfano naweza kusema katika jimbo langu la Kavuu kata ya Majimoto na kata ya Usevya

wamekuwa wakilalamikia sana kodi ya majengo, kodi ya *guest house*, kwa kweli kuwaondolea kule kutawawezesha na wao angalau kusonga mbele, kwa sababu kule sisi tunategemea siku za mnada tu, kwa hiyo hata tulivyokuwa tukitoa zile kodi kwa kweli ilikuwa inawaumiza wananchi na wako huko najua wananisikia, mitandao iko mingi tu wananisikia wanajua nawakilisha mawazo yao hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lakini naomba niende katika suala zima ambalo limekuwa likiongelewa la shilingi 40. Katika hii shilingi 40 tunaelewa lengo ni jema na ni zuri kwa Serikali, lakini ukiangalia kwa ndani hii pesa imeongezwa kwenye mafuta, bidhaa za mafuta ikiwemo na mafuta ya taa. Bidhaa hizi za mafuta ya taa na wananchi wetu vijijini hasa katika jimbo langu ambalo halina umeme, wanatumia mafuta ya taa kwa maana kwamba watachangia hii shilingi 40, sasa kwa msingi huo huo wa wao kuchangia hii shilingi 40 nimuombe Mheshimiwa Waziri usiwe na kigugumizi kwa kuitoa hii shilingi 40 katika ku-*cover* deni la Serikali la shilingi milioni 28 hii shilingi 40 ipeleke kwenye maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lazima iende kwenye maji, usiwe na kigugumizi Mheshimiwa Waziri katika hili kwa kweli ukifanya hivyo ndipo utakapokuwa bajeti yako sasa umeinogesha ipasavyo, pale tutakapoweza kuiweka hii pesa kwenye maji kwa sababu lengo lako ni kukusanya hii shilingi milioni 28 ili iende ika-*cover* lile deni lenu Hazina, sawa hatukatai ni pesa ya maendeleo, sasa tutakaposema kwamba ile shilingi 40 isiende kwenye maji vyanzo wewe vya kupata hii milioni 28; unayo shilingi bilioni 28 unavyo vyanzo? Itafute kwenye vyanzo vingine na hii shilingi 40 uliyoongeza kwenye bidhaa za mafuta ambazo wote itatugusa mpaka wananchi wa kijijini iende kwenye maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine namba niongee kuhusu ahadi ya shilingi milioni 50, katika hotuba ya Kambi ya Upinzani ukurasa sita wameongelea ahadi ya milioni 50. Ahadi hii ni ahadi ya Chama cha Mapinduzi, tumuache Mheshimiwa aliyepita kila kijiji kuomba kura na kuitoa ahadi hii haitekeleze, tukianza kudandia gari kwa mbele, tutapata

kugongwa. Muachieni Mheshimiwa aitekeleze ahadi yake, maana yake imeshakuwa ni nini tumeshapewa maelekezo hapa na Serikali namna gani pesa hii itatoka lakini nashangaa kwenye ukurasa wa sita ndio ajenda kuu ya bajeti ya ndugu zangu pale, tuachieni tuka-*organize* wananchi wajiunge waweze kupata pesa hizi kwa utaratibu maalum na msiseme ni ajenda yenu, maana kazi yenu kudandia mbele magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kodi ya majengo tumesema itaanza kwa shilingi 10,000 nyumba za kawaida na shilingi 50,000 kwa ghorofa, nikuombe Mheshimiwa Waziri katika hili utunyumbulishie ni nyumba gani italipa shilingi 10,000 ni ghorofa gani italipa shilingi 50,000. Maana ukiniambia nyumba kwangu jamani nina tembe, sasa yule mwenye tembe kadi ya bima tu ile ya *CHF* hana, leo ukamwambie atoe shilingi 10,000 inawezekana? Sasa utuambie ni nyumba ya aina gani itakayoanzia shilingi 10,000 na ni nyumba gani itakayoanzia shilingi 50,000 . *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake huwezi kuniambia ghorofa kama lile *LAPF* pale ama *Kilimanjaro Hotel* itafanana na nyumba ya kuishi ya mtu mwenye ghorofa moja ama huwezi kuniambia nyumba ya vyumba viwili vya kulala hapo ukifika Mwitikila hapo itafanana na nyumba ya vyumba vitano *self* ya kulala.

Kwa hiyo, naomba mtuambie vigezo. Maana utakapoweka hivi wale ndugu zangu watoza ushuru na watoza kodi wao wataenda kutoza kama lilivyo hawataweza kusema huyu anafaa, huyu hafai, wao wataenda kutoza kama mlivyolielekeza na wengine wanaweza kusema kwamba sasa nyumba yangu ghorofa saba silipi, tumeambiwa ya ghorofa ni shilingi shilingi 50,000. Sasa lazima mueleze hapo kwamba ni nini mnakusudia katika kupata haya majengo na haya majengo yako kivipi? Huwezi ukaenda mtu mwenye nyumba sita ukamwambia akalipa shilingi 10,000 sawa na yule mwenye nyumba ya chumba kimoja ambacho labda ni chumba, sebule na choo haiwezekani...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Ahsante kwa mchango wako mzuri.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja na ninaungana na Waheshimiwa wote na wananchi wote wa Tanzania kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Badwel, ajiandae Mheshimiwa Jesca David Kishoa na Maulid Mtulia.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa kunipa nafasi na niweze kuchangia bajeti hii ya Serikali kwa mwaka unaokuja wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niungane na waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akiifanya toka amechaguliwa mwaka 2015 na sisi Wabunge tunamuunga mkono na tunaahidi kwamba tutaendelea kumuunga mkono ndani ya majimbo yetu lakini pia kama viongozi wa kitaifa ndani ya nchi yetu yote ndani ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali pia kwa ujumla kwa masuala ya umeme ambayo sasa inaonekana *REA III* inakwenda vizuri na mimi Mbunge wa Bahi nilikuwa nikilalamika hapa kila wakati juu ya kukosa umeme, lakini naona mambo yangu safari hii shwari, kwa hiyo nashukuru sana Serikali kwa kuitambua na kuona Wilaya ya Bahi nayo inaweza kupata umeme tena kwa maana ya vijiji vyote Wilaya nzima, ahsante sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa kupunguza kodi mbalimbali na hususan zile ambazo zinawalenga wananchi wa chini ambao wamekuwa wakifanyia biashara mbalimbali hususani mazao, tunaipongeza sana Serikali na

hivi karibuni niliuliza swali pamoja na mazao mengine lakini pia nilizungumzia sana habari ya ubuyu na ukwaju, nilikuwa naomba pia Serikali itoe ufafanuzi sasa kwa sababu haya yanaonekana kama mazao ya misitu hivi huwenda yasiwe yanajumuishwa katika hili zoezi la upunguzaji wa ushuru mpaka tani moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi Bahi kule ukwaju na ubuyu ni sehemu ya mazao muhimu kwa wafanyabiashara wadogo wadogo kina mama na vijana ambao wamekuwa wakitafuta maisha. Kwa hiyo, ni vizuri ubuyu na ukwaju ukatangazwa hapa rasmi kwamba nao utaanzia tani moja kutozwa ushuru ili wale wananchi wenzetu wanaofanya kazi hii Bahi na ukizingatia Bahi ni Wilaya ya ukame ina vitu vichache sana hivyo ambavyo wananchi wanaweza kuvitumia kwa ajili ya maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze Serikali kwa kuondoa hii tozo ya kodi ya magari kwa maana ya kodi za barabarani na kuamua kuipeleka kodi hiyo kwenye mafuta, uzuri wa jambo hili tu kwamba ingawa tutatozwa lakini *we don't feel* kwamba kuna kitu tunachangia tofauti na wakati ule ukiambiwa kwamba lipia shilingi 300,000/400,000 unaguswa kuzikusanya hizo fedha lakini sasa kwa mtindo huu tumekuwa tulikipa pole pole bila kufikiri kwamba unalipa na hiyo tunaendeleza kuchangia katika maendeleo ya nchi yetu na Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bahi ni eneo la ukamae na Wabunge wenzangu ni mashahidi safari hii ukitokea Morogoro tu ukifika pale Gairo ukianza tu, Mkoa wa Dodoma unaanza kukutana na ukame mkali, tofauti kabisa na wenzetu katika Wilaya zingine na mikoa mingine. Kwa hiyo, nilidhani kwamba kuna haja kubwa ya kuangalia Mkoa wa Dodoma huu katika suala la miundombinu ya umwagiliaji hususani Wilaya yangu ya Bahi. Wilaya ya Bahi ni ndiyo Wilaya kame zaidi kuliko zote katika Mkoa huu wa Dodoma, lakini Mungu ameijalia Wilaya Bahi ina ardhi kubwa ina mabonde mazuri, lakini tunakosa fursa ya miundombinu sahihi ya kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bahi tuna skimu za umwagiliaji kumi, kati ya skimu hizi kumi kama zimekuwa zimeendelezwa vizuri na zinafanya kazi vizuri zingechangia kwanza wananchi wenyewe kupata chakula cha kutosha katika eneo la Wilaya ya Bahi. Lakini pia kwakuwa hapa Dodoma sasa ni Makao Makuu na watu wengi wanahamia tungeweza pia kupata vyakula mbalimbali hapa jirani kuliko kutoa vyakula mbali kutokana na hali halisi ya ukame wa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwahiyo naiomba sana Serikali embu ipitie upya ile miradi kumi ya umwagiliaji iliyopo Bahi, maana mingine ama imechakaa na ni ya muda mrefu, lakini mingine ilijengwa ikaishia nusu haikukamilika, haifanyi kazi, mingine ilianza hata robo haijafika na fedha nyingi zimepotea na zile fedha hazifanyi kazi yoyote, nilikuwa naomba sana Wizara husika waje Bahi wapitie miradi yetu yote hii kumi waone namna ambavyo watawasaidia wananchi wa Bahi kuendeleza kilimo cha umwagiliaji ili hali ile ya sisi kuomba chakula kila mwaka ipungue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati huo huo na tathimini ifanyike ili wananchi wa Bahi waweze kupatiwa chakula hata kama ni cha bei nafuu kwa sababu hali kwa kweli ni mbaya sana sio sisi tu kama wananchi, lakini hata mifugo kwa sababu mvua haikunyesha vizuri pia hata hali yetu ya mifugo itakuwa ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika suala la viwanda Mheshimiwa Waziri sisi Bahi ndiyo Wilaya tunaongoza kwakuwa na ng'ombe nyingi katika mkoa huu wa Dodoma, lakini hatuna hata viwanda vidogo vidogo vya usindikaji wa nyama ambavyo vingesaidia sana wananchi wale mifugo yao ambayo wanaifuga ingeweza kuleta tija zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri huwa nakusihi hapa namna unavyo waahidi Wabunge viwanda na mimi Bahi nahitaji kiwanda cha usindikaji nyama, ninakuomba sana tushirikiane tuweze kupata kiwanda hicho ili wananchi waweze kukuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji, Bahi kama nilivyosema ni Wilaya kame na mji wa Bahi ule ulikuwa ni kijiji tume u-*promote* mpaka umekuwa mji kwa sababu ile ni Wilaya mpya lakini tumekuwa na shida ya muda mrefu sana ya maji katika mji wa Bahi. Nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri miradi ambayo tumeomba ya Bahi kwa miaka saba sasa wa maji pale Bahi mjini hatujapatiwa fedha, kwahiyo siku moja na sisi bajeti ioneshe kwamba Bahi mji ule unakwenda kupewa maji ya kutosha ili wananchi waweze kujenga kitu ambacho kimewashinda sasa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia miradi hii ya maji imekuwa na gharama kubwa mno, nataka niishauri Serikali inawezekana ninao ushahidi kwamba miradi hii ya maji imekuwa ikiongezewa fedha nyingi sana na wataalam wetu sio waaminifu, wamekuwa wakiongeza fedha hizi za miradi ya maji na inakuwa fedha nyingi kiasi kwamba tunashindwa kutekeleza miradi mingi katika vijiji vyetu na nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu iangaliwe kama tunauwezo leo wa kusema barabara ya kilometa moja inatengenezwa kwa bilioni 1.2, tunauweza kusema leo umeme ukisambazwa katika kijiji kilometa kumi utalipwa kiasi fulani, lakini pia tunaweza kufika mahali tukasema kwamba maji yakisambazwa katika kijiji kwa kilometa tatu au nne yatakuwa na gharama kiasi fulani hata kama mazingira yatakuwa tofauti kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa hali hii ambayo tunakwenda nayo siyo rahisi sana kutekeleza hii miradi ya maji, unaambiwa kila mradi ukigusa unaambiwa ule ili ukamilike unataka milioni 700; ili ukamilike unataka milioni 600, lakini wanakuwa watu binafsi wanachimba visima wanasambaza maji wanauza ukimuuliza umetumia milioni ngapi wanasema nimetumia milioni 30, lakini Serikali hakuna milioni 30 ni milioni 200; milioni 300; milioni 400 kitu ambacho kimekuwa ni kikwazo kikubwa. Nadhani kuna haja ya kuipia wataalam wetu hawa waelekezwe vizuri na kupitia kuona gharama za miradi ya maji zinakuwa kwenye *standard* kama miradi ya barabara. miradi ya umeme na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeiacha miradi ya maji wanabuni wenyewe tu kutokana na hali halisi kwahiyo katika ubunifu huo wako wataalamu ambao wamekuwa sio waaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Dodoma tunao punda, tulinde hawa punda kule vijijini wananchi wengi hawana uwezo wa kusafirisha mazao kwenye magari, pikipiki na na kadhalika wanatumia punda leo tukimaanisha kiwanda hapa kila siku punda wanakwenda na punda ndio wanyama nadhani hapa Dodoma wanaozaliana kwa uchache sana, lakini wanyama wenye msaada mkubwa sana, nadhani Serikali iangalie namna ya kuwalinda hawa punda kwa sababu la sivyo hawa punda watapotea latika Mkoa wa Dodoma, Mkoa wa Singida na maeneo ya hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli unafika pale mpaka punda wale unawaonea huruma, kwa sababu punda ni rafiki zetu wazuri, wamekuwa wakitusaidia miaka mingi kwenye mashamba yetu mizigo yetu mbalimbali, lakini leo tunaagalia na wengi tunapita hapo tunaona na nimesikia kile kiwanda kimefungwa sina hakika. Nilikuwa naomba jambo hili liwekewe mkazo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba punda wanalindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimalizie tu kwa kuunga mkono hoja hii, namtakia kila la heri Mheshimiwa Waziri hotuba yake hii ipite salama na baadaye kazi ya maendeleo iweze kuendelea kwenye nchi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante. Mheshimiwa Kishoa, ajiandae Mheshimiwa Maulid Mtulia.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nitaanza kwa kuzungumzia suala zima la ripoti ya madini kwa ufupi, ili kuweka rekodi sawa.

Suala la wizi kwenye sekta ya madini ni suala ambalo wapinzani kwa muda mrefu sana wamekuwa wakilizungumza na endapo kama tungesikilizwa leo hii tusingekuwa tunazungumzia wizi wa takribani miaka 19 iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano wa Bunge uliopita, niligusia pia suala hili kwa maana ya umuhimu wa kuweka mikataba wazi na pamoja na sababu nyingine nyingi nilizozitaja pia nilisema kuna umuhimu kwa sababu sisi ni *member* kwenye *organizations* ambazo zina-*deal* na masuala ya *Open Governance* mfano *EITI*, lakini pia na *OGP* yaani *Open Governance Partnership*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Rais ameagiza wale walio-*initiate* wizi huu kwenye makinikia wafikishwe kwenye vyombo vya sheria lakini pia wachukuliwe hatua, lipo jambo la msingi sana ambalo naomba nimshauri kwa upendo kabisa. *Experience is the best teacher.* Kwa sababu kuna uzoefu ambao umewahi kujitokeza mwaka 2012 ambapo kulikuwa kuna Balozi mmoja anaitwa Mahalu alipelekwa kizimbani kwa kosa la ufisadi wa bilioni 2.5 na alipofika kizimbani akajitetea kwa kusema kwamba yale yote ya ununuzi wa jengo lile ambalo alikuwa amelinunua yalikuwa ni maelekezo kutoka kwa mwajiri wake, na kesi ikawa imeishia hapo. Sasa huu ni uzoefu tu ambao umewahi kujitokeza. Napenda nimshauri Mheshimiwa Rais kwamba ili kuweza kuweka mbivu na mbichi hadharani ni bora atoe *immunity* kwa mapapa ili suala hili liweze kutendeka kwa haki, siyo kuonea vidagaa kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la *IPTL*. Pamoja na kuwepo na ufisadi mkubwa sana kwenye madini na gesi, lakini bado kuna ufisadi mwingine mkubwa kwenye umeme. Wabunge wa awamu iliyopita watakuwa mashahidi na watakuwa wana kumbukumbu nzuri kwamba miongoni mwa maazimio ambayo waliwahi kuyaweka wakiwa kwenye awamu ile ni pamoja na mtambo huu wa *IPTL* kutaifishwa. Nasikitika sana mpaka hivi sasa mtambo huu wa *IPTL* bado Serikali inapiga danadana kuutaifisha.

Mheshimiwa Mwneyekiti, nataka Serikali itoe majibu ni kwa nini mnapiga danadana katika hili wakati mna baraka zote kutoka kwa Bunge, wakati mna baraka zote kutoka kwa Mahakama ya Kimataifa ambayo imehukumu kesi na tunadaiwa takribani bilioni 400 na huu ni mzigo wanaenda kuulipa walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ni vema mkatambua kwamba Bunge ndiyo *Supreme organ of the State.* Pale Bunge linapofanya maamuzi au maazimio ni vema mkayatekeleza kwa sababu mnatengeneza mazingira ambayo tunashindwa kuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna swali la kujiuliza hapa, hivi mnashindwa kutaifisha mtambo wa *IPTL* kwa sababu gani? Je, ni kwa sababu huyu mmiliki wa *IPTL* singasinga anawachangia kwenye kampeni zenu au ni kwa sababu gani? Ni huyu Singasinga amewaweka mfukoni? Ni sababu ipi inasababisha mtambo huu wa *IPTL* ambao unatupa wakati mgumu wananchi wa Tanzania, walipa kodi wananyanyasika kwa ajili ya mtambo huu na Serikali mnaendelea kupiga danadana kwenye mtambo huu? Kuna kitu gani ambacho kimejificha?

Mheshimiwa Rais kama ameweza kuzuia makontena ya mchanga, siamini kama anaweza akashindwa kuzuia *IPTL* au kuifungia *IPTL,* labda kuwe kuna sababu ambayo imejificha. Ninaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha aseme sababu ni nini? Kwa nini *IPTL* mnashindwa kuifungia na wakati inatupa mzigo mkubwa sana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nigusie suala la benki ya *FBME*, nimeona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia ukurasa wa 15. Ni mambo ya aibu sana, nimeona sababu kubwa ya benki hii kufungwa ni uchunguzi uliofanyika kutoka Marekani. Karne hii unazungumzia uchunguzi kutoka Marekani toka mwaka 2012 benki hii imekuwa *reported* kwamba inatakatisha fedha, lakini mnakuja mnasubiri uchunguzi kutoka Marekani, *Financial Intelligence Unit* wako wapi? *PCCB* wako wapi?

Usalama wa Taifa na wengine mko humu ndani mko wapi? Kama mnashindwa ku-*deal* kwenye vitu *sensitive* kama hivi tunaachaje kuamini kwamba kazi yenu kubwa Usalama wa Taifa ni kuudhoofisha upinzani? Tunaachaje kuamini kama kazi kubwa ya Usalama wa Taifa ni kufanya mambo ya ajabu ajabu ambayo yanaendelea kwenye Taifa letu. Haya mambo ni ya aibu sana na si mazuri sana kuyazungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri kwa Serikali kuhusiana na suala hili, kama tatizo lipo kwenye hii kikundi cha *Financial Intelligence Unit* kuna mambo mawili ya kufanya, moja ni kukiondoa kikundi hiki na kukiweka kingine, kama hiyo haiwezekani basi muandae programu maalum kwa ajili ya kuwapa watu wetu hawa mafundisho waweze kuwa na uwezo mkubwa wa ku-*deal* na vitu kama hivi ambavyo ni muhimu sana. Ni aibu sana kwa Taifa letu leo hii tunakaa tunasubiri uchunguzi kutoka Marekani, karne hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na FBME, hivi mnasubiri nini kufungia Benki ya Stanbic? Nini kinawafanya mchelewe kuifungia Benki ya Stanbic au mnasubiri pia uchunguzi kutoka Marekani? Wakati *PCCB* wame-*prove* kwamba Benki ya Stanbic ilifanya miamala ambayo ni ovu, na wakati *CAG* ripoti yake ime-*prove* kwamba Stanbic ilifanya miamala ambayo ni haramu. Serikali inasubiri nini? Kwa nini msichukue hatua? Kwa nini mnakuwa mnategemea tafiti na uchunguzi kutoka sehemu nyingine? Kuna mambo ambayo kwa kweli hata ukiyazungumza yanatia aibu, ni vema tukajitathmini upya, tunakosea wapi? Tunakwama wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka sana nimalizie kwenye suala la kodi. Nimemsikia Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake kuna *page* fulani amezungumzia kuhusiana na *easy of doing business* kwamba Tanzania tumefanya vizuri sana, *your right,* uko sahihi, lakini unaangalia tumefanya vizuri ukilinganisha na akina nani? Ukiangalia kwenye nchi washindani mwekezaji anapokuja au mfanyabiashara kuna vitu anavizingatia anapokuja

kuwekeza. Tanzania ndio nchi inayofanya vibaya katika nchi za *East Africa* kwenye suala la *access of financing* na kwenye suala la *tax rates,* viwango vya kodi ni vikubwa. Haya ndiyo mambo ambayo mfanyabiashara Mwekezaji akija kuwekeza kwenye Taifa ni mambo makubwa anayoyazingatia na ndio mambo ambayo tunayafanya vibaya kuliko mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri pale mnapokuwa mnajidai na kujitutumua kwamba tumefanya vizuri, ukilinganisha na mataifa mengine, kwa kweli sisi siyo Taifa la kuendelea kujilinganisha na Mataifa kama ya Burundi, tunafanya vibaya kweli na nina taarifa hapa kutoka *PriceWaterHouseCoopers* ndio takwimu hizi zinaonyesha tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema sasa Serikali kupitia hotuba yake nzima na mambo ambayo imepanga ikajitathmini upya. Hivi ni vitu gani ambavyo nyie mnavipa kipaumbele? Ni vitu gani ambavyo hamvipi vipaumbele? Kile ambacho mnakihubiri kila siku, kile ambacho mnakisema kila siku, siyo kitu ambacho mnakipa kipaumbele. Ukiangalia kila siku mnahubiri uchumi wa viwanda lakini mnaelekea kwenye maeneo mengine ambayo hayana uhusiano wa moja kwa moja na uchumi wa viwanda ambao mnaouhubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo ni msingi na ni muhimu sana katika kwenye uchumi wa viwanda ni pamoja na umeme. Tuna megawati 1,051 ni aibu, tuna makaa ya mawe yamerundikana Liganga na Mchuchuma takribani milioni 480 lakini hakuna kinachofanyika hapa, mnahubiri viwanda, viwanda vinatoka wapi?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo yanasikitisha sana, naomba nimalize kwa kukushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtulia, ajiandae Mheshimiwa Stella Ikupa, atafuatiwa na Mheshimiwa Silafu Maufi.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kupata fursa hii adhimu kabisa kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mbunge wa Jimbo, vilevile Kiongozi wa Kitaifa nitagawa mchango wangu katika maeneo makubwa mawili. Eneo la kwanza nitazungumzia kama mwakilishi wa Jimbo langu, lakini naamini nikipata fursa nitazungumza mambo yote haya nitachangia kitaifa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiniuliza kuhusu bajeti naionaje? Nitakubaliana kabisa na wenzangu wengi kwamba bajeti ina sehemu imefanya vizuri na ina sehemu kwangu mimi imenikwaza. Sasa kwa sababu sehemu iliyofanya vizuri watu wameshazungumza na kuisifia, nitajikita zaidi katika sehemu ambazo zimenikwaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kifupi katika ile kuondoa kodi ya leseni ya barabara nimezungumza na wapiga kura wangu, watu wa bodaboda, *taxi drivers* kimsingi wanashukuru sana. Wanasema hii kodi imewasaidia sana na niliwahi kuwauliza mnasemaje kama Serikali ikiamua kuirudisha tena kule mnasemaje? Wengi hasa wa pikipiki wamesema bora hivi ilivyo sasa hivi, huu mtazamo wanauunga mkono sana. Kwa hiyo, hili nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, mimi kwa jimbo langu la mjini nina tatizo sana la umaskini na umaskini kwangu mimi ninaupima katika mzunguko wa pesa. Mheshimiwa Waziri mzunguko wa pesa katika Mji wa Dar es Salaam umeshuka sana. Nashukuru kwamba umefanya juhudi za kufuta kodi mbalimbali pale bandarini, ambayo naamini kwa namna moja ama nyingine itaweza kuchochea uchumi, lakini naomba uyaangalie haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa watu wa Dar es Salaam utatusaidia sana kama utaleta ajira mpya. Ninapozungumzia ajira mpya nakusudia kuna walimu wengi wamesoma,

wamemaliza *course* zao mbalimbali wanasubiri ajira. Kuna eneo la afya wanasubiri ajira, kuna wataalam wa kilimo, bila kusahau majeshi yetu yote vijana wanasubiri ajira na bahati mbaya sana hawa watu wanaotarajia kuajiriwa hawataki kukaa vijijini, wanakuja kukaa mjini. Kwa hiyo tuna kundi kubwa la watu liko pale Dar es Salaam linatumia lakini halizalishi.

Mheshimiwa Waziri utanisaidia sana kama ukioanisha na hili la kupandisha madaraja watumishi wetu, kutoa *increment* kwa watumishi wetu, bajeti haisemi. Nimewahi kuzungumza na walimu, wafanyakazi wa afya wanalalamika kwamba sasa hivi *increment* hakuna, sasa hivi watu hawapandishwi madaraja, kwa hiyo Mheshimiwa waziri hili utakuwa umenisaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Mheshimiwa Waziri utanisaidia sana kama benki zetu zikiwa na fedha. Mikopo kwenye benki zetu za baishara, watu wa Dar es Salaam wengi wao wanaishi kwa kufanya biashara na wanakopa katika benki hizi za kibiashara, benki hizi ndogondogo mitaji yao ni midogo. Natambua kwamba Serikali imekopesha mpaka bilioni 500 lakini tunapenda ingekuwa ni vizuri tukafika angalau trilioni moja.

Natambua Serikali tumeshusha riba kutoka asilimia 16 mpaka asilimia 10, lakini mimi natamani kwa nini tusishushe mpaka asilimia tano kwa sababu hii mikopo inayokopwa na mabenki, ni mikopo ambayo *risk* yake ni ndogo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kama atayafanya haya atakuwa amenisaidia kwa kiwango fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri atanisaidia sana mimi mtu wa Dar es Salaam kama atalipa madeni au madai. Bajeti inaonyesha mwaka jana baada ya kufanya uhakiki tulikuwa na madai yanayofika trilioni 1.9 na tukalipa bilioni 700 maana yake kuna pesa zimebaki kama trilioni 1.2. Mheshimiwa Waziri ukilipa hizi tena tumelipa deni la nje, takribani trilioni saba, sasa kama tunalipa deni la nje trilioni saba ni vizuri tukamaliza haya madai ya ndani kwa sababu haya madai ya

Wakandarasi, madai ya Wazabuni, madai ya Bohari Kuu ya Madawa, madai ya watumishi, madai ya huduma mbalimbali haya yataleta mzunguko pale Dar es Saalam na wananchi wetu wataanza kuona nafuu ile unayoikusudia kuipeleka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri ninasikitika sana, Dar es Salaam pale ninakabiliwa na hali ngumu, chakula kikipanda. Mwaka huu ndani ya kipindi kuanzia mwezi wa tatu mpaka tunakuja hapa mwezi wa sita iliwahi kufika kilo ya unga shilingi 2,400, na unga ndio chakula nafuu kwa watu wa Dar es Salaam, kwa sababu ugali hauchagui mboga. Sasa unapopanda unga maana yake mwananchi wa kawaida atapata hali ngumu, wamejitahidi kupunguza matumizi wameacha mambo yote yasiyokuwa ya lazima, lakini mtu hawezi kuacha kula. *(Makofi)*

Sasa Mheshimiwa Waziri utatusaidia sana ukiongeza hifadhi ya chakula na hasa mahindi ili inapofika kipindi kama hiki cha ukame hifadhi yetu ya chakula iwe inauzwa kwa bei nafuu kwa wafanyabiashara wetu ili bei ya vyakula isipande. Kwa sababu bei ya vyakula ikipanda kunasababisha hali ngumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wananchi hawa wanapokuwa na njaa, wakati mwingine hawaoni umuhimu wa *standard gauge*. Mheshimiwa Rais anaweza akafanya mambo makubwa ya kujenga reli hayo, makubwa ya umeme na kuleta ndege lakini hivi mwananchi mwenye njaa atathamini vipi haya? Na kwa kweli kama tunataka kuleta mtengamano, kama tunataka wananchi wa kawaida waone Rais anachapa kazi lazima tutatue suala la njaa na kutatua suala la njaa ni kushusha bei ya chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili ni kwa maana hiyo bei ya chakula lazima ishuke, lazima hifadhi yetu ya chakula itumike kama kiwango ambacho kitaenda ku-*regulate* pale ambapo mazao yanapokuwa hayapatikani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya Halmashauri, kwenye mapato ya Halmashauri mimi nasikitika sana, kwa kweli wachangiaji wengine wanachangia lakini wengine sio wahusika wa moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unajua sisi watu wa Dar es Salaam ni wahusika wa moja kwa moja. Katika *property tax,* Kinondoni mwaka uliopita tulikusanya shilingi bilioni 7.8, baada ya Serikali kutukusanyia mwaka huu wametupa shilingi bilioni moja. Kuna hela zinapotea hapa jamani, wengine tunaposema kwamba tunataka kusaidia nchi yetu, inakuwaje tunapoteza mapato kama haya kwa sababu tu ya kugombania nani akusanye? Kwa nini basi Waziri kama anaona inafaa lazima hizi peza wakusanye wao, kwa nini katika haya Majiji hasa Jiji la Dar es Salaam kwa nini Halmashauri zisiwe kama *agent,* kwamba wao ndio wakusanye halafu wakukabidhi wewe ufanye unavyotaka? Si lazima zile pesa zote shilingi bilioni 7.8 tutumie sisi Kinondoni lakini roho inauma kwamba mnatoka kwenye mapato ya kukusanya shilingi bilioni 7.8 mnarudi mnapewa bilioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaongeza kodi ya mabango ambayo nimemuuliza Mhasibu wangu ambaye nimempigia simu leo hii akaniambia ni shilingi bilioni tatu tumelenga. Sasa kwa kulenga shilingi bilioni tatu ninyi wenzetu mtaichukua mnaenda kuifanyia majaribio wakati hii kodi ya majengo hatujafika mbali, tunaongeza na kodi ya mabango tunaenda kupoteza shilingi bilioni tatu?

Mheshimiwa Waziri, fikiria kama vipi, Manispaa za Kinondoni kwa sababu nayo ni Serikali zikusaidie ili tusipoteze hizi fedha, kwa sababu tunaweza kupoteza fedha zaidi shilingi bilioni 30 kwa Dar es Salaam tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mabadiliko ya sheria, nimesoma hapa katika kitabu cha *Financial Bill* hapa kuna mabadiliko ya sheria yanakuja, Sheria Na. 290…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Stella Ikupa kama hayupo Mheshimiwa Mmasi utafidia nafasi yako ya juzi na akimaliza Mheshimiwa Mmasi atafuatia Mheshimiwa Silafu Maufi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kufidia muda wangu ambao nilipoteza kwa siku ya Ijumaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda leo niongee na wanawake wenzangu wa Bunge lako. Sisi Wabunge bila kujali itikadi zetu za vyama tunakutana kwenye jukwaa moja la Kibunge la Wanawake. Jukwaa hili linaitwa *TWPG* yaani *Tanzania Women Parliamentary Group.* Pia katika jukwaa hili tunakutana kwenye agenda moja kwa kawaida katika kila mwaka tunakuwa na ajenda kama wanawake. Nitawakumbusha wanawake wenzangu ambao mmefika hapa pengine naona wengi wetu sasa tunakata *network,* tumejitoa kwenye agenda hatujui hata tunachokifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015 tulikuwa na ajenda kama wanawake wa Tanzania iliyokuwa inasema *Orange the World* nadhani Mheshimiwa Susan unasikiliza. Siyo hivyo tu, tukasema kwamba agenda hii haijagusa *a real context* ya Tanzania, tukasema kwamba tubadilishe ajenda. *This year* ninapoongea kwamba mwaka huu unaoishia tarehe 30 Juni, sisi kama wanawake tumebeba ajenda moja inayosema rudisha rasilimali ya mwananchi kwa wananchi. Uhuru wa uchumi uwasaidie wanawake na wanaume walioko pembezoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokifanya leo Mheshimiwa Rais ninajiuliza ni nani aliyetutoa kwenye ajenda ya kurudisha rasilimali ya nchi hii kwa wananchi kama siyo sisi wenyewe tumefika mahali hatujielewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekuja hapa ndugu zangu, wameshindwa kukaa na kuangalia, katika nchi ya Tanzania tunazo changamoto nyingi, lakini leo tunakuja hapa tunatoa mustakabali mzima, tunachangia hotuba yetu hii

ya Wizara ya Fedha, wenzetu hawa wanakuja na ngonjera mia, 1000 ambazo zinatutoa kwenye ulingo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja niwaambie hawa ndugu zangu, hivi mnatambua kwamba, mpaka Machi 2017 tuna changamoto kubwa ya bajeti ndogo ya Fungu la Maendeleo kwenye Wizara ya Maji? Mnafahamu tuna asilimia 19.8 tu zilizokwenda? Mnafika hapa mnakuja kutuambia Mheshimiwa Rais ameita wezi Ikulu! Ngoja niwaulize ninyi wanawake, hivi najiuliza na mimi ndio na mimi nipo, najiuliza na mimi ni mwanamke ndio, kwa sababu wamesimama hapa watu wanakuja kusema kwamba Mheshimiwa Rais ameita wezi Ikulu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi *Canadian Embassy* kama Mheshimiwa Rais ataanza kualika watu Ikulu, *Canadian Embassy* watafanya kazi gani? Basi tufute hii *Embassy* ya Canada tuifute, lakini sio hivyo tu, ninaongea na sisi wanawake na mimi nipo katika hilo ninaloliongelea hapa, lakini kama sio hivyo mkaja mkatuambia kwamba tukaombe msamaha! Jamani ngoja niwaambieni, msamaha wa kweli ni msamaha ambao utaambatana na vitendo katika kupeleka tumaini la kweli kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais anachokifanya ni kupeleka tumaini la kweli kwa wananchi na kama msamaha ungekuwa ni jibu, leo mimi ninakaa pale Dar es Salaam niko Tegeta, ninatarajia ningemuona Mheshimiwa Halima yuko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuja hapa akatoa kauli nisameheeni, baada ya kuambiwa mpaka na maaskofu, kuambiwa na mapadri kaombe msamaha, akaja akaomba msamaha. Yuko wapi kama kauli ya msamaha ndio jibu? Sio jibu, ni dhamira ya dhati katika kupeleka tumaini la kweli kwa wananchi. Mheshimiwa Rais ana dhamira ya dhati katika kupeleka tumaini la kweli kwa wananchi. Tumpe nafasi, hii nafasi ni ya Chama cha Mapinduzi, hii Serikali ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi, tunaongozwa na *manifesto,* tupeni nafasi tufanye kazi katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya ninayoyaongea ninapenda tu niwaambie wanawake wenzangu, hebu tusimame katika nafasi zetu. Hebu tuache ngonjera nyingi humu ndani, hazina mantiki, hazitusaidii, tuna mengi. Ukienda kule Jimboni ukamwambie mwanamke nilienda kutafuta *gold* ni nani aliipiga au nilienda kutafuta, nilienda nikatetea ajenda hii ilikuwa ya UKAWA au ajenda hii ilikuwa ya CCM! Hivi kwa nini tuna haja gani sisi kutoka kwenye ajenda yetu kama wanawake? Tuna kauli moja tu, rudisha uchumi wa Tanzania ukamsaidie mwanamke aliyeko pembezoni, hii ndio ajenda yetu, hiki ndicho tulichotumwa tuje kufanya katika Bunge lako hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Mpango. Naomba niguse suala la kilimo. Ni kweli ninapenda sana niipongeze sana Wizara yako, Mheshimiwa Waziri kwamba kwa mara ya kwanza Serikali hii imejitahidi katika kumtua mkulima mizigo mizito aliyonayo. Nimeona kwamba kuna *produce cess ambazo* mmetoa *VAT* kwenye masuala ya kilimo cha biashara, lakini pia kilimo cha chakula. Sio hivyo tu, nimeona mmetoa msamaha wa kodi hata kwenye *capital goods* ili kuweza kuhamasisha na kuboresha viwanda vyetu nchini vinavyozalisha ngozi, mafuta na dawa za binadamu, hii ni hatua nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hivyo tu, mlitoa kodi 108 katika Bunge hili, kodi 108 kwa mwaka mmoja. Lakini sio kodi 108 za mazao, pia mliweza kutoa kodi kwenye tani moja ya vyakula zinazotozwa na Halmashauri za Wilaya. Siyo hivyo tu mmeleta *bulk procurement system* katika kupeleka pembejeo kwa wakulima wetu, hizi ni hatua nzuri sana. Lakini Mheshimiwa Waziri bado tuna changamoto kubwa, nimetafuta sana miundombinu ya maji ya umwagiliaji mmeiweka wapi? Nimeenda kwenye Wizara ya Maji sikuona, nimeenda kwenye Wizara ya Kilimo sikuona, fungu hili liko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tunayo changamoto wewe ni shahidi, kwenye hali ya uchumi wa

Tanzania mwaka 2015/2016 umeandika wewe mwenyewe kwa maandishi kwamba, bajeti ya Kilimo, Fungu la Maendeleo *Vote* 43 ilienda asilimia tatu tu, hii ni changamoto kwetu. Mheshimiwa Waziri siyo hivyo tu, kilimo kimechangia asilimia moja kwenye Pato la Taifa, hii ni changamoto ambayo hatuna majibu. Mheshimiwa Waziri ni lazima tuweze kufahamu ili tuweze kupata malighafi za kulisha viwanda vyetu ni lazima Tume ya Mipango ya Taifa isimame katika nafasi yake na iweze kutoa ushauri maridhawa katika kuongoza Taifa lako hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na masuala ya kilimo mimi ninafikiri nasi wanawake wenzetu tufahamu kwamba, ipo haja ya kusemea kwa sababu, mwanamke wa Taifa hili anazalisha kiwango cha ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWEYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri. Sasa Mheshimiwa Raza dakika tano na Mheshimiwa Maufi ajiandae.

**MHE. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii adhimu. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha hapa salama nikiwa mzima wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia hii bajeti ambayo iko mbele yetu, nimshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya. Katika kipindi kifupi sana ameweza kusimamia mambo ya barabara, mambo ya umeme, mambo ya reli, makusanyo mazuri vilevile katika ununuzi wa ndege. Kwa kweli, Mheshimiwa Rais anapaswa kupongezwa kwa kazi kubwa anayofanya na sisi tunamuombea aendelee na *speed* hiyo, sisi Wabunge tuko nyuma yake kwa nguvu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye bajeti hii Wizara ya Fedha kwanza nimpongeze ndugu yangu

Mheshimiwa Waziri Mpango na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji. Kwa kweli, bajeti ya safari hii ni nzuri, ni bajeti ya matumaini na mimi ni imani yangu kwamba bajeti hii kwa mwaka huu itaipa nafasi kubwa katika nchi yetu na kwa mwananchi wa kawaida, vilevile itampunguzia mzigo mkubwa sana. Nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa bajeti nzuri pamoja na msaidizi wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze hawa *TRA* kwa ukusanyaji wa mapato. *TRA* kwa kweli safari hii wamekuwa watu wastaarabu sana katika kuzungumza na wafanyabiashara tofauti na miaka ya nyuma, nina matumaini makubwa ikiwa *TRA* watakwenda hivi kukaa na wafanyabiashara tukafika mahali ikawa ni *win-win situation* basi, mapato ya nchi yataongezeka sana. Wasichukuliwe wafanyabiashara kama ni maadui katika nchi, lakini wafanyabisahara kwa kweli wana nafasi kubwa sana kuliingizia Taifa mapato. Kwa hiyo, niwapongeze sana wenzangu wa *TRA. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naunga mkono ongezeko la shilingi 40 kwenye mafuta. Hii itatusaidia sana katika kutatua matatizo yetu ya maji na umeme, lakini si vibaya Mheshimiwa Waziri ikiwa tutaongeza *airport tax* japo kwa dola tano kwa sababu, hizi dola tano hizi wasafiri wamekuwa wengi na itatuingizia Taifa pesa nyingi sana. *airport tax* ambayo haimuumizi mwananchi wa chini kwa sababu, wanaosafiri wote *Alhamdulillah* ni watu wanaojiweza ndio maana wanaruka. Kwa hiyo, mimi hilo nilikuwa nataka kuliongezea kwamba, kama kutaongezwa na *aiport tax* dola tano sio vibaya, kwa sababu nchi itapata pesa nyingi na tutapata kufanya mambo yetu mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu umenipa dakika tano ninakushukuru. Mimi naunga hoja ya bajeti hii asilimia mia moja. *Inshallah... (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Maufi.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote napenda kutoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa kunipatia afya na kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mnyimi wa fadhila kama nisipomshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri aliyoifanya katika kipindi hiki kifupi kwa wananchi wa Tanzania. Mwenyezi Mungu ampatie afya, ampatie nguvu na ampatie uwezo wa kuendelea kuifanya, ili adhma yake iweze kutimizika kwa wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii kwa mwaka huu kwa kweli imefanya kitu ambacho kimewagusa wananchi wa Tanzania na hususan wananchi na akinamama wa Mkoa wa Rukwa. Bajeti ni nzuri na bajeti hii tukiisimamia nina imani kabisa kwamba itatekelezeka kwa asilimia kubwa zaidi na hatimaye kuleta maendeleo kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala la maji. Maji imekuwa ni kizungumkuti, maji imekuwa ni suala tete kwa akina mama, ni suala tete kwa wananchi wa Tanzania. Mimi napenda kutoa ushauri kwa Wizara yangu ya Afya na Wizara yetu ya Fedha kwamba tunaomba hii shilingi 40 naomba tuongeze tena shilingi 10 iwe shilingi 50. Kwa sababu hii fedha inahitajika kurudisha deni la Serikali, inahitajika kuleta umeme na inahitajika kuleta maji.

Mheshimiwa Mwenyekii, tunasema kwamba tunatua ndoo ya akina mama kichwani, lakini ukiangalia karibia asilimia 60 vijijini na vitongoji hakuna maji safi na maji salama. Mfano Mkoa wa Rukwa, ningeomba Serikali iangalie umuhimu wa kuangalia kutoa maji katika *Lake Tanganyika. Lake Tanganyika* maji yako ni mazuri, lakini tatizo ni kwamba, hayajawekewa mradi wa kuyaleta kwa wananchi. Mwambao wote huko wa *Lake Tanganyika* kuanzia Kala mpaka Karema, (Katavi) hakuna maji salama na maji safi, lakini *Lake Tanganyika* iko pale! Tungeiomba Serikali ikaangalia mradi wa kutoa maji *Lake Tanganyika* kwenda

kwa wananchi wetu ili kinamama waweze kupumzika na suala la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema kwamba, tunatua ndoo ya mama, kama tunatua kweli ndoo ya mama, lakini mimi naona kuna wasiwasi wa kumpatia tena mzigo mwingine. Mzigo mwingine ni mkaa, nilizungumza katika mchango wangu wa msingi katika maliasili na utalii tukasema ya kwamba ni vema tukapewa semina Wabunge kuhusu mkaa endelevu ambao ni rafiki wa misitu, ili tukiuelewa ikawa ni faida kwa akinamama wasipate mzigo wa pili kabla ya kutuliwa ndoo ya maji kichwani. Kwa maana hiyo, tunaiomba Serikali tuongeze hiyo shilingi 10 iwe shilingi 50 ili iweze kutoa tatizo hili ambalo linakuja la pili kwa akinamama zetu kuwa mzigo wa pili ndani ya kichwa chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaloomba lingine ni kwamba, ni kuhusu suala zima la barabara. Mkoa wa Rukwa tumechelewa, Mkoa wa Rukwa tulisahaulika kuhusu barabara. Hadi hivi sasa bado hatujaungana na Katavi, bado hatujaungana na Kigoma, bado hatujaungana na Tabora. Ninaomba kwa sababu tunakubali kuunga Mikoa yetu na hizi fedha zinatoka katika Serikali yetu ya ndani, kwa hiyo, tunaomba fedha hizi zitoke katika ukamilifu wake ili tuweze kuunganika na Mikoa yetu ya jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mkoa wa Rukwa tunaungana na Kongo, tunaungana na Zambia, tunaomba Matai-Kasanga na Matai-Kasesya hizi barabara zikamilike. Kukamilika kwa barabara zitawasaidia akinamama kwenda kwenye masoko ya mazao yao hali kadhalika kwenda kupata huduma ya afya kwa sababu Mkoa wa Rukwa hatuna Wilaya hata moja yenye Hospitali ya Wilaya, zote tuna Hospitali Teule kwa maana ya Vituo vya Afya; kwa hiyo, akina mama wanatoka huko wanakuja Mkoani kuja kupata huduma ya afya, tunaomba hizi barabara, hizi fedha za ndani zitoke katika asilimia hata 75 angalau hizi barabara sasa ziweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninapenda kuzungumzia suala zima la elimu. Tunao watoto wetu walemavu, hawa watoto wetu walemavu wanahitaji kupata elimu, lakini vifaa vyao vya kufundishia ni vifaa vyenye gharama kubwa zaidi, Halmashauri hawawezi na hata wazazi kuchangia hawawezi. Lakini juzi nimesikia kwa Mheshimiwa Waziri akisema kwamba Waziri Mkuu amepokea vifaa vya elimu. Naomba hivyo vifaa vya elimu ya kufundishia viweze kupelekwa shule ya Malangali ya Watoto Viziwi, Vipofu pamoja na Albino hali kadhalika shule ya Mwenge ambako kuna watoto wenye mtindio wa ubongo waweze kupelekewa vifaa hivyo, waweze kupata elimu nao waweze kujiunga na sisi katika maendeleo ya jamii ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala la shilingi milioni 50. Shilingi milioni 50 tumeizungumza na inawezekana kutekelezeka. Kutokana na kasi ya Rais wetu kuhakikisha kwamba, rasilimali ya nchi hii tunaitumia Watanzania, nina imani kabisa kwamba, hizi shilingi milioni 50 za kila kijiji zitapatikana kutokana na jitihada iliyopo katika Serikali yetu.

Kwa hiyo, ninaomba Serikali iweke tu utaratibu wa namna ya kuzisimamia na namna ya kuzifikisha kwa walengwa na wale wanaohusika ili ziweze kufanya kazi ya maendeleo. Nina imani kabisa kwamba jitihada ya Rais wetu Magufuli atasimamia ahadi zake kwa sababu hili alikuwa akilizungumzia sio kwa kuombea kura, alikuwa analizungumzia kwa kutaka kuhakikisha kwamba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mgimwa dakika tano.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Kaka yangu Waziri wa Fedha pamoja na Naibu wake. Lakini kwa namna ya kipekee naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Jemedari wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nijielekeze kwenye vipaumbele viwili. Kwanza Mchuchuma na Liganga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Mchuchuma na Liganga ulisainiwa mwaka 2012, sasa hivi ni takribani miaka mitano hakuna jambo lolote linaloendelea katika lile eneo. Kwa hiyo, nataka Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atueleze sababu zipi ambazo zimesababisha mpaka leo mradi ule haujaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili katika eneo hilo, nataka Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuambie kwa nini Serikali mpaka leo haijaanza kujenga *transmission line* ya kutoka Makambako - Songea mpaka Ngaka? Hakuna umeme rahisi baada ya umeme wa maji kama umeme wa makaa ya mawe na nchi nyingi duniani ikiwemo Marekani, South Africa wanategemea umeme wa makaa ya mawe. Sasa ni jambo la kushangaza sana sisi kwenye eneo ambalo tuna makaa ya mawe ya kutosha tunashindwa kutumia *facility* iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Sweden kupitia *SIDA Grants* walikuwa tayari kuisaidia Serikali hii dola za Kimarekani milioni 64 kwa ajili ya kujenga *transmission line* ambayo ingeweza ku-*produce* megawati 120 yenye kilowati 220 ambayo ingekuwa *source* kubwa ya kuwasaidia watu wa Kusini pamoja na maeneo mengine. Umeme huu ungekuwa ni rahisi kuliko umeme mwingine *automatically* ungeenda kupunguza *cost of production* na ungefanya bidhaa ambazo tuna-*produce* ndani ya nchi hii ziwe *cheaper* zaidi. Kwa hiyo, namuomba sana Mheshimiwa Waziri, atakapokuja hapa atuambie kwa nini mradi huu haujaanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo jingine ambalo napenda kuchangia ni suala la *Kurasini Hub.* Mwaka 2012 tulienda Beijing tukasaini ule mkataba wa *Kurasini Hubs* na sisi kama Serikali ya Tanzania tulipewa majukumu, miongoni mwa majukumu tuliyopewa ilikuwa ni kukubali kulipa fidia watu wa Kurasini wote na hilo jambo tumelifanya, lakini toka mwaka huo mpaka sasa hivi hatujaanza. Kama *Kurasini Hub* ingekuwa ime-*take place* tungeweza kuteka biashara za nchi zote za *East and Central Africa. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa njia moja au nyingine tunashindwa kufanya shughuli za msingi ambazo zingelisaidia Taifa hili kupata mapato. Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuambie nikwa nini mpaka leo *Kurasini Logisitic Hub* haijaanza kufanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri aangalie sana vijana wake wa *TRA* kuhusu *tarrifs* na *export,* hizi kwa njia moja au nyingine zinasababisha sisi tupoteze biashara. Kulikuwa kuna Wakongo, Wamalawi na Burundi wengi waliokuwa wanakuja kununua bidhaa hapa nchini, lakini cha kusikitisha unaweza kukuta *colgate* ya gramu 1,000 na *colgate* ya gramu 250 zinatajwa katika *tarrif* moja. Matokeo yake inasababisha gharama za ushuru kwa wafanyabiashara wa hapa nchini zinakuwa kubwa, matokeo yake wanashindwa kuziuza kwa watu wa nchi za nje na wale wanahama kwenda kule. Ule ushuru ungekuwa *cheap automatically* tungeweza kuuza sana na tungepata kodi nyingine kupitia *VAT.*

Kwa hiyo, tufanye utaratibu tuhakikishe tunaangalia kwenye hili eneo kusudi tuweze kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa namna ya kipekee naomba nichukue fursa hii kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha Bunge, wachangiaji wetu jioni wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mheshimiwa Devotha Minja

kwa dakika tano, Mheshimiwa Lathifah Chande kwa dakika tano. Atafuatiwa na Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe nikishasitisha Bunge msiondoke. Tuna shughuli ya uzinduzi wa Kamusi na Mgeni Rasmi Mheshimiwa Waziri Mkuu tayari yuko kwenye ukumbi. Wabunge wa CCM ambao mnakwenda kwenye Kikao cha *caucus* mtakwenda baada ya uzinduzi wa Kamusi hii, Mkutano huu ni mfupi sana hautachukua zaidi ya dakika 30.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi Jioni.

*(Saa 07.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Tukae. Katibu.

**NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa Kwa Mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Mheshimiwa Khatib Said Haji.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa mwanzo jioni hii. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia kusimama hapa yote hii ni rehema zake na wala sio lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwanza kwa kusema ninashukuru kwa bajeti tuliyoletewa hapa na kwa sababu kuna mengi ya kuzungumza nataka kutoa na mimi mawazo yangu kama yataonekana ya maana naomba Mheshimiwa Waziri uyazingatie. Katika bajeti hii limezungumzwa sana na katika Bunge hili na awamu hii na Serikali yetu tumezungumza sana habari ya viwanda. Mimi nataka nikupe maeneo matatu ambayo binafsi nahisi kwamba tukienda sawa tunaweza kupiga hatua kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu tumekuwa tukizungumza habari ya kiwanda cha *General Tyre,* Arusha. Lakini cha kusikitisha ni kwamba tunaishia kwenye kuzungumza. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara. Binafsi tumefanya ziara kule siyo chini ya mara tatu kwa kuona umuhimu wa kiwanda kile kufufuliwa. Sote tumefika hapa kwa kutumia gari na ili gari lizunguke au litembee lazima litumie tairi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kile kingefufuliwa yale matairi, magari ya Serikali na mashirika ya umma tu wakawa yanatumia matairi yanayozalishwa na *General Tyre* ingekuwa tayari ni soko moja kubwa. Lakini kwa bahati mbaya sana imekuwa ni hadithi, hakuna utekelezaji katika jambo hili. Naomba sana leo hii ukichukulia idadi ya tairi za piki piki zinavyotumika nchi hii, tena tairi kutoka China sizizo na viwango, ajali sizizo na msingi zinatokea, magari yanapata ajali kwa matairi ambayo yanaingizwa, kwa hiyo, soko la matairi ndani ya nchi hii, wacha kiwanda cha *General Tyre* hata vikizaliwa vitatu bado Tanzania tuna *demand* kubwa ya matairi, hebu fikirieni hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nataka nizungumzie kuhusu Kiwanda cha *Tanga Fresh*. Kiwanda cha *Tanga Fresh* kimekuwa kikiandamwa na majanga mara kwa mara nilimsikia Mheshimiwa Kitandula akizungumzia kuhusu vikwanzo ambavyo wanavipata, Waheshimiwa wale wa Kiwanda cha Tanga wameshindwa hata kupata mikopo ya benki kwa sababu eti kuna waliowauzia majengo yale kwamba *TRA* wanawadai wale wahusika. Anayedaiwa siyo

wanunuzi, wanaodaiwa ni waliouza. Leo iweje kiwanda kile kinakuwa kila siku kiko ndani ya taabu. Mkumbuke kiwanda cha Tanga ni tegemeo kubwa sana kwa watu wa Tanga, wafugaji wa Tanga wanakitegemea kiwanda kile kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba kimetoka kwenye mdomo wa *FCC* wakikishutumu kwa muda mrefu sana kuhusu kukiuka kwa baadhi ya mambo kikawa kiko ndani ya matatizo, wamekuja sijui ni *TBS* sasa hivi wamekuja *TRA.*

Mheshimiwa Waziri unajua kwenye meza yako iko barua ya kiwanda kile kutaka kusaidiwa kufanya kazi zake kwa uzuri, tuvilee viwanda vyetu. Naelewa kwamba kuna viwanda vya Kenya, *Brooklyne* ambao hawapendi kuona *Tanga Fresh* ni washindani wao wakubwa. Leo Tanzania tuna kiwanda cha *Tanga Fresh* na Asas ndiyo viwanda vikubwa vya maziwa. Lazima tuvilee, uzalendo uanzia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie A - Z na mnaelewa kuna tatizo gani. Kuhusu *rate* yao ile ambayo wamewekewa. Nawaomba sana Malaria ni janga la kitaifa na lazima tulikuwa kwenye semina pamoja na Naibu Waziri alisikia malalamiko ya kiwanda kile ambayo ina hatarisha kwenda kufungwa na kupunguza idadi kubwa ya wafanyakazi katika kiwanda kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani michango hiyo mitatu kwenye kusaidia bajeti yetu inatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie kauli ambazo zimekuwa zikitawala sana kuhusu makanikia. Kiongozi mwenza wa UKAWA Mheshimiwa Francis Mbatia aliongea kwamba katika sisi hakuna anayepinga jitihada za kunusuru mali za Taifa hili. Kama limesemwa hilo na Mwenyekiti wetu na hakuna aliyempinga maana yake ni kwamba hayo ndiyo mawazo yetu. Wasijitokeze wengine wakatulisha maneno kuonekana kwa Watanzania kana kwamba tunapinga juhudi za kulinda mali zetu. Hiyo ndiyo ajenda yetu

siku zote na tumekuwa tukiwaambia hivyo. Lakini kwa sababu yalitoka upande huu mliyaona siyo. Sasa mme-*prove* ndiyo twendeni mbele, tusiangalie nyuma tena, tuko pamoja katika hili la kulinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani kila mtu ana-*style* yake ya kulipokea jambo. Wenzetu mnakimbilia sana sherehe *celebrate festivals.* Sisi kwanza tunapima upepo kuona mambo yanaendaje.

Waheshimiwa Wabunge niwape mfano, Bunge la Katiba mlisherehekea sana. Wengine wakakata viuno humu ndani lakini Katiba iko wapi mpaka leo. Hamkutosheka mkaenda jamhuri mkacheza na mkaimba, Katiba iko wapi mpaka leo. Kwa hiyo, si hoja awali, ni heri hatima. Hayo sisi wengine tunaota ndoto kubwa kwa pesa zile zilizotajwa tunatamani yatokee na Tanzania inufaike na yale yaliyozungumzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tunapozungumza haya wengine mnatupa majina mabaya. Yuko Mbunge mmoja kule alinyanyuka akatuita sisi *UNITA* akamfananisha Kiongozi wetu na Savimbi. Lakini nawaonya wanasiasa wenzangu, majina mabaya tusiitane kiasi hicho, kwa sababu leo upo huko inaweza ika-*change ring* ukaja huku. Wako viongozi wakubwa walikuweko huko leo tunao huku na wako wengine tulikuwa nao huku leo wako huko. Haya ni mambo ya mbadilishano tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mtu anatuita sisi *UNITA,* lakini mimi nakumbuka Bunge la Katiba alikuwemo Mheshimiwa mmoja anaitwa Ibrahimu Lipumba aliwaita ninyi *Intarahamwe.* Leo *Intarahamwe* katafute Intarahamwe mwenzio wamekwenda kukaa nao. Ni suala la muda la muda tu kwa sababu anakamilisha kazi aliyopewa ni rasmi tu atakuwa Mkuu wa Mkoa, atakuwa Mkuu Msaidizi wa Gavana tunayaelewa hayo. Tunamwombea safari njema. Akamilishe kazi yake aliyotumwa arudi akaye na *Intarahamwe* wenziwe. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie kuhusu misaada ya wahisani. Hili nisingetaka kulizungumza kwa sababu ninapozungumza wahisani nitaigusa Zanzibar na nikigusa Zanzibar nitagusa uchaguzi wa Zanzibar na najua kuna watu hawataki nizungumze uchanguzi wa Zanzibar, lakini hili haliepukiki. Mwanzo nilisema Uchaguzi wa Zanzibar ni chozi la mbwa mmelikosea kulinywa moto, halitaweza kunyweka tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme hivi, kwenye bajeti yako hii asilimia 12.5 umetegemea fedha za wahisani. Fedha za wahisani kwenye bajeti iliyopita unatuambia haikutoka na ndiyo ukweli. Leo umerudi umeandika tena humu kwamba unategemea asilimia 12.5 ni fedha za wahisani. Wahisani wamegoma kutoa pesa na sababu mnaijua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchaguzi uliofanyika Zanzibar na Sheria ya Mtandao yanainyima nchi hii fursa ya kupata fedha zile za kuisaidia bajeti. Nisingeshughulika sana kama ingekuwa ni pesa ambayo haimo kwenye bajeti ningeacha kusema hilo. Hasa mimi nawashauri Wahisani wanaozuia kutoa pesa zile wazungumza na ninyi lakini ninyi mnashindwa kufika *point*. Mnashindwa kufikia makubaliano nawaomba sana, fursa hii wa sababu ya kumlinda *Babu Ali kule Zanzibar isiwe sababu ya Watanzania kukosa...***[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa tulishatoa *ruling* watambulisheni viongozi kwa majina yao, futa hilo neno na mtambulishe kwa jina lake sahihi.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Ahsante, Daktari Mohamed Ali Shein.

**MWENYEKITI:** Futa lile neno Babu Ali.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, limeshafutika hilo halipo. Ahsante sana nawaambia Waziri wa Mambo ya Nje anajua masuala anayokumbana nayo

msaidieni. Kubalini na eleweni nini kimetokea. Uchaguzi ulifanyika tarehe 25 Oktoba, ndiyo huu uliomuweka Rais John Magufuli madarakani tunamtambua, wala hatupingi kwa hilo, lakini uchaguzi mwingine ule, uchaguzi wa Zanzibar umefanyika matokeo ndiyo yametuweka sisi Wabunge humu. Eti chakula kimepikwa jungu moja wa chini umeiva wa juu haukuiva mmeyaona wapi. Haya ni maajabu ya dunia, uchaguzi uliisha na matokeo wahisani yote wanayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia ilikuwa inaangazia uchaguzi wetu na waliona, leo Mheshimiwa Jecha maana afadhali ingekuwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilifuta uchaguzi ule, lakini Tume ya Uchaguzi haikufuta, Jecha alitoka pale akaenda akakaa kwake sijui siku hiyo aliwekewa kikuba gani na mkewe akakinusa akaenda chafya, akafuta uchaguzi wa Zanzibar. Huu ni upumbavu ambao unatutesa ndani ya nchi. Unatutesa kwa sababu sisi tunaumia sana. Nchi hii inayo bajeti yetu ni *high jump,* hatukufikia asilimia 29 tumeweka 30 na leo mchezo wa *high jump* mrukaji anaanzia chini kwenda juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mara hii ya Mheshimiwa Mpango sasa pale alipokuwa hakufika kapandisha ule mti juu zaidi ili aruke, sasa sijui maajabu ambayo yatatumika. Sielewi maajabu gani yatatumika, mimi nakuombea dua sana. Lakini nakuomba kaaeni mtafakati suala la Zanzibar dunia inatuangalia. Suala la mitandao dunia inawangalia, tumalizeni tufaidike, za makanikia bado zina muda. Mimi yalaiti ingekuwa zile za makilikia zinatoka katika kipindi hiki ningesema tuwaache Wazanzibar waendelee wanavyokwenda, maamuzi yao yadharauliwe. Lakini kwa sababu ya tunategemea wahisani lazima muukubali ukweli hata kama ni mchungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yuko mwanafalsafa mmoja alisema usiyempenda akisema maneno mazuri yakubali, na unayempenda anaposema mabaya uyachukie. *(Makofi)*

Kwa hiyo,...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Devotha Minja kwa dakika tano, ajiandae Mheshimiwa Lathifah Chande kwa dakika tano.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichukue dakika tano kuchangia bajeti. Nilimsikiliza sana Waziri wakati akiwasilisha bajeti ile, suala la kufuta *motor vehicle* na kurudisha shilingi 40 kwenye mafuta ni kama umeiba kutoka mkono huu na kupeleka mkono wa kushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nani asiyefahamu kwamba ukigusa mafuta umegusa kila mahali. Ni nani asiyefahamu umuhimu wa mafuta kwa nchi hii mnatuambia tunakwenda kwenye nchi ya viwanda. Hiyo *motor vehicle* ambayo imefutwa sijui Waziri alifanya *research* kiasi gani nakuona kwamba labda iwe *compansated* na shilingi 40 na ni kwa nini 40 tunataka kufahamu, kwa nini isiwe shilingi 10 au tano?.

Mheshimiwa Mwenyekiti kuna mambo ya msingi ambayo lazima niyaangalie. Ukizungumza habari ya mafuta unazungumza maisha ya watu. Hatuwezi kwenda kwenye viwanda kama mafuta bado yako juu. Huwezi kugusa uzalisaji wa namna yoyote kama mafuta bado yako juu. Kwa hiyo, ni lazima Waziri aangalie upya suala hili la kuongeza shilingi 40 kwenye mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia pia katika kitabu cha bajeti ya Waziri. Anazungumzia kwamba kufutwa kwa hizi *road licence* pengine zitasaidia na hakutakuwa na shida na itawezesha watu wengi wenye magari waweze kuendelea kufanya kazi zao vizuri. Lakini ninachotaka kukuambia *analysis* ambazo tumezifanya shilingi 40 kwa mtu mwenye scania au basi anatoka Dar es Salaam anakwenda Mbeya anatumia *may be* lita 600, *go and return* lita 600 ukizidisha mara arobani tunazungumzia shilingi 24,000 kwa

siku. Kwa mwezi tunazungumzia shilingi 720,000, kwa mwaka nzima tunazungumzia shilingi 8,640,000 wakati hiyo *motor vehicle* ilikuwa haizidi shilingi 500,000. Kwa hiyo, tunachoona ni kwamba watakaokwenda kuumia ni Watanzania, kwa sababu kila mtu lazima atumie usafiri kwa vyovyote vile iwe kusafirisha mazao, kwenda kokote anakoweza lakini tutakwenda kuwaumiza Watanzania, kwa hivyo naona hii shilingi 40 haina tija. *Otherwise* angetuambia ni kwa nini shilingi 40 na isiwe shilingi tano au isiwe shilingi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia kwenye bajeti ya Waziri kila mwaka sigara, pombe zinapanda. Siku Watanzania watalala waamke, wamwelewe vizuri Naibu Waziri Kigwangalla na Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu kuhusu suala la *no smoking* hatutakuwa na bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema sigara hizi ndiyo zinaleta madhara, ndiyo zinazotuletea kansa, kifua kikuu, tunakiwa na maadhimisho ya siku kifua kikuu. Fedha hizi hizi zinazosema tunazosema tuna-*save* huku tunakwenda kutibia watu wetu ambao wanaugua magonjwa yanayotokana na sigara na pombe. Kwa hiyo, ifike mahali tutatafute *sources* nyingine ambazo zinaweza zikasaidia Watanzania na siyo kucheza na afya za Watanzania, kuendelea kupandisha kila wakati haizuii mtu kutumia sigara. Lakini tungetafuta vyanzo mbadala ambavyo ni *reliable* vitakavyosaidia Taifa hili kupata mapato halali bila kuwa na athari kwa wananchi wanaotumia vitu hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala lingine la bandari, ni aibu. Hotuba ya Kambi ya Upinzani imesema kwamba lazima kuwe na vyanzo vingine ambavyo vitalisaidia Taifa hili. Tukiangalia nchi zingine zinafanya vizuri, angalieni Bandari ya Beira, angalieni Mombasa wanavyofanya vizuri na *World Bank* wamewahi kusema endapo tutatumia vizuri bandari, zaidi ya asilimia 30 tunaweza tuka-*save* kwenye bajeti yetu. Sasa hivi bandari imegeuka siasa. Viongozi wa Serikali wanaamka asubuhi na vyombo vya habari wanakwenda bandarini kutumbua watu.

Mheshimiwa Waziri kwa nini tusikubali kwamba tunahitaji watu *professional* watusaidie tufanye nini ili bandari zifanye kazi vizuri. Tuna Bandari ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara yenye kina kirefu lakini bado hazisaidii mchango kwenye hii bajeti yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuangalie haya mambo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lathifah Chande.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru lakini siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE:** Mheshimwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia mjadala huu wa bajeti. Kwa kuwa Wabunge wengi hapa wameongea hili suala la makinikia naona ni vema na mimi niweze kuligusia kidogo pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wizi wa madini ya nchi hii vilevile suala la mikataba mibovu ya madini na suala ya sheria mbovu za madini imekuwa ni kilio cha wapinzani kwa miaka mingi sana na Watanzania kwa ujumla. Na kwa kuwa Serikali hii hii ya CCM ndiyo iliyolea huo wizi kwa kipindi chote hicho kwa kuleta mikataba mibovu ya madini na sheria mbovu za madini, basi Serikali hiyo ya CCM pamoja na Wabunge wake wa CCM wanawajibu wa kuwaomba msamaha na kuwaomba radhi kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kuchangia mjadala huu wa bajeti iliyoletwa hapa. Naunga mkono maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani na ningependa kuanza kwa kuongelea juu ya miradi ya maendeleo. Serikali inapaswa ielekeze pesa nyingi katika miradi ya maendeleo ambayo ina wananchi wengi *(labour intensive),* kama vile sekta za uvuvi, kilimo, na sekta za ufugaji. Kwa nini nasema hivyo,

nasema hivyo kwa sababu hizi ni sekta ambazo zina shughuli ambazo ni endelevu *na* haziitaji watu walioandaliwa *skilled labour.*

Vilevile tofauti na hivyo leo hii Serikali inajinadi kwamba imetoa ajira kwa wananchi wengi lakini hizo walizozitoa siyo ajira bali ni vibarua ambavyo havina mwendelezo wowote. Kwa sababu wameelekeza pesa nyingi kwenye miradi ya maendeleo ambayo ni *capital intensive* ambapo ili iweze kufanikiwa hiyo miradi lazima itumike mitaji ya kuwezesha kununua mashine na mitambo na pesa nyingi zinaelekezwa kwenye kuwalipa wasimamizi na wataalam ambao wengi wao siyo Watanzania ni wananchi kutoka nchi nyingine tofauti, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ningependa kuchangia juu ya Sera za kikodi. Sera za kikodi kwa mfano, Serikali ya Awamu ya Tano ilikuwa na nia njema ya kutaka kukusanya madeni ya kodi ambayo yalikuwa yamelimbikizwa kwa muda mrefu, hiyo ni nia njema kabisa ya Serikali ya Awamu Tano. Lakini sasa sera ya kikodi imeonesha mapungufu pale ambapo Serikali ilitaka wadaiwa hawa walipe madeni yote haya ya kodi ndani ya muda maalum bila kuangalia athari za kiuchumi ambazo zingeweza kujitokeza, matokeo yake wanafanyabiashara wengi wao wakiwa wenye makampuni makubwa walilazimika kwenda kwenye taasisi za kifedha na mabenki mbalimbali kukopa pesa ili waweze kulipa hayo madeni ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mmoja walifanikiwa kulipa madeni haya ya kodi lakini kwa upande mwingine walishindwa kurejesha ile mikopo kwenye hizo taasisi za kifedha na kupelekea sekta ya fedha kudorora na hadi baadhi ya mabenki kufungwa. Sasa sera za kikodi zinapaswa zielekeze na ziweze kuzingatia maeneo mengine ya uchumi ambayo yanaweza yakaathiriwa kwa njia moja au nyingine pale ambapo ikiwa njia za kutekeleza hilo, hata kama ni nia njema lakini pia liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine ni kuhusu sera za kifedha. Sera za kifedha zinatakiwa zielekezwe katika kuhakikisha kwamba ukuaji wa uchumi unakuwa shirikishi yaani *inclusive economic growth* kwa ajili ya kuweza kutoa ule utata uliko kwamba sasa hivi kwenye makaratasi na takwimu ina……

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bupe, jiandae Mheshimiwa Mama Salma Kikwete.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia bajeti hii muhimu.

Awali ya yote namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika bajeti hii muhimu. Pia naomba nimpongeze Waziri Mheshimiwa Dkt. Mpango na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Kijaji kwa kazi nzuri wanazozifanya pamoja na Makatibu Wakuu wote wa Wizara hii nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naomba nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anazozifanya na nina salamu zake nyingi sana kutoka Mkoa wa Rukwa. Wanawake wa Mkoa wa Rukwa wanampongeza sana Mheshimiwa Rais, wanasema sehemu zingine wamezoea kumuandalia Rais ng'ombe, kuku na ndama lakini wanawake wa Mkoa wa Rukwa wamenituma wanasema hivi wa kazi nzuri alizozifanya Dkt. Pombe Magufuli, wamemwandalia mgolole, watambeba na mbeleko ya mgolole. Watambeba mgongoni kwa kazi nzuri anazozifanya, Mungu ambariki huko aliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye maji. Wanawake wa Mkoa wa Rukwa hawana maji, karibu asilimia 20 wana maji, ukienda vijijini wanawake wanapata shida

sana ya maji lakini Wilaya ya Sumbawanga Mjini ninaishukuru Serikali ya Dkt. John Pombe Magufuli imesimamisha matenki, maji watapata ya uhakika. Ninaishauri kule vijijini wanawake wanapata shida, maji yaende kule, ile shilingi 40 ya mafuta naungana na bajeti kwamba iende kwenye maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie kwenye suala la barabara. Mkoa wa Rukwa ni Mkoa ambao unalima mazao na yanakubali, una mvua za uhakika, lakini barabara ya Wilaya ambapo mazao yanatoka mengi, barabara inayotoka Kibaoni inapita Muze, Mtowisa na inaishia Mlowo ile barabara ni muhimu sana, imejengwa kwa kiwango cha kokoto, lakini bado madaraja yake ni shida. Kutokana na umuhimu wa barabara hii, ningeomba bajeti ya safari hii iweke kiwango cha lami kwa sababu ufuta, mpunga, ulezi na matunda yanatoka kule, ninaomba kwa bajeti hii ikumbuke hiyo barabara ijengwe kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye suala la elimu. Mkoa wa Rukwa hauna Chuo cha *VETA,* vijana wanapata shida sana. Suala la *VETA* limeongelewa muda mrefu sana na naipongeza Serikali katika bajeti yake imeongea kwamba itajenga Chuo cha *VETA,* ninaomba iipe kipaumbele Mkoa wa Rukwa kujenga hicho chuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna chuo kingine ambacho amejenga mwanamke/mama ambaye hajasoma lakini amediriki kujenga Chuo cha Wauguzi, amejenga Chuo cha Ualimu na Chuo cha Kilimo, lakini Chuo cha Wauguzi kimefungwa bila sababu za msingi. Naomba Dkt. Mpango atakapokuja kutoa majumuisho hapa anieleze hicho chuo ni kwa nini kimefungwa? Chuo ambacho ni cha mwanamke ambaye hajawahi kwenda shule, ameamua kuanzisha chuo, kwa nini kifungwe bila sababu za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye suala la afya Mkoa wa Rukwa karibu Wilaya zake zote hazina Hospitali ya Wilaya. Ninaipongeza Serikali kwamba pale Mkoa wa Rukwa, Sumbawanga Mjini ile hospitali iliyokuwa ya Mkoa

imepandishwa kuwa ya rufaa lakini hakuna Hospitali ya Wilaya. Wanawake na watoto wanapata shida sana wanapotaka kujifungua, wanaambiwa kwamba mkaanzie kwenye vituo vya afya na vituo vya afya kule wanaambiwa hatuna bajeti za mtoto na mama kujifungua bure. Ninaomba bajeti hii ikawasaidie kujenga Hospitali ya Wilaya ya Sumbawanga Mjini, Nkasi na Kalambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Salma Kikwete, ajiandae Mheshimiwa Taska Mbogo.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Sambamba na hilo, nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya. Kazi hizi nzuri zinazofanywa tukiziainisha hapa ni nyingi na kwa wingi wake huo kumekuwa na mafanikio makubwa sana ndani ya kipindi chake cha uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, niwapongeze Mawaziri wetu wa Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mpango na Naibu wake kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya. Kwa ujumla bajeti hii ya Serikali imegusa kila sehemu yaani bajeti ya wananchi. Wananchi wamepunguziwa kwa kiasi kikubwa sana na bajeti inayoonyesha muelekeo na mwelekeo huu ni ushindi wa mwaka 2020 na hatimaye kuelekea kule mbele ya safari 2025, ongezeni hizo juhudi ili tufike 2025, na hatimaye tuzidi kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kwenye maeneo kama mawili/matatu hivi. Eneo la kwanza, wakati Waziri anasoma bajeti ya Wizara ya Fedha alielezea suala la kinu cha kuchakata gesi pale Lindi ambacho kinu hiki kiko eneo linaitwa Likong'o. Baada ya hapo kwa kweli nilipiga sana

makofi na nilipiga hili benchi nafikiri watu wengi walisikia. Msingi wangu mkubwa ni kwamba kinu kile kikipelekwa pale matokeo yake tunazungumzia hii nchi ni nchi ya viwanda, na ikiwa ni nchi ya viwanda na wananchi wa Lindi wale watafaidika na kauli mbiu hii ya Awamu ya Tano kwamba iwe ni nchi ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini limetokea? Wakati anaisoma hii bajeti ya Serikali ambayo ndio inayotoa mwelekeo nini kinafanyika ndani ya Taifa, hakukuwa na jambo lolote lililojitokeza juu ya kinu kile na wananchi wa Lindi wanasubiri. Hata kama sio leo au kesho, lakini wapewe mwelekeo ni nini kinafanyika. Kikubwa zaidi hii ni gesi na gesi itaongeza uchumi wa Lindi, kiwanda kile kikijengwa Lindi kama Lindi hakuna kiwanda hata kimoja. Wananchi wa Lindi ni maskini lakini sio maskini kwa sababu hakuna rasilimali, ni kwa sababu mimi naamini wakati ulikuwa haujafika na sasa wakati umefika na wananchi wale wa Lindi kufurahia matunda ya nchi yao. Naomba atakapokuja Mheshimiwa Waziri anipe mwelekeo nini hatima ya kinu kile cha kuchakata gesi ndani ya Mkoa wetu wa Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji. Nilizungumzia suala la maji, sasa ninachosubiri hapa ni matokeo. Je, kati ya tarehe 3 mpaka 10 mwezi wa saba maji haya yatapatikana au hayatapatikana, kwa sababu maji ni kilio kikubwa sana ndani ya Mkoa wa Lindi hasa Wilaya ya Lindi Mjini na maeneo yake ya jirani. Tanzania tumejaliwa tuna mito, mabonde na tuna maziwa, kama tukiwekeza vizuri matatizo haya yatapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niende kwenye eneo la elimu. Mimi kwa taaluma ni mwalimu, sasa hii naiomba niishauri Serikali. Unajua sisi tuna senti, inaanzia senti tano hatukuanzia na senti moja mpaka senti mia moja. Ninachoishauri mimi kama mwalimu nilikuwa napata changamoto na hii changamoto inazidi kuendelea. Wakati zinatengenezwa zile fedha zitengenezwe hizi senti tano, ukiingia leo darasani kumfundisha mwanafunzi senti tano, senti 20 na senti 50 zinafananaje. Ni lazima tumuonyeshe kitu

kwa uhalisia, tupeleke vitu wanafunzi wajifunze, hili ni muhimu sana ili wanafunzi waweze kutambua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la elimu kwa kweli tumepiga hatua, tumefanya mambo mengi sana kwenye elimu kwa kipindi kifupi. Tumeboresha shule zote zina madawati, upande wa walimu wa sanaa wote wamejaa, lakini tatizo sasa ni baadhi ya walimu kwenye maeneo ya sayansi. Sasa hapa ni lazima tuwekeze vya kutosha ili watoto wetu wafanye kazi kwa vitendo, halafu hii nitairudia tena na walimu wale ambao wamejifunza na hatimaye wakapata aidha Shahada au Diploma zao wasiendelee kwenda kwenye vyuo kwa sababu lengo ni kuboresha elimu, wabaki kwenye shule zile za msingi, jambo kubwa hapa waboreshewe mahitaji yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo lingine kubwa, kuna suala zima la nyumba za walimu bado hapa tupo nyuma. Kwa kuwa tuna tatizo la nyumba za walimu, vijana wengi hapa wamezaliwa katika mazingira ambayo sisi tunayajua, sasa kijana aliyezaliwa na kukulia Dar es Salaam leo hii umpeleke kule Chikonje ambako mimi ndio nilianzia ile kazi yangu kwa mara ya kwanza, akifika akiangalia, akisikia yale mabundi na wanyama wengine wanalia mwalimu anakusanya na anaondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja, lakini nitakuwa ni mtovu wa fadhila... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Mheshimiwa Taska Mbogo hayupo, Mheshimiwa Edwin Sannda. Waheshimiwa kwa upande wa CCM sasa mtakuwa mnachangia dakika tano/tano.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mimi naomba nimalizie fursa ya kuchangia

kwa dakika kumi halafu tutaendelea na huo mfumo wa dakika tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nataka nichukue fursa hii kuipongeza Serikali, nimpongeze pacha wangu hapo Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Ashatu, nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Mpango, lakini pia nimpongeze Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na timu yake nzima ya Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia labda huenda dakika tano zikawa hazikutosha basi mimi nasema naanza na kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuongelea mambo makubwa matatu ama manne, kwanza ni suala lile la shilingi milioni 50 kila kijiji. Unajua ile ni ahadi yetu kwenye Ilani na tumefika kule tumejitangaza vizuri na kila mtu anasubiria. Kwenye bajeti hii hakuna lililoongelewa. Mwaka jana tuliambiwa na pesa kiasi cha shilingi milioni 59 zitatengwa, mwaka huu kimya kabisa. Hebu tusaidieni tunaenda kujibu nini na ni ahadi ambayo tumeitoa, hii nafikiri haijakaa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, itabidi niende haraka ni zile shilingi milioni 40 ambazo kwenye hotuba tumezungumzia kwa maana ya suala zima la *road license.* Mimi nataka nishauri badala ya kusema *road license* ambayo itapeleka mzigo mkubwa sana kwa wananchi wengi ambao hawatumii hayo magari, ile shilingi 40 ifanywe tuiweke kwenye mfuko wa maji, wengi wamezungumza hiyo. Isiwe shilingi 40 turudishe iwe shilingi 50 badala ya shilingi 40 iingie kwenye Mfuko wa Maji, kama tutatenga kidogo katika hicho kisehemu ika-*cover* kwenye suala la *road license* sawa lakini maji hata ukiweka, najua mafuta yanaongeza gharama kwenye kila kitu lakini kama yanaongeza gharama halafu unaenda kuwapatia wananchi wa kawaida maji umefanya jambo jema kabisa na jambo kubwa. *(Makofi)*

Nafikiri hiyo itakuwa imeondoa sintofahamu ambayo Wabunge wengi wameongelea hapa. Nawaomba sana tulitafakari hilo na tulielekeze huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, nimeona kwenye hotuba yako viashiria vya uchumi jumla; takwimu zote zinaonesha uchumi upo vizuri na tunakwenda vizuri kadri ya taarifa yako sawa, lakini hali halisi kwa wananchi huku ni kitu tofauti kabisa hasa wananchi wale wenye hali ya chini, wa kati na hata wale wa juu, hali halisi ya mzunguko ile tumezungumzia mzunguko wa fedha kuwepo ni ngumu kweli. Nakuomba Mheshimiwa Waziri hebu tufafanulie, huenda sisi labda upande huu wa masuala ya fedha hatuko vizuri sana lakini tuelezee hivi hii hali unaielezaje. Viashiria vyote viko vizuri sana na tunaelekea vizuri, lakini uhalisia hauko sawa, hauko vizuri ni kilio kila mahali, mfanyabiashara wa kati na chini kila mmoja analia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne nimeona tunafanya kuboresha kwenye kuondoa kodi za bidhaa kwenye bidhaa ambazo tunataka walau tu-*promote,* kwa mfano kazi zetu kama lile la upande wa vyandarua na hasa vyandarua vilivyowekwa viuatilifu vya malaria. Tuna dhamira ya kwenda kuondosha malaria moja kwa moja, vyandarua vinavyotengenezwa ndani vina Kodi ya Ongezeko la Thamani wakati vinavyotoka nje huenda havina, hivi una mfanya vipi huyu mtu aweze ku-*compete* na wale wa nje? Ili tuweze kuwapa *incentive* hawa wetu wa ndani wanaoweza kuzalisha hivi waweze kwenda kutusaidia kuondoa malaria basi vyandarua vile vyenye viuatilifu vya kuua wadudu wa malaria basi vifanyiwe utaratibu na vyenyewe viondolewe Kodi ya Ongezeko la Thamani ili waweze kuvizalisha kwa wingi viwanda vyao vikue na viweze kuwa endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nafikiri kwa ufupi ningependa kugusia hayo matano, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Phillipo Mulugo ajiandae Mheshimiwa Jitu Soni.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kupewa nafasi dakika tano hizi za kuchangia Wizara Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina hoja ndogo sana leo, Mheshimiwa Dkt. Mpango naomba unielewe, nakuwa nazungumza kila siku kwenye hotuba zangu namna ambavyo Wizara yako, hususan pale Hazina, sijui kuna mfumo gani mnaoweka, jinsi mnavyopendelea kutuma fedha kwenye Halmashauri. Baadhi ya Halmashauri hatupati fedha, hata kama ni hizo hela ambazo mnakuwa mmekusanya ndogo baadhi ya Halmashauri hatupati fedha, tunalalamika kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema kila siku hapa, nina Wilaya mpya lakini sina maji, sina barabara ya lami, sina vijiji vyenye umeme kama vijiji vingine, sina kiwanda hata kimoja, hata Chuo cha *VETA* hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013 niliambiwa nitafute eneo, tukatafuta eneo ekari 100 pale Mkwajuni na hatimiliki ipo, lakini mpaka leo hakuna mikakati yoyote ya kuniletea *VETA* pale Wilaya ya Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kila siku nasema, nina Wilaya mpya sina Hospitali ya Wilaya, sasa nataka kuona bajeti ya mwaka huu kama mnaniletea hivi vitu, kwa sababu sehemu nyingine wanavyo. Sasa mnapogawa fedha pale Hazina kwa nini hakuna Kamati Maalum ambayo angalau ingekuwa inatenga kwamba *okay,* hiki kinakwenda Same, Same wana hiki na hiki, labda hiki kinakwenda Halmashauri ya Tunduru, Tunduru hawana hiki basi hiki kiende kwenye Halmashauri fulani, yaani kuwe na *relation* fulani ya kuona kwamba Halmashauri nyingine wana hiki basi na hawa wapewe hiki, tungekuwa tunakwenda hivyo nchi hii ingeendelea hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna watu wanapewa *ambulance* hapa, wengine hata haijulikani tunapewa lini. Yaani unakuta kila siku wewe ni mtu wa mwisho tu. Jamani mnataka tuseme nini humu ndani, sisi wengine

sio Wabunge? Naomba, nimelia Barabara ya kutoka Mbalizi kwenda Mkwajuni kilometa 90 tupate lami, hakuna, lakini ukija kwa Waziri wa Barabara hapa unakuta barabara inakwenda maeneo fulani. Wanazo barabara, lakini wana hospitali, wana majengo ya Wilaya, sisi wengine mtatupa lini vitu vyetu? Jamani, wote ni Watanzania tugawane keki hiyo, nalalamika kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Wizara hii hupati chochote, ukienda huku hupati chochote. Juzi nimelia habari za umeme hapa; nashukuru sana Mheshimiwa Dkt. Kalemani hapa amenitafutia watu wa *REA* nimekaa nao tumepanga vitu. Yaani mpaka useme ndio upate, usipolalamika hupati, kwa nini? Mnataka tuje tuanze kulia machozi humu ndani ya Bunge? Jamani, tunataka na sisi tupate keki ya Taifa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi hapa, sijui ni mwaka gani, kuna Mbunge mmoja hapa alisema Serikali inapendelea, tena alisema wazi, nadhani alikuwa ni Mheshimiwa Zitto, na mimi nataka kusema Serikali inapendelea, kwa nini wengine hatupati wengine mnapata? Mikoa ya Rukwa, Katavi, Songwe na Kigoma, hatuna chochote, fedha zote zinakwenda mikoa mingine, kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Dkt. Mpango, weka pale Hazina tume ndogo itakayokuwa inaangalia kwamba hiki kama kimekwenda mahali fulani basi *trip* nyingine wapate na wengine hivi, tugawane jamani, wote ni Wabunge humu ndani na wote ni wananchi, kila siku tunalia mambo hayo hayo, eeh, jamani. Tafadhali, ninaomba kwenye bajeti hii mnipe Hospitali ya Wilaya pale Songwe, ni mbali sana kutoka pale Songwe tunakwenda kuhudumiwa na Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalia kila kitu, mimi nikisimama hapa kila siku ni malalamiko tu, hakuna siku ya kuja kusema jamani na mimi angalau nimepata hiki. Nataka na mimi niwe ni Mbunge ambaye nikisimama niseme Serikali

nashukuru mmenipa hiki, sasa kila siku mimi ni kulalamika tu, hamnionei huruma? Kila siku tunalalamika tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali naomba sana, Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, nataka kwenye bajeti hii mnipe maji. Mwaka kesho kwenye bajeti ya Serikali hapa mtanitambua kama hamjanipa hivi vitu. Tupatieni basi, ni hilo tu kwa leo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Jitu atafuatiwa na Mheshimiwa Waitara atafuatiwa na Mheshimiwa Frank George Mwakajoka.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali, kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri sana anayoifanya pamoja na Serikali yake yote. Nimpongeze Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na timu yake nzima kwa kazi nzuri wanayofanya, tunaendelea kukuombea na tunasema endelea na mfumo huo huo ili tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeomba kushauri; pamoja na kuwa kazi inayofanyika ni kubwa na nzuri lakini bado kuna nafasi kubwa ya kuboresha na hayo ambayo tutayasema ili mjitahidi kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, ninaomba lile suala la Serikali kurudisha madaraka ya Waziri wa Fedha na Mipango ya kusamehe kodi, tulifuta huko nyuma kwa ajili ya matumizi mabaya ya msamaha huo. Mimi naomba haya madaraka yarudi ili miradi mingi ambayo tunapata msaada katika Serikali Kuu, Halmashauri zetu na taasisi mbalimbali iweze kuisaidia Serikali. Leo hii inashindwa kupata msamaha wa kodi na miradi mingi inakwama kutokana na suala hilo.

Kwa hiyo, mimi naamini kwenye hii Serikali ya Awamu ya Tano hakuna atakayethubutu kutumia hayo madaraka vibaya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba mje na

mpango huo tuirudishe ili miradi ambayo inakwama kutokana na suala la kusamehewa kodi, basi na yenyewe tuweze kufaidi misaada hiyo ambayo tunapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ninapenda nikupongeze kwa kuondoa kodi ya *Motor Vehicle Licence,* Sheria ya *Traffic Act*. Hapa tunajichanganya, zile ni sheria mbili tofauti, *Traffic Act* umeondoa kwa kulipa kila mwaka, haijaondolewa kwa ujumla, umeondoa utalipa mara moja tu kwa gari inaposajiliwa. Hii nyingine ni *excise duty* ilikuwepo, shilingi 400 umeongeza hii shilingi 40, hongera sana kwa sababu fedha hizo hizo ndizo zitakazoboresha barabara na huduma nyingine ambazo hawa ambao tunalalamika kwamba mafuta ya taa na nini, kwamba wanafanyaje, kwa sababu hiyo barabara ambayo inaenda huko kijijini ndiyo inalipiwa na fedha hiyo. Mimi nasema ungeongeza zaidi ili huduma hizi nyingine zote ziendelee kuboreshwa huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba katika ule wigo ulipotaja vile viwanda ambavyo vitapata msamaha umetaja sekta kama nne; ya mafuta, ya ngozi, lakini ninaomba mtanue wigo zaidi ili sekta nyingine pia kama za kilimo, mifugo, uvuvi pia viwanda vidogo vidogo. Hao wakubwa watakuja watapitia *TIC* watapata huo msamaha, lakini hivi viwanda vidogo vidogo vya Watanzania wenye mtaji mdogo pia na wenyewe mngewapatia huo msamaha kwenye *capital goods* na wakati wanataka kuanzisha. Hiyo kodi ikiondoka nina uhakika kwamba huko tunakotaka kuelekea kwenye uchumi wa viwanda tutaweza kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, tutakapoelekea kwenye *Finance Bill* nitaomba maeneo mengi yale niliwapongeza kwamba mmeondoa kodi nyingi kwenye sekta ya kilimo; lakini kwenye sekta ya mbegu bado kuna kodi nyingi ambazo zimeachwa, lakini pia tuangalie mfumo mzima kwamba tunafanyaje. Tumesamehe, kwa mfano kwenye mbolea inayotoka nje ya nchi, pongezi kubwa kwa hilo, lakini je, kiwanda cha ndani, huyu wa nje kama amesamehewa yote na wa ndani anaendelea kulipa je, si kwamba tunaendelea na mfumo ule ule kwamba tutaua

viwanda vya ndani kwa kuruhusu vitu kutoka nje kuingia bila kodi? Kwa sababu huyu wa ndani hawezi kutoza *VAT, inputs* zake hawezi kudai, kwa hiyo bado utaendelea kuumiza viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado mimi naona kwenye sera yetu panatakiwa kufanyika mabadiliko makubwa na wigo wa kukusanya kodi bado ni mdogo. Nikupongeze kwamba mmesema kila Mtanzania ambaye anafanya biashara hata kidogo aendelee kulipa kodi, elimu kubwa iendelee kutolewa ili kila Mtanzania aweze kulipa kodi. Muhimu ni kwamba sekta isiyokuwa rasmi bado ni kubwa na inaendelea kukua; mimi ninaomba, sijaona kabisa kwenye bajeti nzima sehemu ambapo mtaweza kufanya sekta isiyokuwa rasmi ihamie kuwa rasmi kwa sababu ile sera haijakaa vizuri na *incentives* zile hazipo, na muhimu kwenye uwekezaji wa aina yoyote ni zile *incentives.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ningependa kuona kwamba vyanzo vingine vyote vipya tuendelee kuviangalia na tuweze kupata kodi ambapo badala ya kutegemea hao wenzetu ambao wanatupa misaada kwa sababu ile pia ni kodi ambayo wamelipa kule kwao. Tanzania kwa rasilimali tuliyonayo tunaweza kujitegemea na inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, mimi naunga mkono hoja na ningeendelea...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara, ajiandae Mheshimiwa Frank Mwakajoka, ninyi mnazo zenu hizo hizo dakika kumi, kumi.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba nijibu hoja ambayo imejitokeza hapa inasema kwa nini hatupongezi.

Kwenye hesabu ya *form five* na *six* au wale ambao mmesoma *Additional Mathematics* kuna *topic* inaitwa *Logic,* yaani kama una *true/false* maana yake ni *false,* kama una *false/ true* unapata ni *false,* kama una *true/true* ni *true.* Sasa sisi hatupongezi wala hatuungi mkono hii bajeti kwa sababu nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kwenye bajeti ya mwaka 2016/2017 Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ilipata fedha asilimia 18 tu, tunapongezaje hapa? Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ni asilimia 3.31, unapongeza nini? Wizara ya Maji na Umwagiliaji ni asilimia 8.4, unapongeza nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmezungumza habari ya madini hapa mnataka sisi tupongeze lakini mikataba hatujaiona, misamaha mliyotoa hatujui, wahusika hawajashughulikiwa, mchanga ndiyo umezuiliwa, dhahabu inaendelea kuzolewa, Wanyamongo pale Tarime wanapigwa wapo ndani wamevunjwavunjwa, tuna makaburi mengi, tuna makovu, kuna watu ambao hawawezi kuzaa kwa sababu wamekunywa sumu madini ya zebaki, tunapongezaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja wapo ya sababu ambazo Mheshimiwa Waziri ametaja ya bajeti kutotekelezwa, ametaja Afrika kwamba uchumi haujakua kwa sababu ya utawala bora, lakini amesahau kwamba sisi watu wa Upinzani, *Wazanzibari wanalia, Uchaguzi wao Maalim Seif alishinda ukafutwa mezani, unataka tupongeze nini hapa au mmesahau?* **[Maneno Haya Sio Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]** *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kule Mawazo Katoro amenyongwa mchana kweupe, alikuwa kijana wetu wa Upinzani, wa CHADEMA, ameuawa katika utawala huu, tunapongeza nini? Tunapozungumza, Ben Saanane hayupo na Serikali haitoi majibu, huyu ni kijana Mtanzania mzalendo, tunapongeza nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, subiri. *Chief Whip.*

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu namba 68(7), napenda nimpe taarifa kwamba tafadhali, jambo ambalo huna ushahidi nalo mkononi usilizungumze kwa sababu unaposema kwamba alishinda unayemtaja, wakati unafahamu kulikuwa na tume zinazohusika na kusimamia uchaguzi, hutendi haki kwa wananchi wa Tanzania, hata kama yale ambayo yalikubalika na mshindi aliyetangazwa wewe binafsi kama humtaki lakini lazima ukubaliane na sheria za nchi. Kwa hiyo, nakuomba ufute maneno yako ya kusema kwamba alishinda huyo unayemsema na badala yake ujielekeze kwenye uchangiaji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, taarifa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kupoteza muda, naomba niendelee.

**MWENYEKITI:** Aah, huo si usemi wa Kibunge, wewe sema tu taarifa yake siipokei.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imepita kama upepo, yaani siipokei, siikubali, ndiyo utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee. Viongozi wa Serikali na Chama Tawala ni muhimu mkawa makini sana...

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** ...yapo matukio ambayo yanatolewa ambayo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, hebu kaa kwanza.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unisamehe sana, na ninatamani sana kuona utulivu wa hotuba zinazoendelea, lakini kama hataweza kuleta uthibitisho naomba afute kauli yake *unless* atuambie analeta uthibitisho na atauleta kwako, kwamba aliyetangazwa hakushinda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Aah, kaa, ngoja.

Jamani, tunafikia mwisho, na mara nyingi Kiti kinapenda amani ndani ya Bunge. Lugha ambazo zinatumika kishabiki ambazo hazitambuliki rasmi, hilo suala la Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Waitara... subirini jamani niseme.

Mheshimiwa Waitara hilo neno la huyo mtu uliyemtaja ameshinda lifute uendelee, kama hutaki kulifuta nikupe muda mpaka Ijumaa ulete uthibitisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waitara, makofi hayo utabaki peke yako, siku zote ninakwambia. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, futa hayo maneno au nikupe muda Ijumaa ulete uthibitisho, mawili tu basi, haina mjadala mwingine. Huu ushabiki wa maneno na makelele achana nao hawa. Sema mimi hayo maneno nayatoa uendelee na mjadala wako.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi nilipewa taarifa sikuombwa nithibitishe, sasa maana yake hii...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, sikiliza Kiti kinavyosema.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye ndiye anayepaswa aseme ukweli ni upi, mimi nimesema hoja, yeye athibitishe mimi yeye alete *counterpart* ya hoja yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, si ndiyo kwa mujibu wa Kanuni?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, hebu kaa kwanza, na Mheshimiwa Mchungaji Msigwa kaa.

Mheshimiwa Waitara, Kiti kinakupa mwongozo wewe futa tu hayo maneno uendelee na mchango wako. Sasa Mheshimiwa Waitara unafundishwa Kanuni huko nyuma utapata matatizo, wewe sema mimi nayatoa haya maneno tuendelee na shughuli.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeyatoa hayo maneno naomba niendelee. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, endelea.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mnafurahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema tu kwamba naomba muda wangu ulindwe. Mnapotaka tujadili kama Taifa, kama Bunge moja ni muhimu pia tukaangalia vipande vipande vya matukio mbalimbali. Kwa mfano mmeteua watu ambao wanaiwakilisha Serikali katika maeneo mbalimbali, lakini tunapozungumza hapa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Hai anazuiliwa kufanya kikao cha

halmashauri, Mstahiki Meya wa Ubungo yupo ndani, amewekwa *lock up.* Tunapozungumza Mkuu wa Wilaya anaongoza wenzake na Jeshi la Polisi ambalo tunalipa kodi kuwapa mishahara na nguo na kila kitu, wanakwenda kuharibu shamba la Mtanzania mmoja amewekeza, Mheshimiwa Mbowe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati mwingine mnaposema tuungane mkono kwa kweli tunashindwa kuwaelewa, haya mambo tunayounganisha, *connectivity,* inakuwaje? Kwa sababu kama mnataka tuungane katika mambo ya msingi, humu ndani kwenye Bunge hili wenzetu akina Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Ester Bulaya wamewajibishwa hapa kwa adhabu kubwa kubwa. Juzi umeombwa mwongozo mtu anaomba mwongozo, Mwenyekiti anasimama anasoma mpaka vifungu, maana yake hilo jambo limeandaliwa limeandikwa. Sasa mnaposema tuunge mkono ni muhimu sana tukubaliane tunataka tufanye kitu gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa nini hatuungi mkono, kwa mfano Mheshimiwa Dkt. Mpango; mjukuu wangu wala sina shida na yeye; Mheshimiwa Dokta Mpango kwenye ukurasa wa 19, watu 7,277 wamefunga biashara zao. Hawa walikuwa wanasomesha, wana wagonjwa, wana watoto, wana kodi wanalipa maana yake zote zime-*paralyze* sasa unaungaje mkono, hili ni jambo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kodi ya majengo, sisi kule Dar es Salaam pamoja na kwamba kuna ufugaji mdogo mdogo, kodi ya majengo tulikuwa tunapata shilingi bilioni 18 kwa mwaka...

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Taarifa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** ...kwenye taarifa hapa, Serikali kupitia *TRA* imekusanya shilingi bilioni 15, Mkoa wa Dar es Salaam peke yake ni shilingi bilioni tisa, unapigaje makofi katika eneo hili? Halmashauri imeondolewa kukusanya kodi, Halmashauri imenyang'anywa... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Subiri, kuna taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe msemaji taarifa kwamba anaponukuu biashara ambazo zimefungwa anatakiwa anukuu na biashara ambazo ziliazishwa kipindi kilekile, hapo ndiyo atakuwa ametenda haki. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Huyu ni Mbunge wa kule Tabora, Wilaya yake ni maskini kweli kweli, kwa hiyo nadhani tutafute hela hapa, yule nimefika kwake Sikonge...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** ...haki ya Mungu hana hata lami yule, acheni kupiga makofi ya kishamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema, mimi naangalia upande wa *negative,* kwamba hawa watu walivyoacha biashara, imewa-*affect,* hii kama wamefungua au wamenufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, nimesema kule kwenye halmashauri hizi Wabunge wanapiga makofi sana...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zima *mic.*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** ...lakini najua hii bajeti ikiisha mwaka ujao kila mtu atakuwa analia na kusaga meno hapa kwa sababu Halmashauri nyingi zinatumia kodi ya majengo, imenyang'anywa...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** ...ilikuwa hata mabango, yamechuliwa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Almas kaa chini.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** ...asilimia tano akina mama na asilimia tano vijana, tunakwenda kuwakopesha nini? Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Mpango lazima aje na utaratibu wa kufanya *replacement* ya fedha ambayo imeondolewa halmashauri ili Halmashauri iweze kujiendesha. Mvua ikinyesha kidogo tu Halmashauri nyingi hazipitiki, hakuna miradi ya maji, tunasema halmashauri. Mheshimiwa Waziri alipoulizwa swali hapa anasema Mbunge ni Diwani aende kwenye Halmashauri wakae wajadiliane, mnajadili nini kama fedha hazipo? Mnajadili nini kama vyanzo vya fedha vimeshanyang'anywa? Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo ni muhimu mkaangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amekuja na hoja, kwenye halmashauri zetu ilikuwa mtu akifanya kosa dogo anapigwa faini shilingi 50,000, imepanda mpaka shilingi 200,000 mpaka 1,000,000, mwaka mmoja mpaka miaka miwili, sasa hawa wananchi wa kawaida ambao ni maskini tunaowatetea tunawatengenezea adhabu kubwa na vifungo. Badala ya kuwaelekeza na kuwafundisha namna ya kufuata sheria tunatunga sheria za kwenda kuwakandamiza wakafungwe zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema Machinga waende wakajiandikishe, ni jambo zuri zaidi, lakini eti ambaye hakujiandikisha atafungwa sasa *mechanism* ikoje kuwatambua hawa watu? Nani anafanya utaratibu huo ili akwame? Nadhani tungeelekeza nguvu kufundisha watu wetu na kuwaelekeza kufuata sheria, tusiende sana kwenye adhabu mbalimbali ambazo zinakwenda kuumiza watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii bajeti Mheshimiwa Waziri hatuungi mkono kwa sababu gani, mlikujaa na bajeti ya shilingi trilioni 29 ya mwaka jana imekamilika kwa asilimia 38 tu. Umeongeza sasa unazungumza shilingi trilioni 31.4 haujaeleza ni miujiza gani itatumika fedha hii ipatikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anakaa kule Zingiziwa kwangu kule Ukonga, unafahamu mvua imenyesha kwako huwezi kwenda kuna mahandaki, hakuna maji, nimenunua mpaka jenereta kule Zingiziwa shule ya Msingi kule ni Dar es salaam sasa kule kwenu kule Buyungu, Kakonko ikoje hali hiyo? Haya mambo ukiyalinganisha huwezi kupiga makofi humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnataka tujadili kama Taifa ni muhimu sana tukubaliane, mnavyotenda mtende kwa Watanzania wenzenu sawa sawa mnavyotendewa nyie, tuheshimiane. Kwanza utaratibu wa kuonyesha kwamba eti mtu akishakuwa mpinzani siyo Mtanzania sio sawa sawa. Hauwezi kutudharau kwenye mikutano, mkatunyima nafasi, *tv* mnatumia mnavyotaka nyie, inakua Chama tawala halafu tukija hapa tupige makofi. Mkiboresha mambo hayo sisi hatuna shida na ninyi na hakuna mtu ambaye anasema tuibiwe, sisi huwa tunapinga kuliko ninyi kwamba wizi mwiko. Leteni mikataba, Twiga walioibiwa, tubadilishe sheria, watu wanyongwe, watu wafilisiwe; na uzuri wa Mungu wote watakuwa Chama cha Mapinduzi hakuna mpinzani hata mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo vipi? Nakushukuru sana, siungi mkono hoja, ahsanteni sana *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kwa kupata fursa hii ya kuweza kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niseme tu ninaunga mkono maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Pia nitumie fursa hii kuwashukuru sana viongozi wangu Mheshimiwa Mbowe pamoja na viongozi wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa jinsi ambavyo wameendelea kutuongoza vizuri kuhakikisha kwamba tunaishauri Serikali na tunaisimamia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie fursa hii kuanza kusikitika sana kwa sababu ya tukio la Mkuu wa Wilaya

ya Hai kuongoza Mgambo katika Wilaya ya Hai na kwenda kuharibu Mashamba makubwa ambayo yana zaidi ya bilioni kwenye *green house* ya Mheshimiwa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). Tuna uhakika kabisa kwamba haya ni masuala ya kisiasa ambayo yamefanyika; na kwa sababu Mheshimiwa Mbowe alikuwa ameamua kuwekeza kwenye kilimo kama mwekezaji mwingine katika nchi hii lakini tumeona hakuna taarifa yeyote wala kemeo lolote la Serikali kwa Mkuu wa Wilaya ambaye amekwenda kuharibu mashamba haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linasikitisha sana, na leo katika Bunge hili tunazungumza kwamba tunataka utengamano wa kisiasa. Utengamano wa kisiasa hauwezi kuja kwa sababu kuna uonevu, kuna husda ambazo zinaendelea ndani ya nchi hii. Tumesikia baadhi ya viongozi wetu wanaendelea kuwekwa ndani. Jambo hili linaendelea kututengenisha na hatutaweza kuwa pamoja kwa sababu viongozi walioko madarakani wameshindwa kutuweka pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nijaribu kuzungumzia jambo lingine. Ninataka kuzungumza kwamba bajeti hii ya Mheshimiwa Mpango na niseme kwamba Mheshimiwa Mpango ndiye tatizo katika Taifa hili. Mheshimiwa Mpango kama Waziri wa Fedha ndiye anayelirudisha Taifa hili nyuma. Mimi nimeshangaa sana wakati anasoma bajeti yake hapa watu wamempigia makofi na anasoma kwa mbwembwe kali, lakini ukiangalia utekelezaji wa bajeti yake ya mwaka 2016/2017 unaona ametekeleza kwa asilimia 38. Kama nchi hii kungekuwa kuna uwajibikaji, Mheshimiwa Mpango angeshakuwa a meshaachia madaraka kwa muda mrefu asingeonekana katika Bunge hili la bajeti ambalo linaendelea. Hata Mawaziri wengine walioweza kuwasilisha bajeti zao wasingeweza kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijaribu kuangalia Serikali hii inasema kwamba inataka kupunguza umaskini wa Watanzania. Umaskini wa Watanzania hauwezi kupungua kwa sababu ya kununua Bombadier, umaskini wa

Watanzania utapungua kwa sababu ya kuwahudumia Watanzania wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kutoa mfano; asilimia 75 ya Watanzania ni wakulima katika nchi hii na asilimia 80 ni masikini; na kati ya asilimia 80 maskini hawa wanapatikana katika asilimia 75 ya Watanzania ambao ni wakulima, wavuvi na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo katika bajeti ya mwaka 2016/2017 katika Serikali ya Chama cha Mapinduzi tuliwaambia bajeti hii hamtaiweza kuitekeleza mkasema mtaitekeleza, hebu angalia, kwenye kilimo tulikuwa tumetenga shilingi bilioni 101 lakini utekelezaji na fedha zilizokwenda kuinua kilimo ili kuhakikisha kwamba viwanda vinakua katika nchi hii na umasikini unaondoka kwa Watanzania asilimia 75 imepelekwa shilingi bilioni tatu tu kati ya shilingi bilioni 101. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuliamua kwamba tuendeleze pia kilimo cha umwagiliaji. Huwezi kuamini katika kilimo cha umwagiliaji tulikuwa tumetenga shilingi bilioni 35 kati ya shilingi bilioni 35 fedha iliyokwenda kwenye shughuli za maendeleo ni shilingi bilioni 1.2 ambayo ni sawa ya asilimia nane ya fedha ambazo zilikuwa zimetengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linaendelea kuonesha ni jinsi gani ambavyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi haijajiandaa katika kuondoa umaskini wa Watanzania. Na ninataka kusema Watanzania hawataweza kuondolewa umasikini wao kwa sababu ya Bombadier wala hawataweza kuondolewa umaskini wao kwa sabau ya *standard gauge.* Ni lazima tuwekeze kwa wafugaji, kwa wakulima na kwa wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi ndani ya Bunge hili wanafika mahali wanashangilia wanasema bajeti ya mwaka, bajeti ya msimu, bajeti haijawahi kutokea, wananchi wenu maskini, wakulima

wako vijijini hawajapelekewa fedha kule mnasema bajeti ya mwaka ambayo haijawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwakumbushe ndugu zangu Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, mwaka 2015/2016 wakati wa uongozi wa Mheshimiwa Kikwete alitenga shilingi bilioni 88 kwa ajili ya wakulima, hizo ni pembejeo peke yake leo mnatenga shilingi bilioni 10 mnasema hii ni bajeti ya mwaka haijawahi kutokea, haya ni mambo ya ajabu sana, mnaongoza watu gani? Sisi tunakaa mjini kwa wafanya biashara, pale Tunduma ni mjini lakini tunaendelea kuwatetea wakulima ili kuhakikisha kwamba maisha ya wakulima yanainuka na yanapanda juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mnasema kwamba mnataka kuanzisha viwanda. Kwenye viwanda peke yake ilikuwa imetengwa shilingi bilioni 42 lakini kati ya shilingi bilioni 42 fedha ambayo imekwenda kwenye viwanda ambayo Mwijage ameipokea ni shilingi bilioni 7.6 peke yake. Leo mnasema Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba nchi inakuwa ni ya viwanda, huu ni ubabaishaji na ni utani kwa Watanzania. Nchi hii hamjajipanga kuanzisha viwanda na hamko tayari kuanzisha viwanda. Msifikiri viwanda vinakuja kwa maneno, msifikiri viwanda vinakuja kwa maigizo yanayofanyika ndani ya Bunge hili. Viwanda vitakuja kwa vitendo, kwa kutenga fedha na kuhakikisha kwamba fedha zinakwenda kwenye matumizi na zinakwenda kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kusema kwamba ni lazima tubadilishe mtazamio wetu. Tumefika humu ndani kila wakati ndiyoo, ndiyoo, ndiyoo! Hamjasema ni namna gani mtabadilisha maisha ya Watanzania. Tunataka maisha ya Watanzania yaweze kubadilika kwa vitendo, mnafanya usanii ndani ya nchi wakati mmepewa madaraka makubwa ya kuongoza nchi hii. Kwa nini mfanye usanii na maisha ya Watanzania? Haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti iliyotekelezwa mwaka 2016/2017 mmetekeleza asilimia 38, leo hii mmetenga bajeti

shilingi trilioni 31 wakati shilingi trilioni 29 mmeshindwa kutekeleza, haya ni maajabu makubwa ambayo yanaonekana katika nchi hii. Tunataka mabadiliko katika Taifa hili, na mabadiliko haya kama mtaendelea kucheka namna hii Watanzania mliowaona miaka iliyopita ya 2000 si Watanzania wa sasa hivi na ndiyo maana mnaona kura zenu zinazidi kushuka kwa sababu ya kutowatekelezea yale wanayohitaji Watanzania, na lazima mtang'oka tu. Endeeni kupiga ngonjera humu, endeleeni kushangiliana, endeleeni kusema kwamba ndiyo mzee, tutawakuta humu mnaendelea kusua sua, tutawang'oa katika viti vyenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine nililoshangaa, Mheshimiwa Mpango eti kuanzisha vyanzo vipya amekwenda kuwaorodhesha Wamachinga, wauza ndizi, wauza mbogamboga eti wajiorodheshe wakishajiorodhesha, wakitambulika waanze kulipa kodi, hii nchi iko namna gani? Haijaweka mipango thabiti ya kuwajengea uwezo wafanyabiashara wadogo ili wawe na mitaji mikubwa na baadae waje wawe wafanyabiashara wakubwa, lini Mmachinga kalipa kodi? Hii itakuwa ni nchi ya kwanza katika dunia hii Mmachinga kumlipisha kodi, itakuwa ni nchi ya kwanza mtu ambaye anauza mbogamboga na matunda kulipishwa kodi katika nchi hii. Ni lazima tufike mahali tufikirie mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mpango hata Buhigwe kule wananchi wameshatoa imani kwako kwa sababu inaonesha wale wanaotumia vibatari umewawekea pia ushuru, wanalipa kodi katika Taifa hili leo unataka wananchi wa Buhigwe wakuamini kwanza unaweza kuwa Mbunge wa Buhigwe, haitawezekana kabisa. Wewe ndiwe unayeshindwa kumshauri Mheshimiwa Rais, unalirudisha Taifa nyuma na ni lazima tufike mahali tukwambie, tuiambie Serikali kwamba imeshindwa kutekeleza wajibu wako sawa sawa ili kuhakikisha kwamba...

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Frank subiri.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji anayezungumza. Anasema kwamba kule Buhigwe Mheshimiwa Mpango wanasema kwamba hawamtaki, naomba niseme hivi; Mkoa wa Kigoma wamefurahia sana kwa ile *road license* aliyoitoa na kila mara tunapokea taarifa ya kumpongeza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Frank taarifa!

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei taarifa yake kwa sababu najua anajikosha, sasa hivi ana adhabu ya mwaka mmoja ndani ya Chama cha Mapinduzi, kwa hiyo, anaendelea kuipunguzia punguzia makali, kwa hiyo, siipokei kabisa taarifa yake huyu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumza tu kwamba liko suala lingine, kuna suala linalozungumzwa sasa katika Bunge hili. Wakati watu wanaendelea kujadili bajeti limekuja jambo la mchanga wa madini kwenye nchi hii. Ni vizuri Serikali ya Chama cha Mapinduzi pia ikakumbuka jinsi Wabunge wetu walivyopiga kelele ndani ya Bunge hili, wakakumbuka ni jinsi gani Wabunge wetu walivyoshauri Bunge hili kwamba ndugu zangu tunaibiwa, lazima tufike mahali tubadilishe mikataba hii, mikataba ni mibovu, ni mikataba ya kifisadi, wakasema hapana ni lazima mikataba hii ipite.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mlishangilia kama mlivyokuwa mnashangilia hapa, leo nashangaa mnatuona sisi ni wachawi katika Bunge hili. Sisi si wachawi, wachawi ni ninyi ambao tayari milipitisha mikataba na Watanzania.

Wachawi ni ninyi kwasababu mlipitisha mikataba hii, tena mikataba ya kifisadi ambayo Watanzania wamepoteza fedha nyingi sana, wameingia hasara...

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo nataka niseme...

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Frank kaa chini, taarifa.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa, unajua kuna watu wengine mitaani wanakuwa mambumbumbu sana. mikataba haipitishwi Bungeni aelewe, ni taarifa hiyo tu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya endelea.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona ana matatizo yake binafsi, hiyo lugha, na yeye ndiye Mbumbumbu pale. Mimi niko vizuri na ninajitambua na ndiyo maana niko Bungeni humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema mikataba haipitishwi humu, tuliishauri Serikali ilete mikataba Wabunge wetu waipitie, wajaribu kuishauri Serikali mikataba iko vizuri au haiko vizuri mkasema hapana, leo nyie wenyewe mnasema mikataba italetwa humu, inaletwa kuja kufanya nini? Inakuja kufanya nini? Mnaleta wakati watu wameshakula imebaki mifupa ndiyo mnatuletea mikataba hapa? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Sheria.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka kusema ni kwamba ni lazima tufike mahali tukubaliane, Wabunge wetu walifanya kazi ya ziada

kuishauri Serikali, kwamba mikataba hii ni mibovu mkasema mikataba ni mizuri, mkagonga meza, wakasema sheria hizi ni mbovu, mkasema hapana. Zikaletwa hati za dharura hapa mkapitisha sheria tatu hapa kwa haraka haraka, kwa mkupuo siku moja, lakini mnataka kuniambia kwamba eti Chenge ana matatizo, sijui Ngeleja ana matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimshitaki Mwanasheria Mkuu wa Serikali tafsiri yake umeshitaki Serikali ya kipindi kilichopita, ndiyo tafsiri yake. Mwanasheria Mkuu wa Serikali hafanyi kazi kwa jina lake kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali, anafanya kazi kwa mujibu wa maagizo ya Mheshimiwa Rais pamoja na viongozi wake walioko juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo kama mtatuambia kwamba hawa watu ambao wanatajwa, Mawaziri, sijui Mwanasheria Mkuu wa Serikali anakwenda kujibu kwa nini alisaini, mimi nina uhakika kabisa hata Mzee Masaju hapa hawezi kusaini mkataba kama Mheshimiwa Rais hajamwambia asaini mkataba, lakini je, akisaini huo mkataba kesho tuje tumwambie Masaju mkataba huu ulikwenda vibaya kwa hiyo tunakufungulia mashitaka? Hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mwanasheria Mkuu atakuwa amefanya makosa haya ni makosa ya Serikali nzima ya Chama cha Mapinduzi kwa kipindi hicho kwahiyo kama ni kuwajibika Serikali nzima ya Chama cha Mapinduzi ndiyo inatakiwa kuwajibika kwa jambo hili ambalo limejitokeza. Kwa maana hiyo waombeni msamaha, msijibaraguze kwamba mnawa... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kiula, ujiandae Mheshimiwa King.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi kwa kuweza kupata nafasi kuchangia

katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Cha kwanza kabisa naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri, pili naunga mkono juhudi zinazofanywa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli za kuiongoza nchi hii kwa umakini kabisa na kwa uhodari mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nilitaka kuweka jambo moja sawa kwamba bajeti inakua, bajeti haiwezi kusimama hapo hapo, bajeti lazima ikue. Ili bajeti iweze kukua kuna mikakati ambayo inakua imewekwa. Kwa mfano tumeweka mazingira mazuri ya kujenga viwanda, na viwanda vinajengwa na wadau mbalimbali Serikali haijengi viwanda. Vilevile mmeona tunatengeneza miundombinu, miundombinu ikikaa sawa ina uhusiano wa moja kwa moja. Tumegusa suala la kilimo, kilimo pia kitasaidia kuleta malighafi katika viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie suala lingine la kusema kwamba CCM itaondoka madarakani, lakini siku chache zilizopita TWAWEZA wametoa takwimu hapa, wameonesha nani anapanda, nani anashuka. Mimi sipendi kuingia huko lakini TWAWEZA wameweza kutuonesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia suala zima la bajeti sasa katika mchango wangu, bajeti ni shilingi trilioni 31, lakini kodi ni shilingi milioni 17 na *tax revenue* shilingi trilioni mbili na madeni ni shilingi trilioni 11 ndipo tunafika kwenye shilingi trilioni 31 maana yake nini? maana yake ni lazima tuangalie vyanzo vipya vya mapato. Na vyanzo vipywa vya mapato vya haraka haraka lazima *informal sector, World Development Report* ya mwaka 2017 inazungumza kwamba katika nchi zinazoendelea, *informal sector* ina-*constitute* karibu asilimia 40; sasa lazima tuangalie hiyo *informal sector* tutaileta vipi kwenye *net* ya kulipa kodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo machache ambayo pia yanatakiwa yaangaliwe, *consultancy*. Watu wanafanya *consultancy* lakini hawalipi kodi, lakini kuna watu wanafanya kazi mbili/mbili hawalipi kodi lakini pia Rais

amesema mikataba itakuja ya madini, mikataba ya madini ikija itaongeza kipato, na hiyo inajibu hoja ya kusema hatukuweza kukusanya vya kutosha, hatuku-*perform* vizuri. Pesa zinakuja, pesa zikija tutaweza kugharamia bajeti yetu bila tatizo lolote lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo lazima sote na Waziri atambue kwamba tumeweka mpango na lazima pesa zipatikane, kwa hiyo, pesa zitapatikana kwa kuweka mikakati mizuri na pesa zikipatikana mimi nina uhakika kabisa hata Jimbo langu la Mkalama Daraja la Sibiti litakamilika, barabara zitakamilika, huduma ya afya itakuwa sawa na maji watu watakunywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *motor vehicle.* Tumeondoa *motor vehicle,* tumeweka utaratibu huo mzuri wa shilingi 40. Hiyo shilingi 40 tupige hesabu tuone kwamba tulitakiwa tukusanye pesa ngapi kama tusingeondoa *motor vehicle.* Kwa hiyo pesa iliyozidi ambayo mimi nimepiga hesabu hiyo pesa imezidi imepelekwe kwenye maji iwe *refenced*, ichangie kwenye mfuko wa maji itakuwa ni jambo zuri.

Niende kwenye suala la madini. Tumezungumzia suala la *gypsum* nazungumza suala la *gypsum* kwa sababu kule kwangu Dominiki *gypsum* ipo. Nashukuru Serikali kwa kuona viwanda vya ndani kutumia *gypsum* ya hapa kwetu, lakini basi uwekwe utaratibu mzuri wananchi wawezeshwe. Hiyo *gypsum* mimi niliangalia haina utaalam sana wa kuchimba, kwa hiyo, kama Wizara ya Madini na Nishati itawawezesha wananchi kuweza kuchimba hiyo *gypsum* wenyewe na masoko ambayo tunayajua wananchi watanufaika. Pia wale maofisa wa madini wanatoa leseni tu wananchi wanakwenda kuondolewa bila utaratibu wowote, hilo jambo liangaliwe na huko wananchi wanaweza kunufaika na madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao chini ya tani moja. Tumesema kwamba mazao chini ya tani moja yasilipiwe ushuru wowote. Hapa yako mambo mawili, kwanza

tunaipongeza Serikali kwa hatua hiyo lakini tutambue kwamba wako wafanyabiashara wajanja, walanguzi ambao wanaweza wakatumia mwanya huo kupoteza mapato hayo. Sasa viwekwe vituo vya kuuzia mazao, kwa hiyo, Halmashauri wapewe leseni za kununua mazao kwenye vituo maalum tusiruhusu walanguzi kuingia kwa wananchi na yenyewe itakuwa ni jambo litakalosaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tujue kwamba sasa Halmashauri zitapoteza mapato, kwa hiyo tukadirie tuone kwamba mapato yatapotea kiasi gani na tuone hizi Halmashauri zitafidiwa kiasi gani. Kwa mfano, sisi Mkalama zile *own source* kubwa zinategemea hizi kodi........

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Aweso, jiandae Mheshimiwa King. Hapana King kwanza halafu Aweso.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza mimi ilikua nianze kwa neno moja ambalo ni maarufu sana ambalo hizi hoja zote zinazozungumzwa zinaingia katika *al-jununu fununu* (uendawazimu una matawi mengi sana), lakini akili fani yake moja tu; leo wako wengine wanaotaka kupongeza huko, wako wengine hawataki, wako wengine wanasema wasishurutishwe, wako wengine wanatakiwa wasilaumiwe sasa mko wapi wenzetu? Hizo ni fani za wendawazimu zote, lakini CCM ni fani moja tu, sisi tunapongeza kwa Rais kitendo alichokifanya, kwa hiyo, ninyi msipopongeza ni kazi kwenu kwasababu *al-jununu fununu* (wendawazimu una matawi mengi) kwahiyo gawaneni hayo matawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watakaodandia la kupongeza, watakaodandia la kusema kwamba lawama, endeleeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine msiseme uongo, mnasema mnafanya *research* ninyi? Mnasema

kwamba bajeti inatakelezwa kwa asilimia 38, ni bajeti ipi? unaijua bajeti? Kuna bajeti ya maendeleo, kuna bajeti yenyewe kuu mnazungumza nini? mnasema mmefanya research hao waliowafanyieni *research* ni wakaotaji kuni wa usiku wamewafungieni na nyoka humo humo. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawajui, hakuna jambo la maana ambalo wameeleza. Tazama bajeti pesa zilizotoka, halafu ukaangalie maendeleo...

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

## TAARIFA

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa King taarifa. Mheshimiwa King subiri.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge anaendelea kuzungumza hajui kwamba anawazungumza kuhusu wandawazimu ni Wabunge wenzake na wana heshima zao. Kwa hiyo, anatumia lugha ambayo ni matusi, ya kuudhi, ambayo asingefaa kutumia. Kwa hiyo, naomba ajizuie katika kufanya matusi, kwa sababu haisaidii Bunge, anajivunjia heshima yake tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa King endelea!

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hafahamu kidogo *al jununu* maana yake ni uwendawazimu una matawi mengi, kwa hiyo wewe tena utajijua kama upo kama tawi la uwandawazimu utakuwa mwendawazimu. Sasa tunasema hivyo ndivyo bajeti inavyotekelezwa. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Hebu nipeni raha, utaratibu gani tena...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, hebu kaa chini kaa, kaa.

Waheshimiwa Wabunge, tuna mjadala muhimu sana hapa, tujaribu kuzungumza lugha za Kibunge na tuwe na staha ndani ya Bunge, tuwe na maneno ya kistaha kwa pande zote. Sitaruhusu sasa ku-*interrupted* kwenye taarifa. Endelea Mheshimiwa King.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nilindie muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kimezungumzwa kitu ambacho hakihusiani kabisa, kumezungumziwa uchaguzi wa Zanzibar. Sawa, tarehe 25 Oktoba, kulikuwa na *NEC* kuna *ZEC* hata kuku wanataga mayai na mayai mengine yakawa viza. Kwa hiyo, uchaguzi ule kwa Wanzanzibar kule *ZEC* ulikuwa ni viza, na kitu viza huwa si riziki. Naogopa kusema kwamba na aliochaguliwa labda ilikuwa si riziki maana hakupata. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nizungumzie jambo moja kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kuhusu takwimu za viwanda. Tunaelekea katika nchi ya viwanda lakini bado tunategemea takwimu kutoka katika taasisi binafsi. Takwimu kutoka katika taasisi binafsi haziwezi kutusaidia kwa sababu kila mmoja ana takwimu zake. Tunacho kitengo chetu cha takwimu za Serikali, kwa nini tusitumie katika kufikia katika *Fiscal Policy* zetu? Tutumie kitengo hicho cha Serikali, namshauri Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na lingine kwa Zanzibar kuna *VAT* ambayo ilianzishwa mwaka jana ya *Section 55(a)* ambayo bidhaa za kutoka Bara kwenda Zanzibar na zinazozalishwa Zanzibar kuja Bara zilikuwa zimewekewa *zero rated.* Lakini *zero rated* hiyo wako watu ambayo ni *registered VAT* na wengine hawakuwa *registered*, hawa ambao hawako *registered* hawatambuliwi, kwa hiyo, wanalipishwa *VAT* mbili

analipishwa na *TRA* analipishwa pia na *ZRB*. Kwa hiyo hapa tuangalie, tusiweke double standard tukiweka *double standard* tutumie *destination principles* kwa wote, tuwatambue kwa vitambulisho ambavyo wanavyo ili tuwasaidie wafanyabiashara hawa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nizungumzie utalii. Ili kuweza kukuza mapato yetu na Pato la Taifa liweze kukua, tuna vivutio vikubwa vya utalii katika Tanzania. Tanzania kwenye dunia ni nchi ya pili kwa kuwa na vivutio vizuri baada ya Brazil. Kwa hiyo, tukitumia vivutio hivi vya utalii tunaweza tukaja tukafikia mahali pazuri ili Tanzania yetu nayo iweze kung'ara na tuweze kupata mapato mazuri katika nchi yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji wa Kambi ya Upinzani katika *introduction* yake alitaja msemo mmoja ambao aliuzungumza Baba Nelson Mandela. Nelson Mandela amesema *no easy walk to freedom* kwamba hakuna *easy walk* katika kuuendea uhuru, lakini wenzetu wanataka uhuru upi? Wale waliofanya hivyo anawatetea ni watovu wa adabu ambao Bunge hili liliwapa adhabu. Sasa wao wanawatetea Waheshimiwa watatu ambao walipewa adhabu hapa kutokana na utovu wa adabu. Kwa hiyo wanawasema hapa kwamba *no easy walk to freedom* kwamba je wanataka uhuru wa kutukana humu ndani? Wanataka uhuru wa kutovuka adabu humu ndani? Wanataka uhuru wa kutokusikiliza kitu humu ndani? Kwa hiyo, hicho sio kitu kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunazungumzia katika upande huo huo, kuna watu walisema kwamba bajeti...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Aweso, ajiandae Mheshimiwa Hassan Masala.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMAA H. AWESO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia bajeti iliyokuwa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza naomba nimpongeze Dkt. Mpango kwa namna ya mpango wa bajeti alivyoipanga imepangika kweli kweli, bajeti ipo bomba. Nataka nimwambie Mheshimiwa Mpango wali wa kushiba siku zote unaonekana kwenye sahani. Na naunga mkono kama mimi Mbunge kijana kwa sababu bajeti hii imeenda kujibu matatizo ya wakulima, imeenda kujibu matatizo ya wafugaji, lakini pia imeenda kujibu matatizo ya wavuvi. Ni watu wenye sifa tu ya miembe ndio wanaweza wakapinga bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupinga si dhambi na ni jambo jema, lakini si kupinga kila kitu. Na ukisoma aya za Qurani Mwenyezi Mungu anasema; *"waama bi neemati Rabbikka fahadith"* (zielezeeni neema za Mwenyezi Mungu kwa kushukuru). Watanzania tulikuwa tunamuomba Rais ambaye ataweza kuleta maendeleo katika taifa letu. Unaweza pia usijue kusoma, lakini pia picha ukashindwa kuiona? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu Wabunge tutapata laana kubwa kwa Mwenyezi Mungu kama tutampinga Mheshimwia Rais Dkt. John Pombe Magufuli. Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli ni jembe tena limekuja wakati mwafaka. Tulitumie ili tuhakikishe kwamba tunaenda kulima na kupanda kwa uhakika katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika Jimbo langu la Pangani tulikuwa na mabadiliko ya tabianchi bahari inakula Mji wa Pangani, lakini kwa muda mfupi leo tunatengenezewa ukuta wa bahari. Kulikuwa na maeneo

ambayo hayajawahi kuona umeme leo wanapata umeme. Mungu atupe nini atupe gunia la chawa tujikune? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali, bajeti ni nzuri lakini naomba nishauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara ni kichocheo kikubwa cha maendeleo katika Taifa. Lakini pia inaweza kuchochea ajira katika maeneo katika jamii yetu na hata katika kuboresha huduma za kijamii. Tunaona maeneo mbalimbali ambayo yalikuwa hayana barabara leo yamepatiwa barabara maendeleo yake ni makubwa. Niombe fedha zilizotengwa katika bajeti hii ili kuhakikisha kwamba zinafika kwa haraka ili miundombinu ya barabara katika maeneo mbalimbali ya Taifa letu iboreshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano katika Jimbo langu la Pangani tulikuwa na changamoto ya barabara, lakini katika bajeti hii tumetengewa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi. Naiomba Serikali fedha zile ziende ili kuhakikisha kwamba barabara ya Tanga - Pangani - Saadani inajengwa ili wananchi wangu wa Pangani waweze kupata maendeleo kwa kasi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la pili, ni suala zima la upatikanaji wa maji. Nchi yetu ina vyanzo vingi vya maji lakini maeneo mengi bado kumekuwa na tatizo la maji. Naomba niseme anayelala na mgonjwa ndiye anayejua mihemo ya mgonjwa. Sisi katika Jimbo la Pangani bado tunakuwa na changamoto kubwa ya maji. Tuna Mto Pangani ambao unapita katikati ya mji lakini bado wananchi wangu wanatatizo la maji. Niombe bajeti hii iende ikatatue tatizo la maji kwa wananchi wa Pangani ili twende kuwatua ndoo wananchi wale wa Pangani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina maneno mengi sana ya kusema, lakini kubwa kwa kumalizia nataka nizungumze tunapozungumzia uchumi wa viwanda lazima tuangalie afya za watu wetu. Hauwezi ukalima, hauwezi ukazalisha

pasipokuwa na afya. Tunaona maeneo mbalimbali bado kumekuwa na changamoto ya vituo vya afya, na hata Zahanati. Niombe Serikali katika bajeti hii kuhakikisha kwamba inatenga fedha hizo zifike kwa haraka ili kuhakikisha kwamba vituo vya afya na zahanati vinajengwa na vifaa tiba vinapatikana ili wananchi wetu waweze kupata maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ahsante sana na Mwenyezi Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Hassan Masalla, ajiandae Mheshimiwa Mhagama.

**MHE. JUMAA H. AWESO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti hii. Naomba niungane na wenzangu waliopita, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, lakini pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuwafanyia Watanzania, ya kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nijielekeze katika maeneo makubwa manne. Eneo la kwanza ambalo nilitaka nichangie ni eneo la kilimo. Kwa niaba ya wananchi ambao nawawakilisha naomba nifikishe salamu zao za pongezi kwa kilio cha muda mrefu cha kuwaondolea adha kubwa ya tozo katika zao kubwa ambalo linatuletea uchumi mkubwa katika maeneo yetu, zao la korosho. Kwa muda mrefu tumekuwa tunalalamikia tozo nyingi ambazo zilikuwa zinapunguza bei ya korosho, lakini kwa sasa kupitia Rais wetu wakulima wa zao la korosho wamenufaika kwa kiasi kikubwa. Ndani ya Wilaya ya Nachingwea, Liwale na Ruangwa kwa mwaka huu peke yake si chini ya shilingi bilioni 46 zimeingia katika mzunguko wa fedha za wakulima. Hii ni kazi kubwa ambayo imefanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hilo, naomba nizungumzie nakupongeza pia suala zima la kutoa pembejeo bure, *sulfur* pamoja na madawa mengine ili kuweza kukuza zao hili la korosho. Changamoto kubwa ambayo nilitaka nishauri kupitia kwa Waziri wa Kilimo na Wizara kwa ujumla ni suala zima la kuangalia pembejeo hizi zinapatikana kwa wakati gani. Mpaka sasa hivi ninapozungumza tayari wakulima wanahitaji kuona pembejeo zimeshawafikia, lakini bado kuna baadhi ya maeneo pembejeo kwa maana ya *sulfur* mikorosho imeshaanza kutoa maua bado *sulfur* haijafika. Kwa hiyo, niombe haraka iwezekenavyo Wizara ipeleke *sulfur* katika maeneo ya mikoa ya Lindi, Mtwara, ili wakulima waweze kupulizia mikorosho yao tuweze kuuwahi msimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kutoa *sulfur* bure bado kuna changamoto ya uchache wa *sulfur* hii ambayo inaenda kutolewa kwa wakulima. Mpaka sasa hivi nazungumza kwa Wilaya ya Nachingwea peke yake ina mgao wa tani 1300, kwa idadi ya wakulima na uzalishaji wa Wilaya ya Nachingwea peke yake idadi hii ya pembejeo ambayo tunaenda kupata ni ndogo na haiwezi kukidhi mahitaji. Kwa hiyo naomba Wizara naomba Serikali iongeze idadi ya mgao ili wakulima wengi waweze kupata *sulfur* na pembejeo za kutosha ili waweze kuhudumia mikorosho yao tuweze kuingia katika Kilimo kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ambalo nilitaka nizungumze ni suala zima la maboresho ambayo tungependa yafanyike pia ili kumnufaisha mkulima. Tunahitaji tuone utekelezaji wa kuanza kazi kwa bodi ya mazao mchanganyiko. Ukiondoa korosho ambayo inatuletea uchumi mkubwa, bado tuna mazao ya mbaazi, tuna mazao ya choroko, lakini pia tuna mazao ya ufuta ambayo muda si mrefu tunaenda kuingia kwenye msimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu tumepigia kelele kuona bodi hii inafanya kazi lakini mpaka sasa hivi bado Serikali imekuwa na kigugumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Wizara, naomba nishauri Serikali ione umuhimu wa Bodi ya Mazo mchanganyiko iweze kufanya kazi kuanzia mwaka huu ili iweze kusimamia bei ya wakulima wetu katika haya mazao mengine ambayo wakulima wetu wameitikia wito wa kulima kwa nguvu na kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo ningependa nizungumzie, unapozungumza uchumi na unapozungumza kuiunganisha Tanzania, unapozungumza suala la viwanda, huwezi kusahau suala zima la umeme. Bado mikoa yetu ya Lindi na Mtwara ina matatizo makubwa ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo tunazungumza, Serikali imeonyesha nia ya kujenga kituo pale Mnazi Mmoja. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atuambie wametenga kiasi gani na wana nia gani ya kwenda kuhakikisha mitambo ile inaanza kufanya kazi ili wananchi wa kule waweze kupata umeme wa uhakika, ambao wataweza kuzalisha kwa ufanisi na kutosimamisha shughuli za maendeleo ambazo mpaka sasa imekuwa ni kitendawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ambalo nilitaka nizungumzie ni suala zima la barabara. Nimepiga kelele toka mwaka jana, nimepiga kelele mwaka huu. Kwenye bajeti ya mwaka huu ya Wizara tumeahidiwa kutengewa bilioni tatu; lakini bado ningependa kuona Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha, kwa uchumi ambao mikoa hii inazalisha, tungependa kuona barabara ya Masasi - Nachingwea na Nganga, lakini pia sasa hivi tunazungumzia barabara ya Ruangwa, fedha hii ambayo imeahidiwa inaenda kupatikana kwenye fungu gani na lini fedha hii inaenda kutoka ili tuanze ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, ambayo nayo imekuwa ni kikwazo kikubwa cha maendeleo katika ukanda huu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo naomba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mhagama, ajiandae Mheshimiwa Mabula.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wote, wanaompongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri sana anayoifanya kwa Watanzania.

Pili, nipongeze sana Serikali kwa kuleta mpango huu na bajeti hii ya mwaka 2017/2018. Ni bajeti ya kipekee sana ambayo inagusa maeneo yote makubwa ambayo kama ya tatekelezwa vizuri, yatawatoa Watanzania na kuwafikisha kwenye uchumi wa kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maslahi ya muda, kwanza niishukuru sana Serikali hii ya Awamu ya Tano kwa kuitazama kwa namna ya pekee sana Halmashauri yetu ya Wilaya ya Madaba na Jimbo la Madaba. Kimsingi kushukuru ni kuomba tena, wana Madaba katika kipindi hiki cha mwaka mmoja, tumeona maendeleo makubwa sana katika maeneo mbalimbali ikiwemo afya, maji, nishati na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri na Wizara zenu, lakini zaidi Mheshimiwa Rais ambaye amewakabidhi haya majukumu. Wana Madaba tunatambua mchango mkubwa wa Serikali kwa maendeleo yetu na ninaamini tutaendelea kutoa ushirikiano kwa Serikali hii kwa sababu tunaamini ndani ya kipindi cha miaka mitano wana Madaba tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango mkubwa ambao nilitaka niutoe kwako na kwa Wabunge leo hasa kwa Serikali, ni mahusiano ya kilimo na Tanzania ya viwanda. Kwa

Muktadha wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2015/2020. Ukitazama katika Ilani yetu, kipaumbele cha Awamu ya Tano ni kuwa na viwanda Tanzania nzima ili kutoa ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sehemu kubwa Serikali imeweka misingi imara ya kutengeneza au yakujenga Tanzania ya viwanda. Miaka miwili tu baada ya kuanza Serikali hii au mwaka mmoja na nusu, tayari tunaona viwanda vingi vinajengwa. Hata hivyo ninaomba niikumbushe Wizara na niikumbushe Serikali kwamba aina ya viwanda vinavyojengwa, pamoja na kwamba ni viwanda vizuri, lakini aina hii bado haiendi kujibu kwa namna inavyotakiwa mahitaji makubwa ya Watanzania wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Chama cha Mapinduzi, inatutaka aina ya viwanda ambavyo vinatakiwa tuvijenge sana ni vile ambavyo vitaongeza thamani ya mazao yetu na hivi kutoa soko na kuongeza kipato kwa mwananchi mkulima.

Tukumbuke kwamba Watanzania asilimia 80 tunaishi kwa kutegemea kilimo, tunategemea masoko mazuri ya kilimo na masoko haya tutayapata tu iwapo tutafanikiwa katika Serikali ya viwanda. Tutajenga viwanda vya kusindika mahindi, pamba, ufuta, alizeti, tangawizi na kadhalika. Hilo ninaliona hatujalifanyia kazi kwa namna ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, unaona kwamba mahitaji ya mafuta ya kula peke yake ni lita 400,000, hizi ni sawa na alizeti tani milioni mbili tu. Na hizi tani milioni mbili wana uwezo wa kuzalisha wakulima 4,000 tu, wanaweza kuzalisha mafuta yote ya kula...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuwe na utulivu ndani ya Bunge, Waheshimiwa tuwe na utulivu ndani ya Bunge.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi hiki, hizi lita za mafuta laki nne wanaweza kuzalisha wakulima 4,000 tu iwapo watajengewa uwezo. Lakini inasikitisha kuona hadi leo asilimia 70 ya mafuta ya kula tunaagiza kutoka nje, wakati wakulima wengi hawana fursa ya kuzalisha na kuuza kwa bei nzuri mazao yao kilimo, kwa hilo ni tatizo. Tatizo hili linatoka wapi...*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzunguzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Ridhiwani.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote na mimi ningependa kuanza kuunga mkono hoja, kwa sababu kama sikuunga mkono hoja, maana yake mipango hii ambayo tunahubiri hapa haitaweza kufanikiwa.

Pamoja na hilo na mimi nichukue nafasi hii kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais wangu kwa jinsi anavyofanya kazi kubwa, kazi inayoonekana, na kwamba sisi wengine tunapokwenda misikitini ni kumuombea Mungu tu, ili Mungu aendelee kumtia ujasiri, nguvu na maarifa zaidi katika kuendelea kuwapigania Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa leo, kubwa zaidi litakuwa ni ushauri tu, kwa sababu mambo mengi kule yanaendelea kufanyika. Nipende tu kuwaambia taarifa kwamba Wabunge watakaopenda kuungana nami, siku ya tarehe 22 Mheshimiwa Rais wetu mpendwa John Pombe Magufuli atakuwepo katika eneo la Halmashauri ya Chalinze akifungua viwanda, kuangalia barabara na maendeleo kwa ujumla wake, lakini pia atapata nafasi ya kuongea na Watanzania na kuwajulisha mambo mazuri yanayoendelea katika nchi ya Tanzania. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nawakaribisheni sana; na kwa kuwa siku hiyo itakuwa ni siku ambayo Bunge nafikili linakwenda katika *break* ya sikukuu, kwa hiyo, ni vema mkaja Chalinze ili mpate maneno mazuri ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu leo nianze katika eneo la uchumi wa viwanda. Mambo mengi yanafanyika, lakini mimi nina ushauri mmoja hasa katika eneo la biashara ya ngozi.

Mheshimiwa Waziri Mwijage anafanya kazi nzuri sana, lakini Mheshimiwa zile chapa zilizoletwa na zinazopigwa ubavuni kwenye mifugo yetu zinafanya ngozi za ng'ombe wetu zinaendelea kupoteza ubora. Na malalamiko yamekuwa mengi sana katika viwanda vya huko nje kiasi kwamba hata tunapohubiri kuweka viwanda ndani tutakabiliana na changamoto ya kwamba bidhaa tunazopeleka nje ziko chini ya kiwango kama kama kinavyotakiwa na hivyo tutakuwa tunakabiliana na changamoto ya kutonunulika kwa bidhaa zinazotoka Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu Wizara iangalie jinsi ya kuja na utaratibu mzuri hata kama ni chapa hiyo hiyo iwekwe, basi iwe chapa ambayo inakaa katika maeneo ambayo hayataweza kufanya athari kubwa katika ngozi za ng'ombe wetu na ubora ukapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo pia niendelee kuishukuru Serikali imefanya jambo kubwa sana katika kutoa ushuru wa mazao yanayosafirishwa. Hata hivyo, tunapozungumza kuondoa ushuru wa mazao pia tukumbuke kuongeza au kuweka mazingira mazuri ya upataikanaji wa mbolea zilizo nzuri, mbolea zilizo bora ili mazao yanayotoka yawe yenye ubora zaidi. Maana isiwe tu kwamba tunaondoa ushuru wa mazao lakini ule unaobakia nao unakuwa ni sehemu ya mzigo mkubwa kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua yako mapunguzo makubwa hasa katika tani ambazo ziko chini ya tani moja kwa yale mazao yanayotoka mashambani kwenda masokoni. Mimi najua kwamba leo hata kama mimi ninakwenda Mbeya siwezi kwenda Mbeya kuchukua tani moja ya mchele ili wananchi wangu wa Chalinze wakale mchele mzuri wa Mbeya. Kinachofanyika ni kwamba

nitakwenda Mbeya nitachukua tani zaidi ya nne ili nizipeleke katika masoko niweze kufanya biashara nzuri. Tutakapofanya majumuisho ningependa mliangalie tena jambo hili la upungufu wa ushuru, ule ambao unaozidi tani moja kwa sababu si kama kweli ile nia nzuri ya kusaidia wakulima wetu mauzo ya mazao yao wanaweza kufanikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuipongeza Wizara kwa kuendelea na mkakati wake wa kumalizia na kuendelea kulipa yale mafao ambayo yalikuwa yanatakiwa yalipwe kwa wale ambao wanapisha ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo. Mheshimiwa Waziri nimeona katika kitabu chako na nimekusikiliza vizuri katika hotuba ya bajeti kubwa, ni kweli kwamba mmedhamilia kufanya jambo hilo. Ninachokuomba Mheshimiwa Waziri baada ya kupitisha bajeti yako jambo hili la Bandari ya Bagamoyo mlifanyie liwe kipaumbele chenu kikubwa. Kwa sababu kama hamtofanya hivyo hii mipango yote mizuri, yale mafao yalishalipwa na mambo mazuri ambayo mmeyapanga hayatoweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika eneo la madini. Pamoja na juhudi kubwa ambazo zimeshafanyika, na juhudi kubwa ambazo Mheshimiwa Rais wetu anaendelea kuzifanya, ikiwemo kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata malipo ambayo yamekuwa yakikosekana katika muda wote. Mimi nina jambo dogo la kuomba Serikali yangu, Serikali ifanye haraka kuleta hiyo Sheria ya madini hapa tuifanyie marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka kipindi hiko kabla sijakuwa Mbunge iliundwa kamati hapa, kamati ya Mheshimiwa Bomani akiwepo kaka yangu Ezekiel Maige, walikwenda wakafanya uchambuzi na wakaja na mapendekezo, lakini sijui mapendekezo yale yamefikia wapi. Hata leo tunamuona profesa wangu, rafiki yetu Bwana Osoro naye amekuja na mapendekezo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiomba, tuielekeze Serikali yetu ilete mapema iwezekanavyo sheria hiyo ya madini ili tuweze kuiweka sawa na ili Watanzania wafaidike

na kile ambacho tumekuwa tunahisi kwamba kinapotea siku zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko hayo ya Sheria ya Madini yaje pia kutatua tatizo kubwa lililopo sasa hivi; kwamba kila mtu ana pembe, inapofika katika suala la kutoa haki ya matumizi ya ardhi ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takribani miaka miwili nimekuwa nikipiga kelele katika Bunge hili, lakini pia nimezungumza na Mheshimiwa Waziri na maafisa wa wizarani juu ya mgogoro uliopo katika kijiji cha Kinzagu na Makombe pale Chalinze. Unakumbuka niliwahi kusema hapa kwamba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ridhiwani unga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sugu, tunamalizia na Mheshimiwa Mabula.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa dakika kumi.

**MWENYEKITI:** Dakika tano.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, *okay,* ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza kabisa na kwa umuhimu, nimetumwa na wafanyabiashara wa Mbeya kuja kuiambia Serikali kwamba wanaiomba Serikali kwa *level* ya Mheshimiwa Waziri waende Mbeya mkae nao kikao kwa ajili ya kujadili masuala ya ulipaji kodi. Kwa sababu kumekuwa

na vikwazo vingi sana kiasi kwamba Mbeya tunashindwa kuzalisha wafanyabiashara mabilionea wa kutosha kama ilivyokuwa kwenye majiji mengine ikiwemo Dar es Salaam, Arusha na Mwanza kutokana na sintofahamu zinazotokana na *TRA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani unakuta mtu ana-*declear* labda mapato mwaka huu shilingi milioni kumi, mwakani ana *declear* milioni kumi *again*, mwaka unaofuata watatu aki *declear* milioni 30 wana *back date* wanamlazimisha kwamba wewe ulidanganya itakuwa hata kwa miaka mitatu, minne yote ulikuwa unaingiza milioni 30. Kwa hiyo, wana *impose* kinguvu kodi tofauti na mapato ambayo yule mfanyabiashara ame-*declear.* Hili ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango mfanyabiashara wa Mbeya akijenga nyumba nzuri inakuwa na madhara kwa sababu wanaenda ku *double* kodi kwenye biashara yake kwamba ulipata wapi hizi hela za kujengea hii nyumba. Ndio maana Mbeya tumechelewa kuwa *mansion* na mpaka leo hatuana *mansion* yako machache machache ndio kwanza yanaanza ukifananisha na majiji mengine na hii haiwezekani kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inasababisha wafanyabiashara wakifikia lengo *level* fulani ya mtaji inabidi wahame Mbeya waende kwenye miji mingine ili waweze kupata ustawi wa kibishara, lakini wakikaa Mbeya inakuwa migogoro na watu wa *TRA.*

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri kwa *level* ya Waziri wafanyabiashara wa jiji la Mbeya wamenituma kwamba wanataka wanahitaji uende mkakae ili mjadiliane na haya mambo kwa sababu yamekuwa hivi maiaka nenda miaka rudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bajeti, naunga mkono maoni ya upinzani, kodi ikiwa kero inachotakiwa ni kuiondoa sio kuibadilisha kiujanja ujanja kama mlivyofanya

kwenye masuala ya *road licence* kupeleka kwenye mafuta kiasi kwamba unawapa mzigo wananchi ambao wengine hawana magari kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni sahihi kwa mujibu wa Kambi ya Upinzani fedha hii ipelekwe katika maeneo hii shilingi 40 kama inalazimika kuongeza shilingi 40 kwa kila lita basi twende tuipeleke kwenye maji. Tukimaliza maji twendwe kwenye miundombinu ya elimu; yaani tunafanya vitu kwa miaka kwa *series,* miaka mitano maji, miaka mitano tunakuja kwenye miundombinu ya elimu ikiwepo nyumba za walimu na hata vyoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa katika Bunge hili na Taifa hili viongozi wakubwa wa Serikali wanazungumzia masuala ya kununua nini hizi *boeing* mpya *jetliner* sijui ziende wapi, lakini wanafunzi wetu wa shule za msingi hawana vyoo, wanakunya nje. Kwa hiyo hivi vitu vidogo vidogo ndio tunatakiwa tuviangalie kwanza kabla hatujaangalia mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madini na mimi nasema mikataba iletwe si ya madini tu, madini, gesi mikataba ya kununua ndege bombardier, nyumba za Serikali zilizouzwa mikataba yote iletwe ndani ya Bunge hili ili tuipitie upya. Tukisema mnasema tunampinga Rais hatumpingi tuko tayari kumsaidia na kumshauri lakini kwa sharti moja kama mimi binfsi Mjumbe wa Kamati Kuu sitaki uteuzi. Sitaki u-*DC,* sitaki sijui Ukuu wa Mkoa, sitaki Uwaziri ninachotaka afanye Mheshimiwa Rais ni kufungua mijadala atuache atusikilize mawazo yetu na ayafanyie, kazi hicho ndio kitu kibwa tunachokifanya, yaani sisi tunaweza tukamsaidia vizuri Mheshimiwa Rais tukiwa huku kuliko kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kirimanjaro au kuwa Katibu Mkuu wa Wizara fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunamuomba sana Mheshimiwa Rais achie mijadala tujadili vyanzo vya matatizo kwa kina, asitubane, hata kama matatizo hayo yatakuwa yamesababishwa na watu ambao sasa hivi ni Marais wastaafu wacha tujadili, ambaye yuko *clean* atabaki

kuwa *clean* ambaye ana mawaa basi Sheria itachukua mkondo wake ili tutengeneze *presidence* kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mwisho katika hizi dakika tano ni chache nikupongeze Dkt. Mpango, Mwakajoka amekuchana kiutendaji kazi, lakini mimi kwa tabia una-*smile* kidogo sasa hivi. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, ahsante Mheshimiwa Sugu, Mheshimiwa Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na inawezekana nikawa msemaji wa mwisho kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze tu kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri na za msingi ambazo anaendelea kuzifanya. Lakini natakata tu niwakumbushe ndugu zangu tulioko humu ndani na ndugu zangu Wabunge wa CCM wala msipate shida msishangae. Ni ajabu sana leo tunazungumza masuala ya bajeti ya kuwasaidia Watanzania watu bado tunawaza uchaguzi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana baada ya uchaguzi 2015 Wananchi waliamua kutenganisha. Kuongoza nchi si sawasawa na kuongoza *SACCOS.* Wananchi wa Tanzania walipoamau kuichagua CCM waliamini Mheshimiwa Magufuli atakwenda kuongoza Serikali. Serikali tunayoizungumza ni Serikali yenye mifumo inayoweka utaratibu wa kuwasaidia wananchi wanyonge maskini na wahali ya katikati. Sasa leo ndiyo maana yako makundi haya, uwezo wa kuongoza *SACCOS* na uwezo wa kuendesha nchi ni vitu viwili tofauti. Tunachangia bajeti mwaka 2017/2018 naomba niwakumbushe...*(Makofi)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MBUNGE FULANI:** Hakuna taarifa.

**MWENYEKITI:** Nilishatoa maagizo sipokei taarifa tena, kwa upande wowote. *(Makofi)*

**MHE. STANSLAUS S. MABULA**: Naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri ...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Rais akikatwa jino huku tunaambiwa kwamba hatumuheshimu, mbona yule kule anasema Magufuli tu?

**MHE. STANSLAUS S. MABULA**: ...tunapokwenda kwenye utaratibu wa ukusanyaji wa kodi, ziko kodi ambazo zimeandikwa kwenye s*chedule* ya leseni ziko biashara ambazo hazijatambulika. Biashara hizi zinazifanya Halmashauri zinazokusanya kodi ziwe na tabia tofauti tofauti. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, mnapokwenda kwenye kipengele hiki tuangalie ili kuweka uwiano ambao utakuwa unafanana karibu kwenye Halmashauri zote nchini. Lakini nikumbushe hapa, nimshukuru tena Waziri pamoja na Mheshimiwa Rais na sisi Wabunge sote wa CCM ambao tulikaa hapa kupanga kuhakikisha wafanyabiashara ndogo ndogo wanatambuliwa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo rafiki yangu *Comrade* Mwakajoka amenishangaza sana, anataka kuwatisha umma wa wafanyabiashara ndogo ndogo nchi kwamba wataanza kulipa kodi, kodi ambayo ukikisoma kitabu hiki hakuna popote ilipoandikwa Mmachinga, mama lishe, mama ntilie, anayeuza mitumba, anayeuza hiki kwamba anakwenda kutambulika na kulipa kodi. Wakati tunasimama hapa tunawapigania wanyonge hawa na mimi najua ndugu yangu Mwakajoka hili kwenu ni pengo upande mwingine hili ni pengo, kwa sababu hawa wafanyabiashara ndogo ndogo ndiyo walikuwa wanatumika isivyo kuhakikisha wanakuwa mbele kusaidia watu kupita mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amezunguka nchi nzima ameona machinga wanavyopata taabu, kaona mama lishe wanavyopata taabu, leo amewatambua na wao watambulike na wao wawe rasmi waache kufukuzwa na mabomu, waache kupigwa, waache kunyanyasika leo tunasema wanatengenezewa kodi ili waanze kuogopa mapema. Ni lazima tuwe na shukrani kwenye mambo yasiyokuwa yanafaa, na mimi nilitegea sana kaka yangu Sugu hata Waitara wangekuwa wakwanza kupongeza kwenye utambuzi wa wafanyabiashara ndogo ndogo maana wao ndio wanaathirika pale sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda ni mfupi lakini nizungumze suala la kodi ya majengo. Wakati Serikali ilipoingilia suala la kukusanya kodi za majengo mwaka wa jana; zilipoondolewa kwenye Halmashauri haraka haraka wote tulifikiria kwamba Serikali imekosea. Nataka niwaambie, Mheshimiwa Rais alitazama mbali na akafikiria jambo la mfano mzuri sana.

Leo tunawaza habari ya vyanzo vipya vya mapato, ninyi nyote ni mashahidi nyumba ambazo zilikuwa hajafanyiwa *evaluation* zilikuwa hazilipi kodi ya pango zilikuwa hazilipi kodi hii muda mrefu. Leo pigia hesabu nyumba ngapi ambazo hazijafanyiwa *evaluation* katika nchi hii zitalipa kodi? Na leo zinakwenda kulipa kodi ambayo itakuwa inakwenda kusaidia kwenye nyanja mbalimbali tunazosema kuongeza dawa, barabara lakini kuimarisha vituo vyetu vya afya na kadha wa kadha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndiyo maana ilikuwa ni lazima hii kupigiwa kelele, Halmashauri zimetumia vibaya sana fedha hizi na mfano mzuri ni Arusha. Arusha imekuwa Jiji ililokuwa na tofauti Diwani akienda kwenye kikao kimoja analipwa zaidi ya shilingi 800,000; lakini ukienda Mwanza na maeneo mengine anambuliwa shilingi 200,000 iliyoko kwenye utaratibu. Ni lazima tusimame kuikusanya fedha ya Serikali ikawasaidie wananchi walio wanyonge. Kwa nini tusiipongeze Serikali?

Sote tunafahamu na mimi niwakumbushe huwezi kuwa ndani ya nyumba hii kikiamuliwa kitu wewe ukasimama pembeni, wewe ni sehemu ya maamuzi yote yanayofanyika kwenye nyumba hii na Watanzania wanalijua hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tukubali. Tunafahamu, kodi ya mabango pia imekwenda Serikalini na mimi niwashukuru Mheshimiwa Mpango naamini mmetengeneza utaratibu sahihi ambao fedha hii mtakapoikusanya kwa pamoja itakuwa inarudi kwenye Kata kwa wakati, kwenye Halmashauri zetu, kwenye Miji, Majiji na Manispaa ili iweze kufanya kazi yake sawa sawa. Tunafahamu jukumu la kupeleka asilimia tano kwa wanawake na vijana ni la Serikali ambao iko chini ya Chama cha Mapinduzi na hii iko kwenye Ilani tutatekeleza. Limejadiliwa suala la milioni hamsini hapa; wenye Ilani Chama cha Mapinduzi milioni 50 tumeahidi ndani ya miaka tano kwa nini mnataka tupeleke leo? Mimi ninayoimani kwamba fedha hizi zitakwenda, na zinatengenezewa utaratibu ili tuweze kufikia malengo tuliyokusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena, suala la kuongoza nchi lina tofauti kubwa sana na kuongoza kitu kingine cha kawaida ili kufikia malengo ya Watanzania. Mungu awabariki sana, ahsanteni kwa kunisikiliza. Naunga mkono hoja asilimia 100. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, orodha yetu imekwisha, niwashukuru tu kwa michango. Lakini Mheshimiwa Waziri hili la vitambulisho vya Wamachinga pesa ziko hapa, Kenya sasa hivi wanakusanya trilioni mbili na nusu kwenye *informal sector.* Hakikisha idara yako wanafanyakazi vizuri utapata pesa za maji kwenye *informal sector. (Makofi)*

Baada ya maneno haya naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12:00 Joni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 20 Juni, 2017 Saa Tatu Asubuhi)*